ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	N/ Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28. Mhe. Ali Mzee Ali	Uteuzi wa Rais
29.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
30.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
31.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
32.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake

39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
55.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
57.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
58. Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini
59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
62.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
63.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
65.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
66.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
67.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
68.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
69.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
72.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75 Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim **Katibu wa Baraza la Wawalishi**

Kikao cha Ishirini – Tarehe 15 Julai, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mahmoud Mohammed Mussa) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 117

Wastaafu wa JWTZ Kuajiriwa Katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

Mhe. Viwe Khamis Abdalla (Kny: Mhe. Ussi Jecha Simai) – Aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa tumekuwa tukishuhudia wastaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) wakiteuliwa kushika nyandhifa mbali mbali za uongozi kwenye Idara mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(a) Mhe. Waziri, ni sababu gani za msingi zinazopelekea hali hii kutokea.

(b) Je, Serikali haioni kwamba kufanya hivyo ni kuwavunja moyo Makamanda wetu walioanzia kwenye Idara hizo.

(c) Kwa kuwa wastaafu hawa wa Jeshi tayari walikwisha maliza muda wao wa kufanya kazi za uaskari. Je, Mhe. Waziri huoni kwamba wanapewa nafasi hizo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wakiwa hawana uwezo tena wa kuleta fikra za mabadiliko ya maendeleo ndani ya Idara zetu.

(d) Je, Mhe. Waziri huoni kwamba kuendelea kuwapa nafasi wastaafu ni kuzuia nafasi za ajira mpya kwa vijana wetu waliomaliza elimu zao na kuendelea kuzurura bila ya kuwa na kazi.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 117 lenye vifungu (a) , (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba wapo baadhi ya Wastaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) walioteuliwa kushika nafasi mbali mbali katika idara zetu Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

(a) Sababu za msingi zilizopelekea hali hiyo ni kupata uzoefu na utaalamu wa kijeshi ambao unahitajika katika idara hizo.

(b) Hatua hii haina lengo la kuwavunja moyo Makamanda wetu isipokuwa kuongeza nguvu katika vikosi hivyo. Kwa mfano, Idara yetu ya Valantia bado ni changa, Makamanda kutoka JWTZ wamesaidia sana kuiwezesha idara hiyo kuwa na mfumo wa kisasa na wa kijeshi.

(c) Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo awali kwamba wastaafu hao huteuliwa kutokana na utaalamu na uzoefu wao. Hupewa nafasi husika kwa mikataba ya muda maalum kama vile wastaafu wa taasisi nyengine wanavyopewa mikataba kwa utaalamu wao.

(d) Mhe. Mwenyekiti, ajira za wastaafu hao ni za mikataba ya muda si ajira ya kudumu, kwa msingi huo wastaafu hao hawazuii nafasi mpya za ajira.

Kwa sasa tuna wastaafu wawili tu ambao wapo kwa mkataba, mmoja yupo JKU na mwengine yupo katika Kikosi cha Valantia, ambao wana uzoefu katika masuala ya kijeshi.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia askari wetu wanapofika umri wa kustaafu huwa wamekomaa kabisa katika mambo ya kijeshi. Lakini wengine hupewa katika nafasi za uongozi kama Mkuu wa Mkoa na kadhalika na kule ana itikadi zake ile ile ya kijeshi.

(a) Kufanya hivi hatuoni kuwa kila mahala panahitajika taaluma maalum ya kuongoza ni lazima awe jeshi.

(b) Tuna matatizo makubwa ya wafanyakazi katika idara kadhaa, kama walimu wa sayansi, madaktari na kadhalika na hao hustaafu mbona wao hawarejeshwi tena kazini wakapewa sehemu nyengine kama wanavyofanyiwa majeshi.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, kama sijampata vizuri naomba baadae aniulize tena Mhe. Mwenyekiti, lakini nataka kusema kwamba sababu za msingi hawa watu tunawachukua kuwapeleka katika idara zetu kuongeza uzoefu na kuwapa taaluma. Taaluma ya kijeshi siku hizi ni ya kisasa, ya kitaalamu. Tunawachukua wale wataalamu utaona wako maafisa kwa sababu maafisa wale wana taaluma maalum sio kama wanafunza gwaride tu na nidhamu, wanawafunza mengi kabisa mambo ya kijeshi.

Sasa lengo letu kwa sababu vikosi vyetu vichanga basi hii taaluma tuipate moja kwa moja. Suala la nidhamu linahitajika kote kama ulivyosema kwa walimu wengine kama wa sayansi na wengineo basi na huko kwenye kijeshi pia nidhamu ya hali ya juu. Lakini atakubaliana na mimi kwamba wenzetu askari nidhamu yao ya kiaskari na kidogo inakuwa mia juu ya mia, kama haiku mia juu ya mia basi kuna matatizo yanarekebishwa ya kiaskari.

Nam. 134

Kuondoshwa kwa Pampu ya Maji

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny: Mhe. Salum Amour Mtondoo) - Aliuliza:-

Kwa muda mrefu sasa wakaazi wa Shehia za Mwanyanya na Sharifu Muussa wamekuwa wakikosa huduma ya maji safi baada ya pampu ya maji iliyokuwa katika Chemchem. Chemchem ya Mwanyanya kutolewa na kuwasababishia usumbufu mkubwa.

(a) Ni sababu gani iliyofanya kuondoshwa kwa pampu hiyo.

(b) Mhe. Waziri utakubaliana nami kuwa kitendo cha kutolewa kwa pampu hiyo na kukosa huduma hiyo muhimu katika maeneo hayo kinawafanya wawe wanyonge katika nchi yao.

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha wananchi hao wanafaidika na huduma hii muhimu kwa maisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 134 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, kianzio hicho cha Mwanyanya kitaalamu hakitakiwi kufungwa pampu kwa kuhofia kuathiri uzalishaji wa chemechem hiyo ambayo inajitegemea kuzalisha maji bila ya kutumia pumpu.

(b) Kwa kutilia maanani umuhimu wa suala la maji safi na salama kwa wananchi wa Zanzibar wizara yangu imeamua kuchukua hatua za haraka za kuliondoa tatizo hilo kwa kuwaunganisha na mtandao wa mradi wa Mkoa wa Mjini Magharibi.

(c) Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu ina mpango wa kununua mabomba madogo madogo kwa ajili ya kuwaunganisha wananchi wa karibu na bomba hilo ili kupatikana huduma ya maji safi na salama baada ya kupatikana kwa mabomba hayo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, sivyo swali lilivyoulizwa na jawabu lake lilivyopatikana. (*Kicheko)*

Mhe. Mwenyekiti: Hebu ulisa tena Mhe. Jaku ili Mhe. Waziri aweze kufahamu na kuweza kujibu vizuri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ni sababu gain iliyofanya kuondoshwa kwa pampu hiyo. Kwa maana hiyo nikija nikimuuliza swali la nyongeza hatotoa jawabu. Kina cha maji kwa kuondosha pampu maji yanatosheleza ndio wakaondosha *water pump* pale, kwa hivyo bora aliwasilishe swali kabla ya kumuuliza swali jengine.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa ungelikaa kwenye hiyo spika ili uweze kueleweka.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba hili swali aliangalie kwanza alivyoulizwa na majibu yake.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi ya kuliweka sawa au kuliboresha jibu ambalo Mhe. Naibu Waziri amelitoa.

Jibu alilotoa Mhe. Naibu Waziri ni sahihi, Naibu Waziri alisema Chemchem ya Mwanyanya inapeleka maji bila ya kutumia pumpu na hiyo ni kweli. *Pump* iliyowekwa pale ni ya akiba inaonekana haikutumika kwa muda mrefu na ndio maana ikaondolewa, wala hakuna nia ya kuirejesha mpaka pale ambapo kina cha maji kitakapopungua sana, kwa sababu safari hii kimepungua sana nab ado

maji yamekwenda Mji Mkongwe hata kama ni kidogo hayakutaosha, lakini yamefika mpaka Mji Mkongwe. Kwa hivyo, *pump* imeondolewa kwa sababu haina haja na haitumiki.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwa maana hiyo kuondoshwa kwa chemchem ile

Mhe. Mwenyekiti: Swali jengine huwezi kuendelea na swali hilo tena.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, sisi hapa tumechukua dhima kwa wananchi, sasa utaratibu unavyoulizwa ujibu unavyoulizwa, huu umekuwa ni mzigo kwa wizara hii kuuliza swali jengine ukajibiwa vyengine.

Nam. 135
Kufanyiwa Matengenezo Chemchem ya Mwanyanya

Mhe. Jaku Hashim Ayoub (Kny: Mhe. Salum Amour Mtondoo) - Aliuliza:

Chemchem ya Mwanyanya ni moja ya vianzio vya maji tegemeo hapa nchini. Chemchem hiyo ilijengwa mwaka 1923 na jengo lake limeshachakaa kutokana na kutokufanyiwa matengenezo. Jambo hilo linapelekea mazingira ya eneo hilo kuwa hatarishi kutokana na usalama mdogo kwa watumiaji maji hayo.

(a) Je, Wizara ina mpango gani wa kulitengeneza jengo hilo na kuyalinda mazingira ya hapo.

(b) Kwa kuwa Mhe. Waziri uliagiza kutengenezwa nyumba ya Walinzi wa Kituoni hapo mnamo mwezi wa Januari, 2011; Je, hivi sasa ni hatua gani za awali zimeanza kuchukuliwa na Wizara yako.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 135 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, jengo hilo la kukusanyia maji ya chemchem kabla ya kutiririka wenyewe kwa kufuata mteremko kuelekea Saateni, ni kweli kuwa linahitaji kufanyiwa maboresho ya kupakwa rangi, maana rangi yake ya asili imechakaa. Kwa kulitilia maanani suala la kuliboresha jengo hilo na kuweza kulirudisha katika hali ya kuridhisha na ya kupendeza.
(b) Wizara yangu tayari imeshaanza kulifanyia matengenezo banda hilo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, atakubaliana nami Mhe. Naibu Waziri tokea mwaka 1923 mpaka hii leo ndio lifanyiwe matengenezo. Haoni ni kipindi kirefu hicho, na matengenezo gani yaliyoanza ili wananchi wa Bububu na Mwanyanya waweze kujua.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimekiri kwamba jengo hilo linastahiki kufanyiwa marekebisho. Kwa hivyo, ni kama halijafanyiwa na ni kweli halijafanyiwa lakini nimekiri kwamba tutalifanyia marekebisho ikiwemo kulipaka rangi na mengi mengineyo.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa na mimi kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali jengine la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, tokea kituo hiki cha maji kilipoasisiwa kwenye chemchem hii ya maji na serikali kwenda kuweka mitambo yake kwa ajili ya kusukuma maji ni miaka mingi sana, jengo hili kama aliavyosema Mhehsimiwa halijatengenezwa, lakini hata kulijengea uzio lile jengo na wakati ni sehemu ambayo inatoa maji na ni tegemeo kwa Zanzibar na ni eneo ambalo lipo karibu na wananchi.

Je, wizara hii itachukua hatua gani ya kuweka uzio na kuhifadhi zaidi lile eneo kwa ajili ya kuhifadhi maji na kupata tegemeo la maji Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Mwenyekiti, jengo lilijengwa mwaka 1923, lakini jengo hili tumelikarabati kila baada ya miaka miwili. Nilipokwenda kutembelea kituo nikalikuta hali sio mbaya kama inavyozungumzwa, kweli halina rangi imechujuuka nikaagiza lipakwe rangi upya kwa sababu halipendezi.

Lakini suala kwamba tokea mwaka 1923 halijakarabatiwa sio sahihi na ningemuomba Mhe. Subeit Khamis pengine akalipitie hili jengo na yeye akalijua lilipo na limekaa vipi. Kwa sababu hivyo alivyozungumza sio sahihi.

Lakini suala la uzio nakubaliana na yeye kwa asilimia mia moja, kwamba kweli ni muda mrefu hatujajenga uzio. Hatukujenga uzio kwa sababu wakati ule mavamizi yalikuwa hayapo, lakini sasa eneo lile linavamiwa kweli pamoja na kwamba linalindwa na majeshi na tuna nia ya kujenga uzio katika kipindi hiki cha bajeti.

Nam. 125

Ulipwaji Wa Fidia Kwa Wananchi Wa Jimbo La Uzini

Mhe. Ashura Sharif Ali (Kny: Mhe. Mussa Khamis Silima) - Aliuliza:-

Wakati wa Ujenzi wa barabara ya Dunga Mitini hadi Kinyasini vipando vya miti ya kudumu katika mashamba ya wananchi wa vijiji vya Mgenihaji, Uzini, Mitakawani, Tunduni, Mchangani na Mkiwa viliathiriwa na ujenzi huo na hadi leo hii hawajalipwa fidia ya miti yao.

(a) Je, ni wananchi wangapi walioathirika na tukio hilo.

(b) Kwa kuwa siku nyingi zimepita bila ya Serikali kuwalipa fidia wananchi hao. Serikali ina mpango gani kuhusiana na jambo hilo na inatoa wito gani kwa wananchi hao wanyonge.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 125 lenye vifungu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana Mhe. Mwakilishi kwamba wakati wa ujenzi wa barabara kutoka Tunguu kupitia Dunga Mitini hadi Kinyasini, wananchi wengi wa vijiji vilivyopita barabara hiyo yenye urefu wa kilomita 26.8 wakati ikiwa inajengwa na Kampuni ya SS. Mehta ya Kenya waliathiriwa na ujenzi huo. Napenda nikiri hadi leo hii kuna baadhi ya wananchi hawajalipwa fidia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa majibu:

(a) Mhe. Mwenyekiti, jumla ya wananchi 735 walioathirika na tukio hilo baadhi yao wamelipwa fidia na wao kwa ujumla wao walikuwa wakidai jumla ya shilingi 83,404,587.50. wananchi hao waliobaki wanaodai madai yao ni kama ifuatavyo kwa mujibu wa idadi na sheria zao:-

- Shehia ya Kinyasini 55
- Shehia ya Kisongoni 51
- Shehia ya Pangeni 90

- Shehia ya Kilombero 99
- Shehia ya Mchangani 81
- Shehia ya Tunduni 52
- Shehia ya Mitakawani 51
- Shehia ya Uzini 64
- Shehia ya Mgeni Haji 83
- Shehia ya Dunga bweni 109

(b) Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa wizara inazo taarifa za vipando vyote vilivyoathirika na tayari vimekwishafanyiwa tathmini, natoa wito kwa wananchi hao wawe na subira wakati wizara yangu inafuatilia kwa karibu mafao ya waathirika hao. Nataka waamini kuwa haki yao haitapotea.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wizara yako imekuwa ni tabia yake sasa kila inapoanza ujenzi kila sehemu ambapo inafanya ujenzi wa barabara basi huwa inawapotezea wananchi wake ama majumba au vipando vyao na kutokuwalipa. Je, wizara yako ina mpango gain wa utaratibu mzuri wa kuwalipa kwanza wananchi hao bila ya kuwaharibia.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, katika ujenzi wa barabara mara nyingi maeneo yanayopita barabara kunakuwa na majengo na vipando. Utaratibu tuliouweka hivi sasa kwamba kwa upande wa majengo hatutovunja jingo la mtu yeyote kabla ya kumlipa fidia ili kuweza kuruhusu barabara ipite.

Mhe.Mwenyekiti, kwa upande wa vipando naomba niendelee tena kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu pamoja na wananchi wenzetu wa Zanzibar. Umuhimu wa barabara unakuwa ni umuhimu wa pekee, serikali baadhi ya wakati inakuwa hatujatenga fedha kwa ajili ya kulipa fidia kwa watu wote. Lakini kwa bahati mbaya au nzuri kuna miradi ambayo tumepata ufadhili, wafadhili wale ili tuendane nao tusije tukakosa yote mawili, hivyo inatulazimu tuwaombe nusura wenzetu hawa wenye vipando watusubirie.

Napenda nimhakikishie Mhe. Mwakilishi na Baraza lako tukufu wizara yangu kufanya hivyo haifanyi kwa kutaka tunafanya hivyo kwa ukosefu wa fedha, lakini tunamhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba imani yetu na madhumuni kuhakikisha deni hili tunalilipa kadiri ya upatikanaji wa fedha unavyoruhusu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, wakati wa ujenzi wa barabara mbali mbali za Unguja na Pemba Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano hupokea tathmini ya vipando kutoka katika Wizara ya Kilimo, tathmini ambazo huzingatia vipimo vya miaka ya nyuma sana na havilingani na bei ya sasa ya vipando hivyo na hivyo hupelekea migomba, mihogo na hata minazi kulipwa kwa fedha ndogo sana ambayo haisaidii kuathirika.

Je, serikali kupitia wizara hii ina utaratibu gani sasa wa kuamua kuangalia upya utaratibu wa fidia kulingana na hali halisi ya maisha ya sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na mawazo ya Mhe. Mjumbe ya kwamba katika ulipaji wa fidia wizara yetu hupokea taarifa ya tathmini kutoka kwa wizara au taasisi husika. Nakubaliana naye kwamba, kwa upande wa vipando huwa tunapokea tathmini Wizara ya Kilimo na upande wa majengo huwa tunapokea tathmini kutoka Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.

Mhe. Mwenyekiti, yawezekana kwamba ikawa gharama hizo ni ndogo au fidia hiyo ni ndogo kama alivyotoa Mhe. Mwakilishi mawazo yake, lakini kwa kuwa wizara yetu sio inayofanya tathmini basi naomba tumuombe Mhe. Mwakilishi kwamba kilio chake hiki serikali imekisikia na ninaamini serikali itakaa itafakari na kwa kuwa serikali ina malengo ya kuwatumikia wananchi wake nadhani sio wazo baya serikali italipokea.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru. Katika suala hili la utengenezaji wa barabara kwa maendeleo kuna barabara inayotoka Konde kuja Wete. Ilipokuwa ikitengenezwa kuna watu kumi ambao nyumba zao ziliharibika vibaya sana mpaka wengine kuzihama nyumba hizo katika eneo la Kinyasini na wizara kila siku wanapokwenda kudai haki yao huambiwa njooni kesho vocha tayari lakini hawajalipwa wakati wengine wote wameshalipwa.

Je, wizara haioni kuwa kwa sababu wote wameshalipwa na wale wengine hawana pa kukaa ipo haja ya lazima kwa watu hao kuwaondolea matatizo yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, katika barabara ambayo anaisema Mhe. Mwakilishi ni kwamba kuna nyumba ambazo tumezilipa fidia, nyumba hizi ni zile ambazo tumeziondosha ili kupitisha barabara hii inayoendelea kujengwa. Nyumba ambazo zimeathirika kwa ujenzi huu tunaendelea kuzifanyia tathmini na ni kweli wadai hao wanakuja, lakini kwa kuwa tunaendelea kufanya tathmini na fedha hizo

hazikuwa zimetengwa kama zile ambazo zilikuwa zimo ndani ya eneo ambalo barabara hiyo inapita, naomba nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba baada ya kwisha kuridhika na tathmini hiyo tutaendelea kutafuta fedha tutawalipa wadai hao.

HOJA ZA SERIKALI

Makadiro ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 – Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe leo kabla hatujaanza kuchangia nilitakiwa nitoe maelezo kidogo. Tunapomaliza kujibu maswali pamoja na kuulizana huwa wajumbe tunatoka kwa wingi kwenda katika sehemu za chai, sasa tunaombwa utokaji wetu na angalau tuwe kumi kumi basi tusizidi hapo ili shughuli za Baraza zisije zikasita humu ndani. Kwa hivyo, tunaombwa tufuate utaratibu huo.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa asubuhi hii ya leo kunipa nafasi ya kwanza kuchangia katika wizara hii kubwa ya elimu.

Kwanza namshukuru Allah kwa kutuweka hai, kutupa uzima na taufik ya kuzungumza katika Baraza lako tukufu asubuhi hii ya leo. Ilivyokuwa hii ni siku ya Ijumaa naamini wizara hii imepata baraka ya aina yake kujadiliwa ndani ya siku ya Ijumaa.

Mhe. Mwenyekiti, kama inavyoitwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali madhumuni makubwa ya wizara hii ni kuelimisha jamii kuanzia wale wadogo kabisa mpaka wale ambao hawakubata bahati katika udogo wao kuelimishwa. Kwa hivyo, ndani ya mchakato wote huo kuna kazi kubwa ambayo ilitarajiwa kufanyika. Elimu katika nchi yoyote ile ina umuhimu wa iana pekee katika kupeleka mbele ile nchi, kuidumisha au kuirudisha nyuma. Moja katika vigezo vizuri vya maendeleo ya nchi ni kutizama jinsi gain jamii ilivyoelimika na inavyoweza kutumia taaluma ile katika kusukuma mbele maendeleo ya nchi.

Kwa hivyo, wizara hii isionekane kwamba kazi ya ni kusomesha tu kama utaratibu, laa! Kazi yake hasa ni kusomesha kwa madhumuni ya kuisaidia nchi kuweza kuleta maendeleo, ile elimu iweze kuwa na maana kwa ile nchi, yaani tuwe na elimu ambayo itasaidia kusukuma gurudumu letu katika kuisaidia nchi kupata maendeleo, kuondoa umasikini, kuongeza ajira na kadhalika. Kwa hivyo, yote haya lazima malengo ya elimu yaweze kufikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, miaka mingi iliyopita nilikuwa Wizara ya Elimu sasa katika baadhi ya mafunzo tuliyohudhuria alihudhuria mwanachuoni mmoja wa elimu kutoka Marekani, Marekani wao katika miaka hiyo waliona kwamba nchi ni kubwa lakini wanapitwa na nchi ndogo ya Japan katika maendeleo yake na teknolojia. Kwa hivyo, wakawakusanya wanavyuo wote wa elimu, yaani wale *educationalist* na kuwaambia hebu tuleteeni hivyo vitabu vyetu na tuangalie mitaala yetu ikoje hata ikawa sisi Japan inatupita na ukubwa wetu. Kwa hivyo, mwaka ule wakakubaliana kubadilisha mitaala yao yote ya nchi nzima ili kwenda sambamba na teknolojia mpya na na kuweza kuleta maendeleo.

Sasa nasema kwamba hii Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tusiwe tunakwenda na kurudi, lakini tulenge katika kuona kwamba je, vijana wetu tunawapa elimu ambayo inastahiki kupewa ili kuweza kuleta yale matumainio ya wananchi.

Lakini la pili ni kwamba baada ya kumaliza mwanafunzi yule muhula wake wa skuli kama ni sekondari au chuo kikuu na kwengineko, ana uwezo wa kiasi gani wa kuitumikia nchi, yaani kutumia ile elimu yake ya kuweza kutumikia nchi.

Mhe. Mwenyekiti, profesa huyo kwa siku hiyo aliagiza sponji dogo akamwambia mmoja kati yetu hebu litie ndani ya maji, akalitia ndani ya maji, sasa akamwambia litoe, lilipotolewa lina uzito kweli kweli lakini akamwambia haya likamue, maji yote yakapukutika na sponji likabakia tupu. Akamwambia hivi ndivyo Afrika inavyosomesha wanafunzi wake na ndio maana tukadumaa. Anapewa mambo weee hata akimaliza skuli hana uwezo tena wa kufanya lolote kwa sababu ile elimu amepewa iliyokuwa haina mwelekeo.

Mhe. Mwenyekiti, tunaipongeza sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuona baadhi ya mambo haya kuanzisha skuli za ufundi, vyuo vya amali, lakini vile vile kama nilivyosema vinafanya kazi yake au vipo tu. Lazima tufanye tathmini hivyo vyuo vya amali tulivyoanzisha, skuli za ufundi tulizoanzisha, zinafanya kazi yake inavyopaswa au vipo tu kwa jina, hili ndio jambo muhimu. Tukenda miaka na miaka tukawa tunachukua ni *formality* tukenda na kuingia skuli na kurudi haitatusaidia kitu.

Matatizo yetu mengi yatabaki pale pale na vijana wetu watakuwa wakihangaika kwa sababu hawana elimu ya kujituma, hawana elimu ya kujiendeleza.

Mhe. Mwenyekiti, nikiingia kwenye hichi kitabu kwanza nashukuru kwamba mwaka huu angalau kwa kila idara imeoneshwa itapewa kiasi gani kwa kazi za kawaida na baadae kuna miradi ya maendeleo. Hili ni jambo la faraja kwa

sababu mimi binafsi nilikuwa nikifuatilia vitabu vya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali miaka mingi bajeti ilikuwa ikitolewa kwa jumla. Lakini bado pana hatua ya kuchukua.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu wamefikia kubagua gharama ya mwanafunzi katika skuli ya msingi ni kiasi gani, gharama ya mwanafunzi katika skuli ya sekondari ni kiasi gani. Sasa tutakapofanya uchambuzi huo ndio tutaona jinsi gani tunavyowalipa kidogo walimu wa sayansi, jinsi gani hatuna maabara, jinsi gani hatuna vifaa vya sayansi kwa sababu hatuna ile bajeti inayopelekea kupata vile vifaa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nilishtuka niliposikia Idara ya Utumishi na Uendeshaji imepewa bilioni 24 kwa Unguja na bilioni 8.6 kwa Pemba, nikasema fedha zote hizi zinakwenda wapi, huko ndani nilipoingia nikaona kumbe walimu wote wameingizwa humu. Hii kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali si sahihi kwa sababu katika wizara hii kuna maeneo mawili, kuna eneo la ofisi na eneo la skuli. Walimu walitarajiwa wawekwe peke yao tujue je, gharama ya uendeshaji wa elimu kwa eneo la ofisi ni kiasi gani na kile wanachopewa walimu ni kiasi gani. Lakini kuchanganya walimu na wafanyakazi kila kitu ofisi pamoja haitoi taswira halisi ya namna gani walimu tunavyowachangia katika mishahara yao, tunavyowachangia katika mapato yao.

Mhe. Mwenyekiti, inawezekana kuna kitu kinazibwa hapo, kwa hivyo tunamuomba sana Mhe. Waziri aje atueleze ni kwa nini walimu wakachanganywa na wizara katika Idara moja ya Utumishi na Uendeshaji wakati wao walimu wana Idara ya Msingi na Maandalizi, Idara ya Sekondari. Kwa nini wasiingizwe katika idara zao mishahara yao na hii wizara ikawekwa peke yake tukajua kwamba wizara inatumia kiasi hichi cha bajeti ya wizara na huku maskulini kimepelekwa kiasi hichi. Hapa ndio utakapojua uchambuzi wenyewe, tukiendelea kupanga bajeti namna hii haisaidii wizara wala haitusaidii sisi katika uchambuzi tutakuwa tukihangaishana tu. Kwa hivyo, tunamuomba sana Mhe. Waziri aje atueleze kashindwa kwa kiasi gani kupanga matumizi ya kawaida asiyaingize katika idara yake inayohusika.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni chuo kikuu cha *SUZA.* Hapa tumepewa bajeti yake ni bilioni 3 ni asilimia 6.6 ya bajeti ya wizara. Kule kunatumika vigezo gani vya kutoa bajeti. Ndio yale niliyosema kwa sababu hatukupanga katika mtandao mbali mbali za elimu tunakuwa tunapeleka tu. Kuna manung'uniko mengi namna gani *SUZA* inavyokwenda, lakini kulitumika kigezo gani cha kuwapa bilioni 3 kamili isizidi hata senti moja. Mhe. Mwenyekiti, tunamuomba Mhe. Waziri aje atueleze.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo *SUZA* nina suala moja jengine. Sasa hivi chuo kikuu kinaanza kupata majengo yake Tunguu lakini kimesambaa sana Mjini Magharibi kutoka Majestic mpaka Beit el Ras. Mimi namuulizal Mhe. Waziri kusambaa huku kunatarajiwa kumalizwa lini. Lini wanafunzi na walimu wa chuo kikuu cha *SUZA* wanatarajiwa kukaa katika paa moja.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar kwa siku za karibuni tumezoea kufuta majina yetu ya kihistoria. Mimi namuuliza Mhe. Waziri yeye yuko tayari kuturejeshea jina letu la Beit el Ras kama chuo cha ualimu wakishapata majengo yake. Mhe. Mwenyekiti, sisi tunavyoelezwa na wazee wetu kwamba chuo cha ualimu cha Beit el Ras kina historia kubwa sana toka wazee wetu, kilianza Dole kikavutwa kikaja Beit el Ras.

Kwa hivyo, ile kwamba chuo cha ualimu kiko Beit el Ras ni suala la kihistoria kwa Zanzibar. Sasa je, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali nayo inataka kufuta jina hili kama ilivyofuta Wizara nyengine Mambo Msiige. Namuomba Mhe. Waziri aje atueleze na yeye kama anataka kuifuta historia ya chuo cha ualimu cha Beit el Ras. Bila ya hivyo tunamuomba sana chuo kikuu cha *SUZA* kikishajengwa kule majengo yake Tunguu basi wahame na vitu vyao chuo cha ualimu kirudi pale.

Maana yake leo unasema walimu wanasoma Chuo cha Kiislam si itatisha ulimwengu hiyo kwamba walimu wanasoma kwenye chuo hicho. Sasa hailingani kwamba walimu wakasome Chuo cha Kiislam au kibadilishwe jina. Hawa wanapo pahala pao pa asili Beit el Ras.

Mhe. Mwenyekiti, moja katika ishara kubwa inayopimwa kwamba elimu ina mafanikio ni matokeo ya mitihani. Muda mrefu sana tulikuwa tunapiga kelele kwamba huu mtihani wa kidato cha pili tunaofanya sisi wenyewe basi matokeo yake yatoke yaonekane, wayaone wenyewe, wayaone wazee wao, wayaone walimu. Lakini tunaendelea na programu ile ile ya kutaja majina tu, hii inatuathiri, halafu tunafika mtihani wa kidato cha nne ndio maana tunaripua.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninayo hapa matokeo ya mwaka 2009 na 2010 ya kidato cha nne na sita ni hatari. *Division* inayopatikana sana ni *division III* na *division 0* ingawa hapa ikitajwa kwamba watu wamefaulu. Lakini mimi nasema kwamba kufaulu maana yake ni uwezo wa kuendelea kuchupa ngazi, sasa ikiwa hawezi akachupa ngazi kafaulu vipi. Mfano matokeo ya kidato cha nne yanatoka ikiwa kijana kaweza kuchupa ngazi kuingia kidato cha tano kwa *pass* zake huyu ndio kafaulu, yule aliyekuwa hakupata uwezo wa kuchupa ngazi hakufaulu hata kama kapata kile cheti.

Sasa mimi nafikiri pia wakati wa kuripoti matokeo haya tungeripoti ukweli kwa sababu bila ya kuripoti ukweli tutakuwa tunadanganyana kila siku idadi fulani wamefaulu lakini hawawezi kuchupa ngazi. Matokeo ya kidato cha sita yakitoka yule mwenye uwezo angalau wa kujisukuma akenda chuo kikuu ndie aliyefaulu, yule wa kubembeleza akaanza tena hajafaulu. Tukitazama katika mtandao matokeo sote tunayajua tunayaona inasikitisha sana lazima tufanye kazi.

Mhe. Mwenyekiti, suala langu la mwisho, kwa mujibu wa sera hii ya elimu inaambiwa kwamba kutakuwa na fursa sawa na uwezo wa kuingia, *excess and equity to the education system for all*, kila kijana aliyefikia umri akaweza kuingia katika skuli na akapata uwiano wa usawa. Mimi nauliza kuna skuli nyengine wana vikalio wengine hawana, skuli nyengine zina maabara, wengine hawana, nyengine zina walimu wa kutosha, nyengine hawana, wengine wana walimu wa sayansi, wengine hawana. Je, sera hii imefuatwa. Wanafunzi wanayo haki ya kuishtaki sasa wizara kwa sababu wizara ndio waliotoa sera kwamba kutakuwa na uwiwano.

Lakini jengine ni kwamba katika sera hii imetajwa kwamba wizara itajenga maabara na kuwafundisha wasaidizi wa maabara. Juzi hapa Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali lake alikiri kwamba hakuna wasaidizi wa maabara wanaofundishwa, sio wanaofanya kazi hata wanaofundishwa hakuna. Hii ni haki kwa somo la sayansi halafu tuendelee kusema kwamba linafeliwa. Skuli hazina maabara, hazina vifaa, lakini hata wale wasaidizi wa maabara hawafundishwi, hawaajiriwi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema kwamba kama tunataka elimu ya kweli bado turudi katika *pipeline* tuwe *serious* tutazame wapi tulipojikwaa tuangalie na tuweze kufanya marekebisho. Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia asubuhi hii kuweza kukutana hapa tukiwa wazima.

Mhe. Mwenyekiti, pili nichukue fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii kuweza kuchangia mchango angalau mdogo katika bajeti hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Lakini tatu nimshukuru na nimpongeze sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri wake na watendaji wake wote kwa juhudi zao kubwa wanazozichukua. *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atawajaalia tuweze kufikia pale mahala ambapo tunapakusudia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu nataka nianze na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu. Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri kulizingatia hili kwa sababu ofisi hii kwa siku hizi kutokana na wingi wa maskuli imekuwa ukaguzi unachukua muda mrefu sana bila kufanyika na hili huwa linarejesha nyuma sana na linawazidishia mzigo mkubwa sana wale walimu wetu wakuu.

Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri ule ukaguzi wa wilaya ambao zamani ulikuwa ukifanywa basi pia uweze kufanywa halafu ule ukaguzi mkuu uweze kufuatia juu yake angalau pengine mwaka kwa mara moja. Kwa sababu bila ya kupita ukaguzi walimu wetu wakuu wanakuwa wana kazi kubwa sana ya ulezi wa walimu pamoja na watoto, lakini wanapopita wakaguzi mara kwa mara inasaidia na wao kuwaweka vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nilikuwa pia nimuombe Mhe. Waziri kuangalia walimu wetu wale tunaowaajiri, ule wakati wa kufanya uajiri kuweza kuona tunawaajiri walimu kutokana na zile sehemu wanazotoka. Hili niseme litatusaidia kwanza kupunguza gharama za walimu na masafa makubwa wanayokwenda, lakini pia litaweza kupunguza uchelewaji wa walimu ambao wanachelewa sana kufika katika maskuli. Mwalimu anatoka pengine mjini anakwenda kusomesha Mbuyutende inakuwa hii inachukua masafa marefu ukilinganisha na usafiri wetu ulivyo.

Kwa hivyo, hapa pia panasababisha matokeo mabaya ya mitihani kwa sababu walimu wanafika wakati sio hawana muda wa kufundisha na huku tayari wanataka muda wa kurudi majumbani kwao. Inakuwa hapa matokeo mabaya tunayapata, hasa mimi niseme katika Mkoa wa Kaskazini hili lipo sana na kweli mkoa wetu unakuwa uko nyuma kielimu kwa sababu walimu wetu wengi wanatoka masafa marefu.

Mhe. Mwenyekiti, ningeomba pia kutokana na upungufu wa walimu ambao tunao basi wale walimu wetu waliokwishasomea ngazi ya cheti wangefanyiwa maarifa ya kuajiriwa ili tukaweza kujaza yale mapungufu tuliyonayo katika maskuli yetu.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, tunakuwa tunalalamika sana kuhusu ukosefu wa walimu wa sayansi. Kwa hiyo, nimuombe Mhe. Waziri pamoja na mapungufu ya walimu lakini pia huwezi kuwasha moto bila ya kuwa na kuni, vifaa vya sayansi hamna kabisa maskuli. Hili Mhe. Waziri nalo aliangalie kwa mtazamo, pia linaondosha hata hamu ya wale wanafunzi kuwa wanarudi nyuma sana kwa kukosa vile vifaa.

Mhe. Mwenyekiti, tuna majengo ya maskuli tunayoyajenga na baadae tunaikabidhi wizara itumalizie. Hili pia Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri tuna majengo yetu mengi tumeshamkabidhi na yapo kwa muda mrefu aweze kuyaona na kuyashughulikia kuyamaliza, ili ule mrundikano wa wanafunzi wetu pale uweze kupungua.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, kuna wakufunzi wetu wa michezo na huwa mara nyingi tunakwenda tukiwasomesha Tanzania Bara. Hatuwezi na sisi kwa upande wetu tukajenga chuo chetu hapa ili wakufunzi wale wakafundishwa hapa na baadae wakaweza kuendelea na kuwapatia elimu wengine.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa leo mchango wangu ulikuwa ni huo na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Unguja naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia, ahsante.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuamsha salama katika nchi yetu tukiwa tunaendelea kujenga taifa letu na watu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, pili nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kutia baraka zangu katika wizara hii muhimu, wizara mama ambayo nina hakika sote tunatokea huko kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, inawezekana hata mimi nisiwe na mchango mkubwa lakini nataka nianze kidogo kwenye Mfuko wa Elimu ya Juu. Mhe. Mwenyekiti, nchi haiwezi kuendelea kama haina wataalam. Kwa hivyo, nadhani suala la kuwasomesha vijana hasa hasa katika elimu ya juu iwe ni kipaumbele cha mwanzo katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, katika Baraza lililopita wakati tunajadili mchakato wa mafuta tuliambiwa kwamba ndio kwanza serikali yetu inatafuta vijana kuwapeleka waende wakasome mambo ya uinjinia wa mafuta, sasa hii ni ishara kwamba hatuna wataalam katika nchi. Sasa ili tuwapate lazima mfuko huu wa elimu ya juu upewe umuhimu wa peke yake.

Mhe. Mwenyekiti, mara moja kamati yangu ilipokuwa inatembelea Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali nilisikitika sana na hata humu katika kitabu cha Mhe. Waziri kaeleza hivyo. Zile pesa zinazotengwa kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wanaosoma vyuo mbali mbali ulimwenguni kwa kweli hazikidhi haja hata nusu ya mahitaji na hili ni jambo la kusikitisha sana. Tukaambiwa zilitengwa bilioni 4 kama sikosei lakini kilichopatikana kwa mwaka mzima ni nusu ya safari hiyo ya mwaka yaani ni bilioni 2.

Sasa wizara inatoa mikopo inahudumia wanafunzi ikifika miezi 6 ina-*collapse*. Kwa hivyo, tatizo linatokea hapo wanafunzi wameshapoteza muda, pesa za kuwaendeleza hatuna, kurudi pia ni kupoteza pesa, matokeo yake ni kutazamana macho. Manung'uniko hayeshi kwa wanafunzi kila siku wanapiga simu jamani mbona hatupewi pesa, hatimae hata sisi mara nyengine hulazimika kuchomoa pesa mifukoni tukiwapelekea ili wajishikize, lakini haziwasaidii kwa sababu pesa utakayotoa wewe ni ndogo sana.

Mhe. Mwenyekiti, nawaomba Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo wajitahidi huu mfuko wasiukoseshe pesa, vyenginevyo nchi yetu tunahitaji maendeleo na kama nilivyosema maendeleo hatuyapati bila ya kuwa na wataalam. Tutakuja kujikuta hapa hatuna wataalam na tuko katika soko la Afrika Mashariki sasa hivi.

Wenzetu wa Kenya wana elimu zao, Watazania wana elimu zao wakija Zanzibar huku hatuna wataalam, tutakuwa tukinung'unika kila siku hatupati ajira lakini kumbe tatizo liko hapa. Mimi nadhani tukiwa na wataalam wetu tutaweza kufanya ushindani katika soko. Kwa hivyo, naomba sana mfuko wa elimu ya juu usinyimwe pesa, bora tupunguze pahala pengine lakini huu mfuko wa wanafunzi walio nje ya nchi ambao tumeshawaanzisha kwa pesa nyingi basi tuwaendeleze mpaka watimize kozi zao.

Lakini la pili Mhe. Mwenyekiti, maskuli yetu takriban Zanzibar nzima tuna tatizo la hatimiliki, yale maeneo ya skuli hayana hatimiliki na tumeshasema sana na inaonekana hili jambo ni tatizo sugu sana. Matokeo yake Mhe. Mwenyekiti, maeneo ya skuli yanavamiwa, wakaazi wa jirani wale kila mtu anasogea pale anasema hili lilikuwa shamba letu bwana, hatimae skuli inataka kujipanua haina nafasi tena. Sasa kama hakuna uwezekano wa kupata hizo hatimiliki, basi hata kwenda kupimiwa zile *beckon* zikaonekana wasiingie mle haiwezekani. Mhe. Mwenyekiti, naomba sana suala hili wizara ilizingatie sana.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo nataka niliguse kidogo ni kwamba Mhe. Waziri kwa kweli ana changamoto sana za mafao ya walimu. Kuna walimu wanatumwa kwenda kusahihisha mitihani, wanatumwa kwenda kusimamia mitihani, wanakopwa sana hawa na masikini ya Mungu ukimkopa vile akiwa na matumaini ya kupata pesa basi huwa yeye anatumia kabisa huku sasa ni bughudha kubwa hiyo.

Halafu isitoshe kuna walimu wanaojiendeleza, kama mtu anatoka cheti kwenda diploma, au anatoka diploma kwenda digrii, akirudi kwenye kazi kile kiwango chake kinaweza kikachukua mwaka mzima hawajarekebishiwa mishahara yao. Mhe. Mwenyekiti, huu nao ni usumbufu mkubwa naomba sana wizara

ilizingatie suala hili. Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi kuna walimu wa aina hii kwa mamia wanatunung'unikia sisi hawajarekebishiwa viwango vyao vya mishahara, wameshatimiza mwaka wapo kazini wanafanya kazi lakini mshahara ni ule aliotoka nao kabla ya kusoma. Sasa hili nalo ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine nilitaka niisifu wizara katika hili. Nasema tuwe na mwelekeo wa kubadilika kidogo, lazima tuwe na sera itakayojali zaidi kwa wakati huu tulionao sasa hivi, hii elimu ya sayansi na mafunzo ya amali. Kwa sababu nimeangalia majadweli kiasi matatu au manne hapa, nikapata takwimu ambazo tukiendelea nazo basi mwisho wa siku tutajikuta tuko pabaya.

Kwa mfano nimeangalia jedweli nambari 26(a) Chuo Kikuu cha SUZA, wanafunzi wanaofanya Shahada ya Sayansi ya Ualimu pale ni watu 141, lakini wanaofanya Shahada ya Sanaa ya Ualimu ni 633, hiyo tofauti ni kubwa sana na huku nyuma tayari tumeshakuwa na mrundikano wa sanaa nyingi sana kuliko sayansi na sasa hivi viwango ndio vinakwenda hivyo. Halafu nikaangalia Chukwani wanaofanya Shahada ya Sayansi ya Ualimu ni watu 148, lakini wanaofanya Shahada ya Sanaa ya Ualimu 638, pia tofauti ni ya kutisha kwa kweli.

Vile vile nikaangalia Chuo cha Kiislamu Mazizini walimu wanaosomea Stashahada ya Sayansi pale ni watu 7 tu, hao ni sekondari. Lakini wanaosomea Stashahada ya Sanaa sekondari ni watu 56, yaani kutoka watu 7 mpaka 56. kwa hivyo bado idadi inaendelea. Ukija kwenye Stashahada ya Ualimu ya msingi sasa, Sayansi ni watu 7. Lakini ya Sanaa ni watu 27. Sasa hii *trade* kwa kweli inaleta *indicator* mbaya tutafika pahala tutakuwa na walimu wa sanaa wengi na wasomi wa sanaa wengi yaani digrii za sanaa nyingi ambapo hazina soko tena katika wakati wa leo.

Kwa hivyo, nilikuwa naomba hii walioianzisha ya kusomesha elimu mbadala na mafunzo ya amali, basi iwe ni kipaumbele vile vile. Kwa sababu siku moja mtu ukishamsomesha ukampa utaalamu na hapa wamesema kwamba mtu kama amehitimu vizuri, wanaweza kumkopesha hata mfuko wa kuweza kupata *row material* na kuweza kujiajiri mwenyewe na kujitegemea. Kwa hivyo, hili ni jambo la faraja na nataka niseme kwamba wameanza, wanasema kila Mkoa angalau kuwe na skuli moja ya amali. Mimi nilikuwa nafikiri haitoshi, wajitahidi angalau ziwe zina uwiano sawa kati ya skuli hizi za kawaida na za amali yaani ziwe nyingi ili ule mzigo wa kuwa sasa mtu kamaliza aje kwenye serikali iwe tunaupunguzia mzigo serikali wa kuwaajiri watu, bali iwe wenyewe wanajiajiri. Nafikiri nilikusudia nitowe wazo hilo.

Halafu bado tuna changamoto sana ya maskuli, kama sehemu ya kusomeshea, lakini hata vikalio bado ni tatizo kubwa sana, najua ni mzigo mzito sana kwa serikali, lakini kwa kweli kuna haja ya kujitahidi zaidi, tuwaombe wahisani maana yake hatujiwezi lakini angalau tuombeombe.

Mhe. Mwenyekiti, unajua tunachangamoto nyingi na pesa hatuna. Mimi hufika pahali nikasema suluhisho la hili ni yale mafuta yetu, tukishakuwa na mafuta yetu yote haya yatakuja yenyewe. Kwa hivyo, hata kama leo sio wizara ya kuchangia mafuta, lakini bado inaonekana kutochimba mafuta bado ni tatizo katika nchi yetu. Kwa sababu haya mimi nina uhakika waziri hawezi kuya-*solve*, huwezi kupata vikalio vya wanafunzi wote wa Zanzibar nzima kama huna pesa. Hii bajeti yenyewe ukiiangalia karibu asilimia 80 ni misaada kutoka nje. Je, tukiwa na mafuta yetu. Mimi nafikiri tulione hilo.

Jambo jengine ambalo ni changamoto kwa wizara ya elimu. Tumeanzisha jambo lakini tumelianzisha kwa maneno, hapa tulipitisha kwamba mtoto akitaka kusoma darasa la kwanza hadi kwanza awe amepita katika darasa lile la maandalizi, tunaita chekechea sijui. Sasa yale madarasa tumeyasema kwa maneno tu, maana yake madarasa ya maandalizi nayo yanahitaji kuandaliwa. Kunatakiwa walimu wa maandalizi vifaa mbali mbali vya kumuwezesha mtoto angalau katika ule mwaka wake wa maandalizi aweze kuandaliwa vizuri kwa ajili ya darasa la kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi kila unapopita unaambiwa wananchi wenyewe wajitegemee kulitafuta hilo darasa la maandalizi. Sasa ni kikwazo tutafika pahala kama kweli itakuwa ni lazima mtoto apite maandalizi basi itafika pahala itakuwa wale watoto wetu hawapasi kwa sababu hawakupita katika madarasa ya maandalizi. Sasa sijui wizara isiyokuwa na pesa itafanya nini, lakini hili kwa sasa hivi halitekelezeki. Maana yake wameachiwa mzigo wananchi wenyewe, jambo ambalo hata sisi. Mimi huko jimboni kwangu nimepewa maombi ya kujenga mabanda ya maandalizi hayapungui 18. Sina uwezo wa kufanya hivyo, sasa sijui itakuwaje.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli bado tuna changamoto la utovu wa nidhamu wa wanafunzi, hili jambo linakidhiri kila leo. Sasa sijui kama ni ile sera ya kuwacha kupiga bakora, lakini wanafunzi hawana adabu hata mbili. Bahati mbaya sana hawakataziki. Ukimuona mwanafunzi sasa hivi anavyojadiliana na mwalimu wake huwezi kuamini. Maana yake inafika pahala hata mwalimu anaogopa kumwambia mwanafunzi neno. Anaweza akamtolea matusi hajawahikuambiwa hata siku moja. Mimi nafikiri tuangalie tena namna ya kuweza kuwadhibiti wanafunzi kinidhamu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilishawahi kulisusia darasa kwa sababu wanafunzi hawaniheshimu, kila nikienda darasani utovu wa adabu na uhuni, nikawaambia haya mtajidhuru wenyewe siji mimi. Sasa na walimu kama watakuwa na moyo kama huu. Wewe ni mwalimu bwana unakwenda darasani ni lazima wanafunzi wakuheshimu na wakusikilize. Leo unasomesha huku wanafunzi wanakuzomea nyuma. Unafika pahala huna moyo wa kuwasomesha. Kwa hivyo, hapa pia pataporomosha elimu.

Sasa nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri pamoja na kuwa kuna utandawazi, lakini mimi nilikuwa namuogopa mwalimu wangu kwa sababu alikuwa akinipiga mikwaju. Hii bakora Mhe. Waziri ndio ambayo inawanyoosha watoto, lakini adhabu mbadala hii, hata kama ulimwengu ndio unavyotaka haitusaidii. Labda vichwa vyetu vya kiafrika tofauti na vile vya wazungu kule, maana mzungu ukimwita pengine ukampiga maneno laini na ushauri nasaha basi anarekebishika lakini Mwafrika harekebishiki, akishaona sipigwi basi. Huu utandawazi umezidisha huu utovu wa nidhamu maskulini, kwa sababu kiwango kikubwa cha ukosefu wa nidhamu ya wanafunzi sasa hivi ni mambo haya ya *sex* na haya wanayapata kwenye utandawazi.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nafikiri kwa mazingira tuliyonayo, haidhuru ni jambo gumu lakini hebu sasa serikali ianze kuliangalia. Tuwe na skuli za wanaume na skuli za wanawake mbali. Mimi nafikiri wanafunzi ni wale wale ni kuwabagua madarasa tu, darasa hili litakuwa ni la wanawake watupu na hili litakuwa ni la wananume watupu, la ikiwa itakuwa ni kuwanyanyapaa basi twendeni, lakini tutafika pabaya.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema sitokuwa na mchango mkubwa sana ila ni kutia baraka zangu kwa sababu hii ni wizara mama. Baada ya kusema hayo, mimi nasema kwamba kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chonga nakubaliana na hotuba hii ya bajeti ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia kwa mia.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijakaa naomba niwasifu sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa takwimu. Hiki kitabu hotuba ya kusoma kwa maneno ni *one third* na *two third* ni takwimu sijapata kuona katika wizara yoyote. Kwa hivyo, nawapongeza sana kwa takwimu, ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia fursa hii ya kueleza machache kuhusiana na hoja ilioko mbele yetu. Awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kutufikisha siku ya leo kuwa hai, na hatimaye kutujaalia hazina ya afya na uwezo wa kutoka majumbani kwetu mpaka kufika hapa bila ya kukamatwa mkono. Hii ni hazina kubwa aliyotujaalia Mwenyezi Mungu na kwa vyovyote vile hatuna budi kumshukuru.

Mara baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nadhani nitakuwa mtata wa shukrani kama sikutumia fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri wake kwa kushirikiana na wataalamu wao, kutuletea kitabu hiki cha bajeti yao. Kwa kweli wamekitayarisha vizuri sana na matayarisho yote yametayarishwa kitaalamu na nimefurahi zaidi katika uwasilishaji. Yaani Mhe. Waziri pamoja na umri wake kidogo kuwa juu lakini alituwasilishia hapa kwa umakini wa hali ya juu. Nadhani hata kama kungekuwa kuna mlemavu wa masikio basi angesikia, kwa hilo nampongeza sana.

Mhe. Mwenyekiti, niende moja kwa moja katika hoja iliopo mbele yetu. Mbe. Mwenyekiti, kwa kweli katika mipango ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika mwaka huu wa 2011/2012 nadhani wangewaangalia sana walimu. Walimu Mhe. Mwenyekiti, wa Zanzibar wana matatizo makubwa sana. Walimu wana mtatizo ambayo yanahitaji hatua za dharura ili kuyatatua. Mimi mwenyewe binafsi nilikuwa mwalimu, matatizo ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali nayajua fika.

Mhe. Mwenyekiti, nikianza kwanza hivi tunavyozungumza ni kwamba Wizara ya Elimu wanakuwa na tatizo kubwa sana pale mwalimu anapokwenda kusomea na kuhitimu masomo yake kumfanyia marekebisho ya mshahara basi wanakuwa wanachelewa sana, sijui ni tatizo gani ambalo linapelekea ucheleweshaji huo.

Mhe. Mwenyekiti, juzi tu katika miaka ya karibuni tu hivi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia vile vituo vyao vya TC. Walimu walichukua mafunzo wengine walichukua mafunzo ya vyeti, wengine katika fani ya Stashahada na wamemaliza katika kipindi kirefu. Kozi walizokuwa wakitoa TC wanasema nyengine zinalingana na Stashahada. Kwa hivyo, wengine walijiendeleza kutoka cheti kwenda kwenye Diploma, lakini hadi leo hii karibu mwaka wa tatu sasa walimu wale wanalipwa mishahara yao ya kawaida bila ya kufanyiwa marekebisho.

Nadhani Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ingejitahidi katika hili, kwa sababu wanasheria wengi hapa wanatuambia, kwamba ile ni haki yao na imechelewa sana na wanasheria wanatuambia kwamba haki ikichelewa kutolewa basi ni sawa na kwamba haikutolewa kabisa. Kwa hivyo, nadhani wasiwanyime hawa walimu haki zao wawapatie kwa kuwarekebishia mishahara.

Tatizo jengine kwa walimu Mhe. Mwenyekiti, ni likizo. Likizo kwa walimu nakusudia hutuma ile ya kupata likizo ni mtihani. Kuna walimu wameshasomesha miaka 15 na wengine 20. lakini yale mafao ya kwamba

wanapewa mafao ya kwenda likizo ni mtihani mkubwa. Walimu wengi wananung'unika kwa hili na katika watu watuliokuwa maskini katika nchi hii ni sisi walimu. Kwa hivyo, namuomba sana Mhe. Waziri awaangalie walimu katika hili kwa jicho la huruma sana.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, walimu tuko pale tunawasomesha wanafunzi wetu. Sisi pengine tuna cheti, mwanafunzi wetu anakuja pale kusomeshwa ana digrii ya kwanza, akifika anatuzidi kwa mishahara. Kwa hivyo, ningeiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali iangalie *scheme of work*, yaani mwalimu aangaliwe na uzoefu wake wa kufanya kazi. Walimu tumegaragara pale mwanafunzi wetu tumemsomesha juzi, leo anakuja kutupita kwa mshahara sana. Kwa hivyo, tunaomba ule uzoefu wetu katika kazi nao utiliwe maanani ili tuweze kupata mafao ya *scheme of work*.

Mhe. Mwenyekiti, walimu hasa wanaosomesha katika Skuli za Sekondari, inafika pahala siku nyengine tunaona haya kwenda kule. Unakwenda Skuli ya Sekondari mwanafunzi ana buti, wewe una kandambili, mwanafunzi kavaa suti, wewe una yebo yebo na mtumba. Kwa hivyo, ile *approach* ya mule darasani inakuwa ngumu.

Mhe. Mwenyekiti, tunaomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali iwaangalie sana walimu katika kuwapatia angalau posho la mavazi, kwa kweli ni tatizo, japo walimu wa sekondari tupatiwe posho hilo. Umaskini umetufanya tuvae yebo yebo na umaskini umetufanya tuvae mitumba. Kwa hivyo, tunaomba tuangaliwe walimu tupatiwe japo posho ndogo ya kuweza kununua mavazi angalau baada ya miezi sita tupatiwe posho la kununulia mavazi na tuweze kuwasomesha wanafunzi wa sekondari. Huyo mwanafunzi ukimuona basi utamuona yeye ndio mwalimu na wewe mwalimu utaonekana ndio mwanafunzi. Tunaomba sana katika hili.

Mhe. Mwenyekiti, juzi hapa tulikuwa tukinung'unika sana kwamba utalii umetupotezea maadili. Lakini kuna taarifa za kusikitisha sana Wilaya ya Mkoani kwamba Maafisa wa Elimu wa kule wanawalazimisha walimu wavuwe mashungi wakati wa kusomesha. Hili ni tatizo sana.

Mhe. Mwenyekiti, hili suala la mashungi ni mila na silka ya Kizanzibari, hivi karibuni Sweeden na kama nitakuwa sahihi, wanafunzi walikataa wasivae hijabu na yenyewe serikali ya Sweeden imekubali sasa wanafunzi wavae hijabu, itakuwa Zanzibar jamani ambayo mavazi haya ni ya asilia. Kwa hivyo, kuna taarifa hiyo Mhe. Waziri naomba ulifuatilie. Kama kuna maafisa wako ambao wanawakataza walimu wasivae mashungi hilo ni tatizo kubwa sana, ni tatizo kwa sababu mwalimu ndio kioo. Ikiwa unataka mwalimu ende skuli

kichwa wazi basi na mwanafunzi ataiga na yeye mwanafunzi ataanza kuonesha kichwa na atakwenda zaidi mpaka atafika kuonesha maziwa. Samahani sana Mhe. Mwenyekiti, kwa lugha hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niende katika Chuo chetu Kikuu hichi cha Taifa, Chuo Kikuu cha Zanzibar SUZA. Mhe. Mwenyekiti, SUZA ndio chuo chetu cha taifa na ndio chuo chetu sa serikali. Kwa mnasaba huu ni kwamba Wizara ya Elimu inatakiwa iwe makini sana na serikali ipewe umuhimu katika kukiendesha kile chuo.

Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha kwamba maelezo ya Chuo Kikuu cha Taifa katika *campus* ya Nkuruma na ile waliyopewa ya Tunguu tayari yameanza kuvamiwa. Wafanyabiashara wameanza kuvamia katika *campus* zile za chuo na wameshaanza kujenga majengo pale. Sasa hapa sitaki niende sana kwa sababu nasikia kuna kesi mahakamani na jambo likishakuwa mahakamani halitakiwi lisemwe. Lakini kule Tunguu nasikia kuna maeneo ambayo yanaanza kuuzwa hasa ya chuo.

Sasa mimi natoa tanbih kwa serikali na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwamba tukihoji. Juzi tulihoji pale kuhusu hati miliki, nikaambiwa Wizara ya Elimu haihusiki, sijui ni ya mambo ya ardhi. Serikali ni serikali bwana ikiwa ni ya ardhi au ni ya Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais, basi itowe hatimiliki kwa taasisi zetu za serikali kikiwemo chuo cha SUZA. Ni lazima ipatikane hatimiliki.

Mhe. Mwenyekiti, la kusikitisha zaidi ni kwamba hizi taasisi zetu za serikali zikiwa na kesi na hawa wengine basi mara nyingi taasisi zinashindwa sijui kwa nini. Kwa hivyo, tunaomba mzimilikishe hizi taasisi, mzipe hatimiliki ili waweze kuhami hizi ardhi zao.

Mhe. Mwenyekiti, Chuo cha SUZA sasa hivi kinatoa mafunzo ya sayansi, kwa kweli mwanafunzi wa Chuo Kikuu anatakiwa a-*work in practical* ili aweze ku-*develop thinking ability, inquiry minds.* Halikadhalika ile *intellectual honestly* aweze kui-*develop*. La kusikitisha na jinsi serikali ilivyoundiwa bajeti ndogo kwa hiki Chuo chetu cha Taifa.

Inasikitisha sana Mhe. Mwenyekiti, kwamba mwaka jana wanafunzi wa *physics* hawakupata kufanya mitihani ya vitendo pale ni aibu. Ni aibu chuo cha taifa mwanafunzi kushindwa kufanya mtihani wa vitendo ni tatizo kubwa sana. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri hiki chuo chetu cha taifa bajeti yake iinuliwe ili waweze kuingia katika ushindani wa taaluma, ni aibu chuo chetu kuonekana kiko chini ukilinganisha na vyuo vya *private*. Sisi kama wasimamizi

wakuu wa matumizi ya fedha za walipa kodi, tutaonekana na sisi kama Baraza hatuna maana hatuielekezi serikali wakati tunapiga kelele. Tunaomba Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Fedha ikiangalie sana chuo chetu kikuu cha SUZA.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye dahalia kuna matatizo katika *campus* ya Nkurumah, haikidhi hata kukaa wanafunzi wa sekondari, wachilia mbali wa Chuo Kikuu. Naomba sana Mhe. Waziri uliangalie hilo. Kama kuna pahala pa kumega kidogo ukaweka pale basi angalia, kwa sababu likianza zogo pale katika chuo kile kimoja basi itaendelea katika vyuo vyengine, ni mafuta ya kuwasha haya. Kwa hivyo, tunaomba sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikipongeze hiki Chuo chetu Kikuu cha SUZA kwa kuweza kutaka kufungua tawi lao Pemba. Nakipongeza sana. Pia naupongeza Uongozi wa Chuo, akiwemo Dk. Kanduru pale pamoja na uongozi mzima wa chuo kwa kuweza kufikiria kitu kama hicho.

Mhe. Mwenyekiti, jambo la kusikitisha ni kwamba hawa chuo wanataka kufungua *department of agriculture*, wameomba ardhi Chamanangwe, ardhi iko wazi. Lakini inasikitisha kwamba wizara ya ardhi mpaka sasa hivi haijawapa jibu.

Aidha, wametaka nyumba kufungua afisi hapa Machomanne. Wameambiwa anakaa mfanyakazi wa wapi sijui. Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Waziri uwasaidie SUZA ili waweze kupata afisi kule Pemba na hatimaye waweze kufungua *department of agriculture* kule Pemba kama tawi lao.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba wenzetu wa SUZA wana nia nzuri. Kwa hivyo, Mhe. Waziri tunakuomba uwasaidie sana.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu usajili wa mashule haya

Mhe. Mwenyekiti: Unadakika mbili Mhe. Mjumbe.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye bodi ya mikopo basi. Mhe. Mwenyekiti, katika bodi hii ya mikopo kuna mfuko huu ambao unawasaidia sana vijana wetu kuweza kupata angalau elimu. Jambo la kusikitisha Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo ambayo yanaleta manung'uniko pale.

Kwanza wanafunzi wanaosoma Tunguu, hawapati lile posho la kujikimu na makaazi ni tatizo na inawapa usumbufu hasa wale wanaotoka katika kisiwa chengine, hawana pahala pa kukaa, wanalazimika kwenda kukodi nyumba za

kienyeji uswahilini, zogo moja kwa moja Yaillahi Yarabi Toba, kwa hivyo taaluma inakuwa tabu kupatikana. Kwa hivyo, tunaomba hili posho la makaazi na wao wapewe hawa.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, kuna kozi ambazo zinapatikana hapa nchini. Mhe. Mwenyekiti, kumsomesha mwanafunzi nje, kuna mikopo inatolewa kwa wanafunzi kwenda kusoma nje ambapo wanatumia pesa nyingi sana na huku bajeti ni ndogo lakini wanakopeshwa kwenda kusoma nje, wakati kozi zipo.

Mhe. Mwenyekiti, nimepata taarifa lakini sijahakikisha, kuna mwanafunzi mmoja kaenda kusoma *law of the financial administration* Uingereza, wakati *course* hii inapatikana pale Morogoro. Sasa wakati angekwenda Morogoro mwanafunzi yule angetumia si zaidi ya milioni 5 na kule Uingereza anatumia karibu milioni 40, kwa hivyo anazuwia wenzake kusoma. Kwa hivyo, kipaumbele kitolewe katika utoaji wa mikopo, *course* zinazopatikana hapa nchini basi wanafunzi wapelekwe hapa nchini, kwa sababu wakipelekwa nje ya nchi wanatumia fedha nyingi na wenzangu inakuwa ni tabu kupata mikopo.

Mhe. Mwenyekiti, mwisho nimalizie kwa haya mafunzo ya amali. Chuo cha Mafunzo ya Amali kilichopo Vitongoji, kimejengwa katika ardhi ambayo kulikuwa na mazao ya wakulima mengi tu na mazao yale yamefanyiwa tathmini karibu miaka mitano iliyopita. Wakulima wale hadi leo hii hawajapewa fidia zao. Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Balozi Seif Ali Iddi baada ya kunung'unika sana alimtuma waziri Mhe. Mohammed Aboud kuja kwenye ardhi ile na akaonana na wakulima. Lakini wale wakulima ambao mazao yao yamekatwa pale hadi leo hii bado hawajalilipwa fidia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa naomba wale walipwe fidia zao. Lakini pale watakapoona tumekwenda katika ofisi ya elimu pala panapouzwa maji, wananchi wa Vitongoji wasiopungua 300 na visahani vyetu pamoja na watoto wetu kwenda kudai vyakula pale, tusije tukaeleweka vibaya. Tutakaa miezi minne au mitano pale pale kudai haki zetu, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tukiwa tunaendelea naomba kuwajulisheni kuwa naomba tutambuwe uwepo wa Dk. Said Gharib Bilal, Mbunge wa Bunge la Afrika ya Mashariki, ambaye amekuja kuja kushirikiana na sisi, yuko pale juu. *(Makofi).*

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii iliyokuwa ni ya Mhe. Subeit. Kwa sababu ya muda na kwa sababu ya siku ya leo Ijumaa, nitakuwa na mchango mfupi sana, kuliko siku nyengine zote.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nianze kwa kutuoa pongezi zangu za dhati kwa Mhe. Waziri na Naibu Waziri kutokana na kuteuliwa kwao kushika nafasi hizi, kati ya moja ya wizara ambazo ni muhimu sana katika maendeleo ya uchumi na jamii yetu kwa hapa Zanzibar. Naamini kwamba Mhe. Rais kafanya hivyo baada ya kuelewa uwezo na uzoefu alionao Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, tunajadili bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, kwa fikra zangu shughuli za elimu zinapaswa zigaiwe katika sehemu mbili kubwa. Kwanza ni shughuli ya utawala, ikijumuisha makao makuu, ofisi kuu pamoja na mambo mengine yanayohusiana na utawala.

Eneo la pili ni muhimu tugawe shughuli za elimu katika eneo maalum la maskuli au mashule kwa lugha nyengine. Tutakapoweza kugawa shughuli za elimu katika maeneo haya muhimu, nadhani ndipo ambapo tutaweza kufika pahala tukaona hasa maendeleo ya elimu yanakuwa katika hali gani.

Kwa mwaka huu sekta hii ya elimu imetengewa bilioni 57 kwa shughuli za kazi za kawaida na bilioni 45 kwa shughuli za kazi za kawaida na shilingi bilioni 57 kwa shughuli za kimaendeleo.

Lakini mimi nataka nijiulize kwamba kati ya hizi shilingi bilioni hizi 45 ambazo zitatumika kwa shughuli za maendeleo na katika mughutadhwa ule niliosema mwanzo, kuwa tunapaswa tuzigawe shughuli za elimu katika maeneo mawili makubwa, yaani shughuli ya utawala pamoja na maskuli. Mhe. Mwenyekiti, skuli ndiko ambapo kwenye walimu, pia wako wanafunzi ambao ndio lengo la wizara hii pamoja na masuala ya ufundishaji yako skuli. Kwa kweli lengo hasa la Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Mhe. Mwenyekiti, ni kitendo cha wanafunzi kufundishwa, yaani hilo ndilo lengo kuu la wizara hii.

Sasa naomba nijiulize katika hizi shilingi bilioni 45 tukiachia mbali ile kasma ya mishahara ya walimu. Naomba nimuulize Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, ni kiasi gani kati ya fedha hizi zitakwenda moja kwa moja katika uendeshaji wa maskuli?

Katika utafiti wangu wa haraka nimeona hakuna kitakachokwenda katika uendeshaji au kitendo cha kufundisha mwanafunzi. Kutokana na hali hii Mhe. Mwenyekiti, ndipo ilipopelekea Baraza lako kuwa na maswali kutoka kwa Waheshimiwa Wawakilishi kwa niaba ya wananchi pamoja na wazazi, kwamba hivi sasa lazima tufike pahala tuiangalie tena upya Sera ya Walimu na suala zima la Elimu Bure na suala ambalo limejitokeza hivi karibuni kuhusu michango au malipo ya elimu.

Mhe. Mwenyekiti, katika kitendo cha kufundisha mwanafunzi ni kitendo mbali ya kumuhitaji mwalimu mwenye uwezo, kwa sababu kwanza lazima tuwe na mwalimu mwenye uwezo, pia tuwe na mwalimu mwenye hadhi ya kuwa mwalimu.

Kwa kweli bahati mbaya sana leo kama alivyosema Mhe. Saleh Nassor Juma walimu wetu kusema kweli hali zao pamoja na hadhi zao haziridhishi hata kidogo na hupelekea wakati mwengine wanafunzi huwa na hadhi kubwa zaidi ukimtizama, yaani huwa na *confidence* zaidi wanafunzi kuliko hata walimu.

Sasa ndipo pale inapojengeka ile tabia aliyoizungumza Mhe. Abdalla Juma Abdalla wanafunzi kukosa nidhamu au adabu, hii inatokana na hali halisi ya hadhi ya walimu wetu. Kwa mfano, walimu wetu tangu ukiwaangalia *appearance* zao, mapato yao kwa kweli hayalingani na hadhi ya walimu, kwa sababu miaka ya nyuma mwalimu alikuwa na hadhi, lakini miaka hii na sijui ni tatizo gani labda ni mapato au usimamizi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nadhani wakati umefika pamoja na wizara kama ilivyopendekezwa hapa nakubaliana kwamba kuwe na posho maalum angalau kwa mwaka mara moja walimu kuweza kupewa posho la mawazi. Kwa kweli haipendezi kumuona mwalimu anakwenda skuli na viatu vya yebo yebo au mwalimu anakwenda skuli hakuchomelea shati yake, kwa sababu walimu wa zamani walikuwa na *principles*, yaani mwalimu lazima achomelee shati, hivi leo mwalimu anakwenda skuli na sharti kama anakwenda kuchunga ng'ombe, sasa hatuwezi kuwalaumu, kwa sababu kipato chao ni kidogo. *(Makofi)*

Katika hili kama zilivyotaasisi nyengine za kiserikali, basi nashauri serikali iandae utaratibu maalum wa kuwapatia walimu posho la mavazi. Mhe. Mwenyekiti, serikali itakapofika hatua hiyo anaonekana mwalimu anakwenda skuli ovyo ovyo, basi ndipo pale mwalimu anaweza kuadhibiwa kwamba na yeye mwenyewe hana *discipline*, lakini vyengine vyovyote tutaendelea kuwalaumu walimu wakati hali zao si nzuri.

Kwa mfano, mwalimu wakati anaporudi kufundisha basi mwalimu huyo pengine ni mvuvi, yaani aende kuvua, mwalimu huyo ni mpigaji pande, yaani kulima kwa pamoja, maana yake ili kuweza kuyakidhi maisha yake. Sasa ikiwa mwalimu anazo kazi mia unategemea mwalimu atakaa wakati gani kufanya *reference* kwa ajili ya kuwafundisha wanafunzi. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja hapa kufanya majumuisho atueleze ni namna gani kati hizi shilingi bilioni 45 ukitoa fedha za mishahara, ni kiasi gani hwenda moja kwa moja katika *operations* za kuendesha skuli zetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu katika skuli zetu ni kitendo cha kufundisha kinahitaji angalau chaki, vikalio, mabuku, vitabu vya kiaya na vya ziada. Kwa hivyo, ni kiasi hii bajeti shilingi bilioni 45 imekwenda kutekeleza suala hilo?

Kutokana na matatizo hilo Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mara nyingi kama nilivyotangulia kusema kwamba kuna kuwa na tatizo kubwa sana la michango isiyoeleweka. Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni niliuliza swali la kwamba serikali itupe hasa ni michango gani ambayo imeruhusiwa na wizara ambayo inatambulika na serikali, pia michango gani ambayo haitambuliki na serikali, kwa sababu hivi sasa kuna mfumko mkubwa sana wa michango isiyofahamika kwa wazazi, kitu ambacho kinapelekea mizigo mzito sana kwa wazazi kuweza kumudu mambo haya. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa taarifa tulizonazo walimu hawana utaratibu wa kuandika kwenye mbao, isipokuwa walimu huwalazimisha wanafunzi wanunue karatasi za kuandikia, kuchangia fedha za kutolesha *photocopy*, kwa sababu hawana muda.

Kwa mfano, tulivyokuwa tunasoma sisi na nyinyi wazee, basi mwalimu hupoteza muda mwingi sana katika kuandika kwenye mbao, lakini sijui ni kwa sababu hakuna chaki. Kwa kweli hivi sasa kuna tatizo la walimu kuwalazimisha wanafunzi wachangie mpaka fedha za kutolesha *photocopy*, fedha za kununua karatasi kila siku na hili ni tatizo. *(Makofi)*

Namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, wakati atakapokuja aje atupe ufafanuzi kuhusu suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala la michango kwa sababu ni tatizo kubwa ambalo linalolielemea jamii yetu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, atakapokuja aje atueleze ni michango gani ambayo ni halali inayoruhusika. Kwa kweli tatizo ni kwamba hivi sasa mwanafunzi asipokwenda na michango hiyo, basi hulazimishwa arudi nyumbani na hili ni tatizo ambalo lipo. Kwa maana hiyo, Mhe. Waziri alitolee tamko hili. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba kunakuwa na michango mingi na skuli hupata fedha nyingi sana, lakini fedha hizi hazina uangalizi. Kwa hivyo, tatizo tunaloliona sisi kwa mujibu wa Sheria hii Nam. 12 ya Fedha, yaani fedha yoyote inayochangwa Mhe. Mwenyekiti hiyo ni fedha ya serikali, kwa sababu ni fedha ya serikali basi ina utaratibu wake.

Kwa mfano, fedha lazima ichukuliwe ipelekwe benki na baada ya kupelekwa benki hapo ndipo wizara au taasisi inaweza kuomba *retention* kwa ajili ya

matumizi. Lakini hali ilivyo hivi sasa ni tafauti, kwa sababu watu hukusanya fedha hakuna risiti inayotolewa na wala haijuikani ni kiasi gani cha fedha kimechangwa pale, alimuradi watu hujitafunia tu katika skuli, yaani fedha zinazochangwa hazilingani na mambo yanayofanywa kwenye skuli.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo kama hili lilijitokeza katika Wizara ya Afya kwenye ukusanyaji wa mapato katika Hospitali ya Mnazimmoja, tunashukuru serikali imechukua hatua, kwamba fedha zote zile zinazopatikana hivi sasa kwa ajili ya kuchangia zile baskeli na gari sasa zitaingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali na baadaye taratibu nyengine zitafuata. Kwa hivyo, hilo nalo tunaliomba lifanywe na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ili serikali, Baraza la Wawakilishi liweze kujua pamoja na wazazi waweze kujua ni kiasi gani kimechangwa na kupatikana na kiasi gani kimetukima kwenye shughuli za maendeleo katika skuli husika. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, katika hili kuna posho kama walivyozungumza wenzangu, ni kweli kwamba walimu wetu wanapata matatizo hasa wanapoteuliwa kwenda kusimamia mitihani.

Kwa kweli kuna tatizo pamoja na kilio kikubwa sana walimu hulipwa shilingi 1,000/= sijui hili lina ukweli gani, tena hiyo shilingi 1,000/= kwa siku maana yake ni kusema huwa kuna mkopo mkubwa unaotolewa. Kwa mfano, inawezekana kazi iliyofanywa mwaka jana mpaka leo bado hawajalipwa mafao yao tena fedha zenye ni shilingi 1,000/= kwa wiki mwalimu anakuwa na shilingi 7,000/=.

Mhe. Mwenyekiti, tulinganishe shilingi 7,000/= kazi ya wiki Mhe. Mwenyekiti, ni wapi na wapi. Kwa maana hiyo, hii inatoa tafauti kubwa sana baina ya viwango wanavyoteuliwa kusimamia mitihani ya Bara na hapa Zanzibar, yaani Zanzibar inaonekana kuna tatizo kubwa sana. Kwa hiyo, tunamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, atupe maelezo juu ya hili.

Mhe. Mwenyekiti, suala la pili ni kuhusu Chuo Kikuu cha Taifa *SUZA*. Kwa kweli niipongeze sana serikali kufikia hatua ya kuanzisha Chuo Kikuu, kwa hakika kitendo kile ndicho kinachoonesha kwamba sasa Zanzibar ni nchi na yale mambo yanayoifanya na kuionesha Zanzibar kama nchi basi moja wapo ni hili kuwa na Chuo Kikuu chetu. Kwa hivyo, kama tungekuwa hatuna Chuo Kikuu basi tungelikuwa bado tunaendelea kupata tatizo kubwa sana la wanafunzi wetu katika kupata elimu ya juu, hivyo naishukuru sana serikali. Lakini tuseme kwamba ni kitendo ambacho kilichukuliwa wakati maandalizi ni madogo, kwa sababu ya ile hamu. Kwa hiyo, kitendo tayari kimeshatokea na tuone sasa tunaendelea kukiboresha zaidi Chuo Kikuu chetu.

Chuo Kikuu hiki kiliomba bajeti yao ya shilingi bilioni 26, yaani mahitaji yao yalikuwa ni shilingi bilioni 26 na *ceiling* waliyopewa ni shilingi bilioni 3.6 hii kiwa ni sawa na asilimia 3 ya mahitaji. Mhe. Mwenyekiti, hebu tujiulize ikiwa waliomba shilingi bilioni 26 na wakapewa shilingi bilioni 3.6, yaani asilimia 3 tunapata tafsiri gani?

Tafsiri tunayoweza kuipata ni kwamba *SUZA* mahesabu au bajeti yao haikuwa sahihi, maana yake huwezi kufanya bajeti ya shilingi bilioni 26 ukapewa bilioni 3, basi inawezekana bajeti yao walipoifanya hawakuzingatia mambo, yaani haikuwa sahihi.

Lakini ikiwa bajeti yao ni sahihi na serikali ikaamua kuwapa shilingi bilioni 3.6 maana yake nini, maana yake ni kusema kuwa kilichoongezeka pale na inavyosemekana ni shilingi milioni 200/= tu ukilinganisha na bajeti ya mwaka jana. Sasa ukichukua *inflation* utaona kwamba hakuna kitu kilichoongezeka kutokana na tatizo la *inflation*.

Mhe. Mwenyekiti, ninasema kwamba tafsiri yake kupewa bilioni 3.6 pengine linafidia kwenye mambo ya mishahara tu, yaani ni kukifanya Chuo Kikuu katika bajeti hii kisiweze kufanya kazi zake. Tafsiri nyengine ni kukifanya Chuo Kikuu kisiweze kuendelea, maana yake tatizo la Vyuo Vikuu na hasa Chuo Kikuu chetu, kwa sababu bado ni kichanga kilikuwa kinategemewa mwaka hadi mwaka bajeti yake ikue, ili chuo kijikuze kitaaluma pamoja na kada zake. *(Makofi)*

Sasa tunachokipata ni kwamba hakutokuwa na maendeleo yoyote katika taasisi yetu ile muhimu ya serikali. Vile vile nina hofu katika hali na mwenendo kama huu Mhe. Mwenyekiti kwamba hata wanafunzi wanaotoka pale kuchukua *degree* zao, basi isijekuwa hali ni kama hii ilioko chini katika skuli za sekondari pamoja na za msingi, kwamba *quality* ya education ikawa ni mbovu na hii ndio hofu yangu.

Kwa hivyo, naishauri serikali kwa sababu inavyoonekana serikali baina ya *SUZA* na Taasisi nyengine kama Chukwani na sehemu nyengine inaonekana hakuna tofauti baina ya chuo hiki na vyuo vyengine, yaani na hizi taasisi nyengine za elimu. Kwa kweli bajeti zao takriban zinalingana sana. Kwa mana hiyo, naomba kuishauri serikali kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba lazima ifike pahala tukipe umuhimu maalum chuo hiki na tukipe mamlaka na tusiifanye ikawa kama ni Idara ya Serikali, tufike pahala tuipe *autonomy* kubwa sana pamoja na bajeti yake maalum. Katika hali hiyo ndipo ambapo chuo chetu kitaweza kulingana na Vyuo Vikuu katika Afrika Mashariki na nchi nyengine za dunia.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka na suala hilo bado katika suala hilo kuna suala la tatizo la walimu, tatizo la walimu wanafundisha *SUZA*. Taarifa tulizonazo ni kwamba walimu wanaendelea kutukimbia katika chuo hiki. Kwa mfano, katika kipindi cha miaka miwili, mitatu waliofundishwa kwa ajili kwenda kufundisha Chuo Kikuu si chini ya walimu wanne tayari wameshatukimbia wengine wawili wana *PhD* tayari wameshakimbia.

Sasa naiomba serikali kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, katika mazingatio yake ya kuboresha mishahara na maslahi, basi wajaribu kuwe priority maalum katika Chuo Kikuu, ili kuzuia wimbi hili la wataalamu wetu wanaoendelea.

Kwa hivyo, sijui ni kiasi gani asilimia 50 hii itakuwa vipi, lakini takriban itakuwa hailingani na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo alituambia hwenda wakapishana na asilimia tano baina ya wataalamu walioko Bara na hapa na wala sina hakika kama nyongeza hii itakuwa ni kweli kutokana na nyongeza iliyoongezwa kule Bara.

Nikiendelea na mchango wangu sasa nigusie Skuli yangu ya Chanjaani, asubuhi hii nilikuwa na mazungumzo na Afisa Mdhamini, naye alinihakikishia Skuli ya Chanjaani iliyojengwa kwa nguvu za wananchi wa Chake-Chake itatekelezwa katika mwaka huu wa bajeti.

Kutokana na hali hiyo, naipongeza serikali na ninaomba hilo lifanikiwe, kwa sababu kama hilo halikufanikiwa, basi itakuja kuwa skuli hii iliingizwa katika bajeti miaka mitatu iliyopita nyuma na Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika ambaye alikuwa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Awamu ya Sita, mara kwa mara alikuwa akiizungumzia Skuli ya Chanjaani katika bajeti na mara hii haikuingizwa kwenye bajeti, katika hoja aliyonieleza Afisa Mdhamini kwamba tayari imeshatengewa kila kitu mpaka walimu. Kwa hivyo, naponge hilo na matarajio yangu hilo litafanikiwa katika mwaka huu wa bajeti. *(Makofi)*

Mwisho naomba nimalizie, Mhe. Mwenyekiti tunapongeza sana Skuli za Binafsi zilizozinduliwa na hasa kwa ajili ya kutekeleza Sera ya Serikali ya Kuwepo kwa Skuli za Maandalizi. Kwa kweli Skuli Binafsi zimekuwa zikisaidia sana katika hili, hivyo napongeza juhudi hiyo na ninaiomba sana serikali kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, iendelee kusimamia na kuiunga mkono Sekta Binafsi kwa sababu itasaidia mzigo mkubwa sana katika serikali.

Lakini katika hilo naomba nitoe kilio changu kwamba kumekuwa na utaratibu ambao usioeleweka katika kuwasafirisha wanafunzi hao wadogo kutoka skuli kwenda nyumbani.

Mhe. Mwenyekiti, wamekuwa wakipakiwa kwenye magari katika hali mbaya sana, yaani hupakiwa watoto wadogo mpaka inakuwa ni hatari, ni vyema tumuombe Mwenyezi Mungu siku zote kwa kweli magari haya ayavushe salama katika barabarani na Mwenyezi Mungu aliepushe hili. Sasa pindipo ikaja ikatokea ajali basi taifa litakumbwa na kilio kikubwa sana, yaani watoto hupakiwa kwenye magari kama nguru hulaliana.

Kwa hivyo, tunaiomba serikali, wizara pamoja na taasisi zote zinazohusika kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, katika kuliendeleza hili suala zuri la Skuli hizi za Maandalizi, basi serikali ilisimamie suala hili ili wanafunzi wetu hawa wapakiwe katika kiwango kinachokubalika kwa ajili ya kuepusha taifa kuja kupata hasara katika suala hili muhimu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo narudia tena kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na Mhe. Naibu Waziri nawaombea kila la heri naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi siku ya Ijumaa ya leo na wakati huu wa asubuhi hii kunipa fursa ya kuzungumza machache kuhusiana na wizara inayotupa nuru, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwa kweli mengi yameshazungumzwa, isipokuwa na sisi tutatia kalafati.

Kwanza naomba niwapongeze kwa sababu wameona maeneo ni mengi sana ambayo yanahitajika kuyafanyiakazi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze pale ambapo Mhe. Omar Ali Shehe naye amepagusia. Kwa kweli hivi sasa kuna Agizo au Utaratibu wa Wizara ya Elimu, unaowataka wanafunzi wanaoingia skuli kwa mwaka wa kwanza kulipia sijui ni ada au mchango.

Hivi sasa sisi moja katika vipao mbele vyetu ni kuhakikisha kwamba wanafunzi wetu wengi au vijana wetu waliofikia umri wa kwenda kusoma basi wanapata kuandikishwa na wanaendelea na kusoma. Lakini huu mpangilio wa kuwafanya wananchi ambao wanaopeleka wanafunzi wao skuli kwa mara ya mwanzo kutoa *fee* au mchango fulani inarudisha nyuma na inawafanya vijana wengi wasiandikishwe, kwa sababu wazee wanakuwa hawana uwezo.

Sasa hii kwa vile si sheria ambayo inatakiwa itekelezwe na serikali ni mpangilio tu na utaratibu, basi ninaiomba Wizara moja kwa moja kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwa wale wambao wanaoingia kwa mara ya mwanzo kuandishwa skuli basi ikaondoshwa ada hii na tukabakisha na wale walioingia skuli na wanaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa tumekuwa na *tuition* nyingi, yaani vituo vingi vya *tuitions*. Sasa sijui kama vituo vile vinaratibiwa rasmi na wizara na je walimu wanaosomesha kwenye *tuition* zile au wanaosaidia wanakuwa na wao wanajulikana wana kiwango gani cha elimu au ni watu ambao wamejikusanya wakijua kwamba mimi nikisema nitafundisha Lugha ya Kiingereza, basi nitapata wananchi watakuja hapa na nitajipatia ajira.

Katika hili Mhe. Mwenyekiti, pia ninaomba kuwauliza wizara kwamba hizi tuitions kipindi hiki zimekuwa ni nyingi sana. Je, huko skuli tayari kumeshafanywa *analyze* na *evaluation* ambayo itatuwezesha sisi kujua je, hizi tuition ni sababu ya kwamba walimu wana kiwango kidogo cha ufahamu au ni wanafunzi ndio walio na ufahamu mdogo ama pengine masomo yao yamekuwa ni mengi kule darasani kiasi kwamba hawapati ku-*concentrate* katika somo au jengine. Kwa hivyo, imesababisha wanafunzi wengi kukimbilia masomo ya ziada na kwa nini hakuna utaratibu maalum?

Sasa labda ningependa kuona kwamba wizara inasimamia ikiwa kama ni *tuition* basi skuli baada ya kwisha kufanya *analyze* wakajua kwamba hili ndilo tatizo, basi wakaandaa utaratibu ikawa zile *tuition* zinafanyika katika skuli zile zile na walimu wakarejea na baadaye kupatiwa posho maalum, ili tukapata mfumo mzuri wa elimu pamoja na kiwango kizuri cha elimu.

Kwa kweli huu mpango tunaokwenda nao hivi sasa unasababisha mambo mengi, wakati mwengine tunasikia mwanafunzi amebakwa au ametiwa mimba na mengineyo. Sasa kuepusha hayo, nadhani hizi ni vyema kutafutiwa utaratibu maalum.

Mhe. Mwenyekiti, wizara pia inao utaratibu wa kuwaruhusu vijana au walimu wetu kwenda masomoni. Kwa kweli sina uhakika, lakini nafikiri kuna utaratibu ambao kama mwalimu hajafikia miaka miwili kufundisha hapati fursa ya kwenda kusoma. Kwa hivyo, nadhani hivi sasa tungeondokana na suala hilo, kwa sababu zamani mara nyingi tulikuwa tunaokwenda kusoma masomo ya juu inakuwa aidha ni serikali au pengine ni *scholarship* ambayo inatokana labda nchi fulani imefadhili lakini kupitia kwa serikali. Sasa ilikuwa utaratibu wake kidogo tafauti na wale.

Kwa mfano, hivi sasa inawezekana kwamba kijana anayekwenda kusoma amepata ufadhili wa Mjomba wake au pengine Ami yake ni Mwakilishi ama Bunge au mtu fulani. Sasa inapotokea ile fursa tukimnyima kwa wakati ule, mwaka unaofuatia hatoweza kupata ule ufadhili, kwa hiyo atakosa ile fursa ya kwenda kusoma.

Mhe. Mwenyekiti, naomba suala hili likaangaliwa tena, ili hawa watu wanaopata fursa kwa wakati basi wakatumie ule wakati wakeenda, lakini kinyume cha hayo inakuwa mara nyingi tunawa-*discourage* na wakati mwengine unakuta mtu yuko tayari aache kazi, ili aende kusoma na anaporejea, basi anakuwa hana tena *interest* hata kujiunga na hizo Skuli za Serikali na kuona ah! bora niende katika Skuli Binafsi ambazo pengine huduma zake zinakuwa nyingi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, kama sisahau miaka ya 1970's serikali yetu iliamua kwa makusudi kuziweka baadhi ya skuli katika mfumo wa vyuo vya kutoa huduma. Kwa mfano, nakumbusha tu mwaka 1977 Skuli ya Sekondari ya Fidel Castro iliwekwa katika mfumo wa Chuo cha Kilimo na tukaitangaza rasmi ni kuwa Fidel Castro *College of Agriculture*, hiyo inakwenda sambamba sana Skuli ya Lumumba ambayo nayo ilitangazwa ni Skuli ya kutoka Mafunzo ya Uvuvi na Skuli ya Mbweni Mafunzo ya Ufundi. Maalum, Mainjinia pamoja na Skuli ya Mikunguni ambayo ilikuwa ikitoa Mafunzo ya Umeme.

Hivi sasa serikali ina lengo kubwa la kufanya Mapinduzi ya Kilimo. Mhe. Mwenyekiti, ninachokiona ni kwamba kama vile haiba yake iliyokuwa ipo miaka ile imeondoka, kwa sababu wataalamu wetu wengi sana tulionao wa kilimo, basi walitokea katika skuli hizi za Fidel Castro na wale walijifunza fani za uvuvi pia walitoa kwenye vyuo vyetu hivyo, pamoja na mainjinia wengi wetu wa meli walitokea katika Skuli ya Mbweni.

Lakini nashangaa vyuo hivi sasa vimeondoka na haiba hiyo haipo tena, sasa sijui serikali au wizara imesahau kama tunavyo vyuo hivyo ambavyo vilikuwa vinatoa huduma kama hizo na hivi sasa vimewekwa nyuma kiasi kwamba vinatoa elimu ile ya kawaida. Kwa hivyo, nadhani tungeviangalia vingeliweza kusaidia kutoa wataalamu, ambao baadaye wangelipatiwa kozi za juu katika fani za kilimo ambazo kwa hivi sasa ndio kipaumbele chetu na tumekusudia kuingia kwenye Mapinduzi ya Kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa kweli kuna upungufu wa walimu na hilo halifichiki. Taarifa tuliyonayo ni kwamba wizara inakusudia kuwaajiri wafanyakazi au walimu 800 na tunazo skuli 700 na kimahesabu sijui tunakwenda na *ratio* gani, labda *ratio* itakuwa ni 1.25 pengine.

Kwa hivyo, kama tumekusudia kweli basi tungefanya utaratibu wa kuongeza walimu hawa hawatoshi ni kidogo, kwa sababu walimu 800 kwa skuli 700 ambazo tulizonazo ki-*ratio* itakuwa tupo pale pale na kila siku skuli zinaongezeka, nadhani ni vyema tukafanya utaratibu mwengine wa kuongeza walimu hawa bado.

Kwa mfano, wapo walimu waliosomea masomo ya cheti nafikiri kuna karibu *bench* nne bado hawajaajiriwa na wao wametumia fedha za wananchi katika kusomeshwa na wao wenyewe. Mhe. Mwenyekiti, nadhani tungeandaa utaratibu mwengine ili na wao hawa tukawapa ajira kwa ajili ya kupunguza huu upungufu wa walimu.

Sasa ikiwa ni hivyo Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa kweli skuli zetu utakuta kuna walimu ambao hawana fani ya *science* na tunawapeleka kwenda kusomesha masomo ya science na hili ni kosa. Kwa kweli ikiwa mtu ame-*specialize science* basi wawe mwalimu wa *science* na asiende kusomesha *art*.

Sambamba na hilo kuna walimu ambao wanatoka *primary* wanakwenda kusomesha *secondary*. Mhe. Mwenyekiti, hapa itakuwa ni kudanganyana, kwa sababu uwezo wake haupo au hana uwezo wa kutoka *primary* na kwenda kusomesha *secondary*. Kwa hivyo, kama tunao nia kweli ya kutafuta *quality* ya *education* basi haya tusingeliyaendeleza na hapa itakuwa tunawadanganya, ndio maana leo utakuta kila mtu ukifika nyumbani watoto hawapo wamekwenda *tuition*, kwa sababu walimu wetu uwezo wao pamoja na mparaganyo tulionao ndio unaosababisha haya.

Vile vile hapo zamani tulikuwa na *specialization* na hivi sasa tunayo nia ya kufanya masomo ya *science* yapendwe au yasomeshwe kwa ziada katika skuli zetu. Sasa utakutia tunayo masomo mwanafunzi anaingia kidatu cha 9 (*Form I*) katika masomo ya sayansi na mwengine akaingia katika masomo ya *art* ili kumpunguzia ule mzigo kwa sababu yeye yuko katika masomo ya sayansi atajua *specialize* masomo yangu, matano kwa hivyo *consultation* ya masomo yake itakuwa ni kubwa na nina imani kwamba na ufahamu wake utakuwa ni mkubwa. Na yule wa *art* nae atafanya hivyo tukaendelea na mfumo huo moja kwa moja ili kuboresha hii sekta ya elimu, si hivyo itakuwa tunachanganya na tunakwenda na hatujui tutafikia wapi.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa utaratibu wetu ni kwamba tunatoa elimu ya lazima mpaka vijana wetu wa *FORM* II vijana hawa kimazingira yetu ukimaliza unakuwa na miaka kumi na 17 au kumi na 18, kiilivyo inakuwa bado hujawa nguvu za kuingia sekta nyengine zinakuwa hazipo. Kwa hivyo mimi ningependekeza kwamba hii elimu ya msingi tukaiongeza au ya lazima tukaongeza tukafikia *FORM* IV angalau yule kijana ambae atatoka katika kipindi hiki au awamu hii akawa na uwezo wa kusema sasa unakwenda kumfundisha ufundi stadi au anaweza kuingia katika fani yoyote ya ajira.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala ambalo ni sera ya taifa la elimu bila ya malipo, utaratibu huu tulionao hivi sasa ni mzuri kwa sababu tunadumisha moja katika

maagizo ya viongozi wetu wakuu, lakini utaratibu wetu tunaotumia hivi sasa nafikiri unahitaji ufanyiwe mapitio, hivi sasa wanafunzi wetu wengi tunawatumia katika shughuli kama hizi za michezo na likianza tamasha hili tunakuwa karibu miezi minne, mitano tumo katika mbio hizi na wanaochangia zaidi katika kufanikisha masuala haya wanakuwa ni wale wale walimu ambao tunawabebesha mzigo mkubwa au shule tunaibebesha mzigo mkubwa katika kufanikisha utaratibu huu.

Kwa hivyo mimi nafikiri tungeuangalia utaratibu huu kwa njia nyengine, badala ya kuwa kila mwaka tunayafanya maazimisho haya basi tukatafuta utaratibu unaofaa labda wa kupunguza ule mzigo wa maskuli na kuwashughulisha wanafunzi, tukawaachia tukawapa muda wakawa wanasoma na haya maazimisho yakatafutiwa muda maalum kama baada ya miaka mitatu ndio tukayaandaa.

Mhe. Spika, mimi baada ya kusema hayo machache naomba niunge mkono hoja mia juu ya mia. *(Makofi)*

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti kunipa fursa hii asubuhi ya leo na mimi kuchangia machache katika wizara hii ya elimu na mafunzo ya amali, kwanza na mimi napenda nimshukuru Mhe. Waziri kwa kutuletea bajeti yake hii hasa ukizingatia kwamba elimu ndio mti wa mgongo wa kila kitu kwa mwanadamu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nianze kwa kuzungumza haya machache ambayo nitakuwa nayo, katika kipindi tulichokuwa nacho zama hii tuliyokuwa nayo sasa hivi Zanzibar Mwenyezi Mungu katukirimu neema ambayo tulikuwa hatunayo kwa muda mkubwa nyuma tuliokuwanao, katukirimu serikali hii ya umoja wa kitaifa ambayo kuwa imepunguza matatizo mengi tuliyokuwa nayo ya kutoaminiana, kutohurumiana, kutostahamiliana na mengine mengia ambayo yalikuwa yakijitokeza.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko katika Wiara hii ya Elimu naona bado katika Wizara hii kuna watu ambao kuwa bado wao wakiendeleza mapambano kwa sababu hawajakubali na kuna baadhi ya walimu hawajakubali suala hili tulilonalo zuri la serikali ya umoja wa kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa nini niseme hivyo karibu katika jimbo la Kaskazini ya Unguja yaani Nungwi jimbo ambalo kuwa linaongozwa na Naibu Waziri wa Nishati kwa jitihada yake Mheshimiwa huyu alifanya jitihada ya kupata muhisani, kutafuta mfadhili ambaye ameshirikiana na kampuni ya maisha, kampuni hii ilimsaidia Mhe. Naibu Waziri kwa kuomba vitu mbali mbali

ambavyo kuwa ni vitu vya hospitali, vya skuli na vitu vyengine ambavyo vilikuwa vimepatikana. Bahati nzuri aliwaalika wahusika wakaja wahusika wale watu wa afya kama ni vitanda na magodoto na mambo mengine aliwasaidia na Wizara ya elimu kupata vitabu na kompyuta na itu vyengine.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko kuna mwalimu Mkuu wa Skuli ya Nungwi alimuita kama alivyowaita wengine kuja kuchukua vile vifaa kwa masikitiko mpaka sasa hivi kuna kompyuta 8 na vitabu vya kufundishia wanafunzi mwalimu huyu hakwenda, kwa sababu tu vitabu vile vimetolewa na Naibu Waziri wa chama cha CUF.

Mhe. Mwenyekiti huyu mwalimu anatupeleka wapi huyu sisi mambo hayo tumechoka nayo kwa hivyo namumboa Mhe. Waziri amwite mwalimu Mkuu huyu na amueleze wazi kwamba tumechoka nayo tunapokwenda sasa hivi tunakwenda na serikali ya umoja wa kitaifa, tunayohitaji ni maendeleo. Leo waziri katafuta vifaa vya kufundishia watoto mwalimu anakataa kuvichukua kwa sababu vinatokana na Naibu Waziri CUF sisi tuntaka kupata maendeleo hatutaki kurejeshwa nyuma.

Mhe. Mwenyekiti namuomba Mhe. Waziri mwalim Mkuu huyu wa Kuli kya Nungwi amwite amuonye asiturushe nyuma tunakotoka, sisi tunasokea mbele haturudi nyuma tena asiturudishe nyuma, kwa nini afanye hivyo avikatae vifaa hivi nab ado mpaka leo hivi vifaa viko kama Mhe. Waziri unavitaka wewe neka ukavichukue. Ushahidi upo vifaa vipo, kwani hao wengine waliovichukua sio binadamu, kwa hivyo vile vifaa sisi vimeletwa kwa ajili ya kuwasaidia watoto wetu. Mhe. Waziri nakuomba huyu mwalimu uzungumze nae asiturudishe nyuma.

Mhe. Mwenyekiti, hilo natoka hapo sasa nakwenda kuna skuli hii ya Bweni hapa yaani Chuo Kikuu cha Kiislam cha Mbweni, lakini sasa hivi naona hiki chuo kimebadilishwa jina sio chuo tena cha kiislam Mbweni sasa ni skuli ya Mbweni, hivi kulitokea tokea nini mpaka hili jina la Chuo libadilishwe na kisiwe tena chuo cha Kiislam Mbweni. Kwa sababu mimi ninavyojua Unguja chuo cha Kiislam kilikuwa ni Mbweni na kule Micheweni Pemba ndio kuna chuo cha kiislam, lakini leo kimebadilishwa jina na hakuna tena lile jina la chuo cha kiislam Mbweni. Basi namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atueleze kulitokea nini au kuna nini mpaka libadilishwe lile jina na sasa kisiwe tena Chuo cha Kiislam.

Mhe. Mwenyekiti, pia sasa hivi napenda kuzungumzia Chuo cha Kiislam kilichoko Micheweni, kipini cha bajeti zinazopita za miaka mitano nilikuwa napiga kelele kama hivi na leo nasema tena, namuomba Mhe. Waziri anieleze

hivi kule Chuo cha Kiislam Micheweni kuna sababu zipi za msingi mpaka wale watu wakoseshe usafiri kuwe kuna gari lile la kubebea mizigo la makuni, ndio gari wanalopewa chuoni ndio gari ambalo kuwa alikuwa akilishughulikia Naibu Waziri juzi akasema kuna gari, gari lenyewe ni TATA limeshachoka kabisa la kiaka na miaka, chuo kile cha kiislam mpaka leo hawajapewa usafiri wala hakuna usafiri wa aina yoyote, chuo kipo mbali na hospitali, watoto wakiumwa hakuna wanafunzi wanaosoma hakuna gari la kuwapeleka hospitali,

Hivi huyu mtu ikiwa anaumwa umpakie gari lile mpaka umfikishe huko hospitali ni mzima tena na barabara ile mbovu, kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri bado namuomba na atakapokuja anipe maelezo mazuri kuhusu suala la Chuo cha Kiislam kilichoko Micheweni hivi tutakwenda vile mpaka lini.

Suala jengine kile ni chuo cha Kiislam kipindi kilichopita nilisema kama haistahiki chuo kile mpaka leo kuwe hakuna msikiti, wanafunzi waliopo pale zaidi ya watu 600 vyumba vile vya walimu ndio vinavyofanywa msikiti ndio watu wanamoswalia, halafu chuo kile tunakiita Chuo cha Kiislam hivi jamani hatuoni kama ni aibu. Hata wakija wageni tukiwaambia hiki ni chuo cha kiislam lakini hakuna hata msikiti wa kuswalia miaka nenda napiga kelele lakini naona kelele zangu zinagonga ukuta, kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri masuala haya atakapokuja anieleze mpaka niridhike maana kama sijaridhika nitakuwa mkaidi kweli kweli kwa suala hili.

Pia kile chuo kinahitaji kujengewa uzio kwa sababu kiko wazi, kile chuo kinafanya kazi kwa wanafunzi wetu kutoka sehemu mbali mbali za Unguja na Pemba , kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri aone kama kile chuo kuna haja ya kuboresha kweli kiwe Chuo cha Kiislam. Chuo kinafanya kazi vizuri, kinatoa wanafunzi wazuri kinapasisha vizuri kwa hivyo kuna haja ya kile chuo kuenziwa. Namuomba Mhe. Waziri aone kama kile chuo ni chetu cha Zanzibar na akienzi.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo bado Chuo cha Kiislam kuna hakuna metron, hakuna wapishi, wapishi waliopo wanajitolea mwaka wa nne huu wanafanya kazi ya kujitolea. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri aone kama wale wapishi waliopo pale basi angalau waajiriwe na huyo metron aone kama kuna haja ya kupatikana metron kwa sababu metron ndio mchungaji wa wanafunzi waliopo pale wa kike, leo chuo kinakwenda tu hakina metron. Kwa hivyo naomba Mhe. Waziri aone hilo.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine naomba nizungumze kuhusu skuli zangu za Jimbo la Micheweni, skuli ya msingi ya Micheweni ina madara kumi na mbili lakini madarasa manne tu watoto wanayokaa katika vikalio madarasa nane

hayana vikalio watoto wanakaa chini. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri awaangalie kwa jicho la huruma aone watoto wetu kukaa pale chini ndio tunawadumaza kiakili kwa hivyo serikali ifanye jitihada kupitia wizara yake kuwapatia vikalio wale watoto wa skuli ya Micheweni.

Suala jengine ni kwamba skuli ya Micheweni mwalimu wa sayansi hapana sekondari ya Micheweni, mwalimu aliyekuwepo pale ni mwalimu anayetoka Chuo cha kiislam apate zamu aje pale afundishe fundishe watoto siku mbili atoke na huyo mwalimu aliyepo inasemakana kwamba karibuni atakwenda kwenye likizo ka hivyo pale patakuwa ni pakavu kabisa hapana.

Hao walimu wa kawaida waliopo pale hawatoshi Mhe. Waziri ana mpango wa kuajiri walimu 800 lakini kama walivyosema wenzangu kwamba walimu mia nane ukilinganisha na skuli tulizokuwa nazo mia saba hawatoshi. Kwa sababu itakuwa kila skuli ni mwalimu mmoja tu, kwa hivyo naomba Mhe. Waziri ili kukuza watoto wetu kielimu aone kama kuna haja ya kuongeza walimu na hasa ukizingatia kuna walimu ambao kuwa wameshamaliza masomo ya elimu ya ualimu lakini hawajaajiriwa, kwa hivyo waone kwamba kuna haja ya kuwaajiri hawa watu ili kusaidia watoto wetu.

Mhe. Mwenyekiti suala jengine ni kwamba kuna walimu waliomaliza kusoma diploma lakini walimu hawa tangu mwaka 2007 lakini bado hawajalipwa *area* zao ambao walikuwa kwenye masomo, kwa hivyo na hili naomba aone kwamba sasa tuko mwaka 2011 tangu mwaka 2007 bado walimu hao wameshamaliza kusoma lakini *arrears* zao hawajalipwa, kwa hivyo na hili namuomba Mhe. Waziri aone kwamba kuna haja ya kulipwa, waliolipwa ni Unguja tu lakini Pemba wote hawajalipwa kwa hivyo na hili Mhe. Waziri alishughulikie nao wale wapate *area* zao.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ni suala la walimu kuwapunguzia michango kwa sababu tulisema juzi katika suala hapa, Mheshimiwa Naibu Waziri akasema ile ni michango ya hiari sio michango ya hiari kwa sababu kama ni michango ya hiari walimu wasingelalamika, lakini walimu walio wengi wanalalamika michango imekuwa mingi nao, kuna mchango wa mwenge kuna siku ya walimu wengine wanachangia TC wengine wanachangia siku ya Tamasha sijui la nini.

Kwa hivyo Mheshimiwa hii michango ipunguzwe kwa walimu mishahara yao nao wale haiwatoshi halafu tunawaongezea michango mingine kuwachangisha michango ambayo kuwa serikali ina uwezo wa kuibeba wenyewe. Namuomba Mhe. Waziri wakae wazingatie waone kama kuna haja ya kuwapunguzia mzigo walimu, michango iliyokuwa sio ya lazima mingine iwachwe na mukisema sio

michango ya lazima haiwezekani kwa sababu mwalimu hawezi kuwa wenzake wote wameshatoa yeye asitoe, inakuwa ni mchango wa lazima kwa hviyo naomba na hili alione Mhe. Waziri awapunguzie mzigo huu walimu.

Mhe. Mwenyekiti suala jengine naomba Mhe. Waziri aone kama Ofisi iliyopo ya Wilaya ya Micheweni wao wenyewe wafanyakazi wa serikali Ofisi ya Micheweni hawatoshi ofisi yenyewe ni finyu, hapa kuna Afisa wa Wilaya wa elimu yupo pale pale kajiweka kwenye chumba na chumba chenyewe hakitoshi hakikidhi haja. Kwa hivyo namuomba Mhe, Waziri aone kwamba kuna haja ya kufanya utaratibu wa kupata Ofisi ya Elimu ya Wilaya pale Micheweni japo kama ni kibanda kidogo chenye vyumba viwili tu lakini wapate wajue kwamba hii ni ofisi yetu tumekaa, kuliko kujipenyeza mule kwenye vijichumba ambavyo havitoshi, naomba na hili nalo Mhe. Waziri alitizame na aone kwamba kuna haja ya kupata ofisi, kwa sababu viwanja Micheweni tunavyo havina tabu kwa hivyo kuna haja kusimamia hili suala akaona inapatikana Ofisi ya Wilaya ya Elimu katika Wilaya yetu ya Micheweni.

Mhe. Mwenyekiti kwa haya machache naomba niunge mkono hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Elimu, lakini baada ya Mhe. Waziri kunipa ufafanuzi wa Chuo cha Kiislam kwa kina. Ahsante sama. *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru tena anayepaswa kushkuriwa Mwenyeti Mungu mtukufu kwa kutujaalia asubuhi ya leo kukutana hapa tukiwa hai na wazima wa afya, kuendelea na mjadala kwa masuala ambayo yanaigusa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, pili nikushukuru na wewe kwa kunipatia nafasi hii naamini utanipa muda wa kusema yale niliyokusudia kusema ambayo naamini yataisaidia wizara hii katika kuzidi kujipanga vizuri zaidi.

Tatu nimpongeze Mhe. Waziri ndugu yangu Ramadhani Abdalla Shaaban ambae ni mmoja katika Mawaziri wa zamani katika Baraza hili na Naibu wake Ndugu yangu Zahra Ali Hamadi, Katibu Mkuu ambae ni Mwalimu wangu Bimwanaidi na viongozi wote na watendaji wa wizara hii ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya kutujengea msingi wa taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti hakuna asiye fahamu umuhimu wa elimu, elimu ndio msingi wa maendeleo na mataifa yaote duniani yanayoendelea na yaliyoendelea yameendelea kwa sababu ya kuweka mkazo katika elimu, Zanzibar ina historia kubwa sana katika elimu ni katika nchi chache Afrika ambazo ziliona mapema umuhimu wa kuendeleza elimu, na rekodi za Kikoloni zinaonyesha wakati

Zanzibar inapata uhuru wake ilikuwa ni miongoni mwa nchi chache sana Afrika nadhani ni nchi tatu tu ambazo zilikuwa zikijitosheleza kwa mahitaji yake ya wataalam katika kila fani na hata uwezo wa kutoa wataalam na kupeleka katika baadhi ya nchi.

Lakini hapa kati kati Mhe. Mwenyekiti tukapata msuko suko kwa sababu ya lengo la kutaka kupanua zaidi huduma za elimu ziwafikie watu wengi zaidi, kwa hivyo uwezo wetu ukawa mdogo kuliko na matokeo yake ndio maana baadhi ya sekta zikaathirika, lakini nafurahi Mhe. Mwenyekiti kwamba sasa inaonekana tunaelekea katika kuipa elimu nafasi yake na dalili moja jana nilikuwa nikiwambia wenzangu ukikitizama kile kitabu cha hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mawasiliano lile jengo jipya la Air Port ukitizama ile *shape* yake ni kama kitabu. Nikasema kwamba ni dalili nzuri kwamba mtu akiingia Zanzibar anakaribishwa na kiwanja cha ndege ambacho kinaonyesha mwelekeo wa taifa ilivyokusudia kwa kuipa stahiki elimu.

Mhe. Mwenyekiti baada ya kusema hayo sasa naomba nielekee kwenye mchango wangu kwanza kwa kusema kuungana na Maalim Rashid Seif Muwakilishi wa jimbo la Ziwani aliposema kwamba, kama tunataka kujenga taifa ambalo linathamini elimu tusiwe tu tunakwenda kwa mazoe kama tunavyokwenda kila siku lakini lazima tujipange katika hali ambayo inaonesha jinsi tunavyosomesha watoto wetu inalenga kujenga taifa la aina gani. Mhe. Mwenyekiti mfumo wa elimu tuliokuwa nao ni ukweli usiopingika kwamba tumeuridhi katika mfumo wa kikoloni wa kielimu, mfumo wa elimu wa kikoloni ulikuwa unawajenga zaidi watu kutii maagizo, hautoi nafasi ya kumjenga mwanafunzi kuwa mbunifu, anayeweza ku-*challenge* vitu.

Kwa sababu angepewa elimu ya aina ile ange-*chalenge* ile *system* ambayo ilikuwa inatawala wakati ule, sasa tuna miaka hamisini tumejitawala kama ni hivyo Mhe. Mwenyekiti, maana yake na mfumo wetu sasa ubadilike, sasa katika hili nataka kutoa wito kwa wizara ya elimu na serikali kwa ujumla wake, hebu wakae watazame kwa kutizama *vision 2020* kwa kutizama MKUZA kwa kutizama mipango mingine ya muda wa kati na muda mrefu tunataka kujenga Zanzibar ya aina gani. Kisiasa, kiuchumi na kijamii tukishalijua hilo dhamira kwa sababu tunazo hizo *document* zinazotuongoza huko, sasa hapo badi mfumo wetu wa elimu uandaliwe kutekeleza ku-*suply* watu ambao wataweza kuhudumia ile jamii wanayotaka kuijenga.

Kwa hivyo kama tunakusudia Zanzibar kuwa ni *service centre* katika Afrika ya Mashariki tuone mfumo wetu wa elimu unatoa kiasi gani wataalam watakaoweza kuhudumia hizo *service* tusije tukafika pale ikawa ni *service centre* Zanzibar lakini wataalam wetu wote wanatoka nje ya Zanzibar kwa

sababu sisi wetu hatukuandaa, mfumo wetu wa elimu hatukuelekeza kule. Kama unataka kujenga Zanzibar iwe ni kituo kikuu cha biashara au kituo kikuu cha huduma za fedha kwa Afrika ya Mashariki basi tuone mfumo wetu wa elimu unatuelekeza huko. Kama unataka kujenga uchumi wa kitalii basi tuelekee huko, na kama tunataka kujenga uchumi wa uzalishaji wa mafuta na naamini tunataka kuelekea huko basi na mfumo wetu wa elimu tuelekeze huko.

Kwa hivyo nilikuwa naomba jambo moja kwa jumla kuanzia mitaala, uendeshaji wa sekta hii ya elimu na kila kitu kijielekeze kuwe kuna *syncronize* na nadhani juku la kufanya hivyo katika serikali zima kwa ujumla ni tume ya mipango, tuone kwamba isiwe kila mmoja anafanya kivyake vyake tu lakini tuone na ile mipango inayoandaliwa yote ukiunganisha inakuelekeza mahala pamoja ambapo ndio shabaha ya nchi yetu. Kwa hivyo huo ulikuwa mchango wangu wa jumla ambao nilitaka niseme.

La pili nije katika walimu Mhe. Mwenyekiti, hatuwezi kuzungumza elimu bila ya kuzungumza walimu, tunaambiwa kwa muda mrefu serikali kwamba takriban asilimia thamanini au zaidi ya walimu watu wamepata mafunzo, kwa hivyo ni *traning teacher* lakini kama ni hivyo Mhe. Mwenyekiti, tungetegemea kwamba pasiwe na *out put* ya walimu hawa ambao tunaambiwa wamepewa *traning* kwa asilimia thamanini ingeonekana katika kiwango cha kufaulu, lakini kiwango cha kufaulu kama anavyosema Mhe. Rashid Seif ni kile cha kwamba tunaridhika mtu kapata cheti, akishapata *Divishen four* tunasema huyo kafaulu. Lakini katika kipimo tungeona wangapi wametoka katika ngazi moja kwenda katika ngazi nyengine, hili mimi nafikiri Mhe. Mwenyekiti wizara iliangalie tena suala hili la walimu.

Mhe. Mwenyekiti katika kuangalia hili tusiangalie katika mafunzo tu lakini na maslahi yao vile ile ari ya walimu ya kusomesha imeshuka kwa sababu ya maslahi yao ni madogo, kwa muda mrefu *scheme of service* zilikuwa hazitekelezwi, sasa nafurahi kwamba mara hii Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora kasema kwamba ataangali masuala haya ya miundo ya utumishi kwa ujumla wake. Ningeomba katika kuangalia miundo ya utumishi kipaumbele kwanza kwa sekta ya elimu, kwa sababu kama nilivyosema jamii ambayo haiendelezi elimu haiwezi kupata maendeleo ya namna nyengine yoyote. Kwa hivyo suala la walimu lizingatiwe san asana katika kuwaboreshea au kufanya huduma zao kuwa bora zaidi Mhe. Mwenyekiti.

Suala jengine katika walimu Mhe. Mwenyekiti pengine kwa sababu ya uwezo wao mdogo walimu wetu wengi wanasomesha wanafunzi ambao viwango vyao vya elimu haviruhusu, huko nyuma tulikotoka kulikuwa kumewekwa ili

mwalimu asomeshe daraja hili anapaswa awe na *Degree hii* lakini sasa hivi mambo hayo yamepungua sana kutokana na uhaba wa walimu tulionao, kwa hivyo katika mipango na hili litizamwe. Mhe. Mwenyekiti, jengine katika walimu ni kwamba hata hao wachache tuliokuwa nao hasawambazwi kwa uwiano, kasema Mhe. Rashid Seif hapa ukitizama sera ya elimu inazungumzia kuwepo kwa uwiano, lakini je uwiano huo upo kwa skuli za mjini na mashamba baina ya Unguja na Pemba isiwe tunaendeleza elimu lakini ikawa ni eneo fulani tu la kijografia ndio linaloneemeka kwa maana pana hakuna uwiano wa kusambaza hao walimu ambao wana uwezo.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo nizungumzie mahitaji ya walimu ni nyumba za walimu mara nyengine tunapiga kelele kwamba walimu hatuwezi kuwasambaza na wanakuwa hawataki kwenda kufanya kazi katika maeneo mengine, au wakifika wanafanya kazi chini ya kiwango kinachotakiwa kwa sababu hakuna motisha na motisha wenyewe ni nyumba za walimu Mhe. Mwenyekiti, unampeleka mwalimu shamba unamuhamishia aende Pemba akifika kule hakuna nyumba ya walimu tofauti na ilivyokuwa zamani, nafurahi katika ile skuli mpya mara nyingi uliyiokuwa ukitwambia Mhe. Waziri hapa kwamba mbali ya mambo mengine pia kuna nyumba za walimu, sasa nitegemee kwamba hii ndio iwe *standard* kwa skuli nyengine zote.

Mhe. Mwenyekiti mimi nadhani kuna haja sana ya kuangalia hili suala la walimu lakini niseme pamoja na kutoa wito huu mimi nimeshtuka na naomba akija Mhe. Waziri anisaidie hili , nilipoiangalia bajeti ya Wizara yake katika hii Idara ya Mafunzo ya Ualimu naona bajeti yake imeshuka sana

Mhe. Mwenyekiti, bajeti ya mwaka huu iliyotengwa ni Shs. 130 milioni mwaka jana makizio ilikuwa ni 140 milioni. Mwaka 2009/2010 hasa ilikuwa ni Shs. 360 milioni na mwaka 2008 ilikuwa 352 milioni, sasa imetoka 352 milioni mia 360 milioni ghafla imeshuka imekuja 140 milioni mwaka huu imeteremka tena imekuja 130 milioni.

Sasa kama nilivyosema hii tumeipata katika kitabu cha *estment* kwenye ukurasa 323, sasa kama tunasema walimu ndio roho ya kuendeleza elimu, lakini huku bajeti ya mafunzo ya ualimu yanateremka kwa kasi kiasi hiki sijui tunafanya nini naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, katika walimu vile vile pamezungumzwa suala la uhaba wa walimu katika fani za sayansi, hesabu na kiingereza. Hapo nyuma palikuwa na utaratibu wa kupata msaada kupitia kwenye mashirika ya *Voluntary Services Overseas* la Uingereza na *Peace Corps* ya Marekani wakisaidia kutoa elimu ambayo walikuwa angalau wanatusaidia kwa kiasi fulani. Sijui Wizara

inamejipanga vipi kuendelea kutumia fursa kama hizi na za wale walimu wengine kutoka nchi mbali mbali ambao zamani nakumbuka wakija katika maskuli yetu wakisaidia angalau kuziba mapengo.

Baada ya kuzungumzia suala la Elimu Mhe. Mwenyekiti, nije suala la tatu suala la vifaa katika sekta ya elimu. Hapa naomba nigusie kwanza vitabu vya kufundishia. Tuna tatizo kwanza la *standard* ya vitabu vyenyewe. Katika hili Mhe. Waziri na uongozi mpya wa Wizara ya Elimu utupie macho katika ile *section* yake inayohusika na kuthibitisha zile kampuni zinazopewa kazi ya ku-*supply* vitabu katika maskuli yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna manung'uniko huko nje sina ushahidi nayo lakini yapo manung'uniko hayo kwamba mara nyengine kuna watu na *interest* zao katika hili kwa hivyo kampuni zinazochaguliwa hazichaguliwi kwa ubora wa vitabu wanavyoviwasilisha lakini kwa sababu pengine watu fulani na maslahi yao. Kwa katika hili namuomba Mhe. Waziri akija anithibitishie wanaliangalia kiasi gani hili.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo niseme katika vitabu Zanzibar tunao waandishi, kuna vitabu hasa katika mfano maeneo ya lugha Kiswahili, Kiingereza, historia, kamusi, mashairi, sarufi ya Kiswahili, tamthilia, vitabu vya watoto, kuna vitabu 64 vilivyoandikwa na Wazanzibari katika fani mbali mbali. Hivi havipewi nafasi katika skuli zetu. Vyengine humu nimepewa maelezo na wataalamu wanasema vinatumika kufundishia mpaka Kenya lakini hapa kwetu havipewi nafasi. Mpaka pamejengeka dhana kama vile Wizara ya Elimu huko nyuma tulikotoka pengine kwa uongozi uliokuwepo ilikuwa mwandishi wa vitabu vya Kizanzibari hathaminiwi na wizara hii. Ili kitabu kikubalike awe aliyeandika sio Mzanzibari.

Kwa hivyo naomba baadaye nitampatia ili avitizame, halafu aone ni kiasi gani anaweza kuangalia uwezekano. Lakini hata hawa watunzi wa hivi vitabu ni kiasi gani tunawathamini, tunawakumbuka. Mhe. Mwenyekiti, nadhani hili ni muhimu sana kuliangalia katika vitabu vya kufundishia. Pia kuna matatizo katika maabara sina haja ya kuyarejea yamazungumziwa sana. Kama tunakusudia kuimarisha elimu ya sayansi hatuwezi kuimarisha hiyo kama skuli zetu hazina maabara.

Mhe. Mwenyekiti, katika kampeni vyama vyetu vyote viwili CUF na CCM vilikuwa vikiahidi kwamba vikiingia serikalini basi kutakuwa na kompyuta katika kila skuli pengine kwa kila mwanafunzi. Nakumbuka wengi walikuwa wakiliegemeza hili kwa msaada uliokuwa umeahidiwa na Wamerakani. Humu nilichokiona katika hotuba ya Waziri ni kwamba kunategemewa kila skuli

kupata kompyuta. Lakini hebu tuambiwe lile la kila mwanafunzi kupata, na siku hizi kuna mfano makampuni ya kama ya Bill Gates yanatoa komyuta za *standard* ndogo ya kuanzia wanafunzi wa kiwango cha chini kwa bei nafuu kabisa. Tumeambiwa *Bill Gates* keshawahi kuja mpaka kulala Zanzibar kwa kuipenda Zanzibar. Sasa hivi hatuwezi kumu - *approach* badala ya kuishia Dar-es-Salaam pia tukamu- *approach* akaja hapa Zanzibar, tukamuomba vitu kama hivi, pengine tungeweza kupunguza mahitaji ya yetu ya vifaa kama hivi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nipongeze nimefurahi sana kuona kwamba Wizara ya Elimu sasa imeanzisha Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu. Niliwahi kulizungumza suala hili mara moja katika Baraza hili nilipoingia. Kwa wenzetu katika nchi za *Commonwealth* kwa mfano Uingereza, Mkaguzi Mkuu wa Elimu ni mtu mwenye nguvu sana. Hii ni idara ambayo inayojitegemea hasa na kule kwa wenzetu anatoa ripoti kila mwaka *independent* haipo chini ya Wizara ya Elimu wakishakagua, yeye anakagua utendaji wa Wizara ya Elimu. Ripoti ile huwa inafikishwa mpaka katika Bunge la Uingereza kwenda kujadiliwa, ili kuona wapi pana mapungufu parekebishwe na wapi pana nguvu ziongezwe.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nadhani kwa sababu sasa wizara imekusudia kuanzisha afisi hii baada ya kuwa na Idara ya Ukaguzi kukawa na Afisi ya Mkaguzi Mkuu. Basi tuone kuwe na utaratibu wa kutoa ripoti nazo zinaletwa hapa ili zitusaidie.

Mhe. Mwenyekiti, la nne nije kwenye suala la mitaala. Nadhani Wizara inahitaji kuangalia mitaala yetu. Kwa mtazamo wangu bado mitaala ni mikubwa sana, masomo ni mengi, haizingatii mahitaji ya wanafunzi. Kama nilivyosema pale mwanzo sina haja ya kurejea kwamba bado imejikita katika ule mfumo uliorithi wa kikoloni. Hebu tuangalie mitaala yetu katika hali ya kisasa hali ambayo itapunguza wingi wa masomo kwa kila mwanafunzi lakini itasaidia kuwa na wafunzi wetu tangu mapema wakitoka wanajielekeza wapi ambapo wanataka ku- *specialize* ili kusaidia ku-*supply* mfumo wetu wa elimu.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Elimu ya Juu, hapa kuna nukta mbili ninazotaka kuzizungumzia. Kwanza kuna wanafunzi ambao tunawa–*sponsor* kuwapeleka katika vyuo mbali mbali vya Tanzania Bara na vyengine vya nje ya nchi, lakini hata vya hapa ndani. Kuna maneno Mhe. Mwenyekiti, naomba Waziri akija atusaidie hapa kwamba hii *crisis* tunayoipata mara kwa mara ya wanafunzi wetu kushindwa kupelekewa fedha kama ambavyo wameahidiwa katika mikopo na mambo mengine, na hivyo kudhalilika mara nyengine wanafanya mitihani katika hali ngumu kabisa.

Tuliopitia katika elimu ya juu tunajua ugumu wa kufanya mitihani ukiwa bado una mambo mengine hayajamalizwa kwako. Tunaambiwa hili limetokana na uongozi uliopita na hasa Mhe. Waziri aliyepita kwamba kapeleka wanafunzi mara mbili zaidi ya ile idadi iliyokusudiwa. Kwa hivyo ile bajeti imekuwa ndogo kupita kiasi, matokeo yake tumeshindwa kuwahudumia wanafunzi wale. Nilikuwa naomba hili kwanza nipatiwe maelezo.

Lakini hapo hapo Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nataka maelezo kwamba sisi Elimu ya Juu tulivyoambiwa ni suala la Muungano. Mwaka jana Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa Bungeni niliwahi kuulizwa swali kwa Naibu Waziri wa Elimu, wakati ule Mhe. Mwantumu Mahiza, kwamba katika *allocation* ya elimu ya juu kutoka serikali ya Muungano inayokwenda kwa Vyuo Vikuu. Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kinapata kiasi gani. Ilikuwa ni jukumu la Serikali ya Muungano kutujengea Chuo Kikuu, hawajatujengea tumeanzisha chetu wenyewe. Sasa ile bajeti iliyo juu inatupa kiasi gani sisi.

Mhe. Mwenyekiti, nikaambiwa hicho Chuo Kikuu cha SMZ kigharamiwa na SMZ, Serikali ya Muungano haihusiki nacho. Sasa nikajiuliza faida ya kuambiwa elimu ya juu ni ipi basi, kama sisi hatupati mgao wowote. Nilikuwa naomba Mhe. Waziri katika hili anisaidie kwamba hivi hatuna haki sisi katika ule mgao uliokuwepo kule.

Hapo hapo Mhe. Mwenyekiti, nimeona katika bajeti nimeona katika bajeti nataka kupongeza ni matarajio yangu kwa kuongezeka kwa bajeti hii ya Mfuko wa Elimu ya Juu basi labda hizi *crash* za wanafunzi wetu za kutafuta fedha zitapungua kwamba mwaka huu kumetengwa bilioni nne badala ya bilioni 2.5 za mwaka jana. Nilisema Mhe. Mwenyekiti nina nukta mbili katika elimu ya juu hilo la kwanza.

La pili niende katika Chuo Kikuu cha SUZA. Sitaki kuyarejea maelezo ambayo Mhe. Omar Ali Shehe keshayazungumza. Kusema kweli napongeza sana, sana, serikali kuja na uwamuzi wa kuanzisha Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Hii ni moja katika mambo ambayo Mhe. Rais Amani Abeid Karume atakumbukwa Zanzibar kwa kulisimamia mpaka akalifanikisha.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, Rais Karume alivyokuwa akizindua Chuo Kikuu cha Zanzibar alisema kwamba matarajio yake ni kwamba hichi kiwe *One of the best* katika Afrika ya Mashariki. Ndio maana alitaka malipo ya wahadhiri na vitu vyengine viwe vinalingana na *standard* ambazo zipo katika ukanda huu wa Afrika Mashariki.

Mhe. Mwenyekiti, inasikitisha tulipoanza wanavyotwambia wenyewe wetaalamu wa Chuo Kikuu, walikuwa bajeti yao walitengewa bilioni 20. Kwa hivyo, ilikuwa inaendana na lile lengo alilolisema Rais Karume wakati ule kwamba ituelekeze katika kufanya chuo chetu kiwe bora na kiwe kinatoa huduma nzuri. Lakini imeshuka mpaka leo kwa mwaka ruzuku yake imefika bilioni 3.6 . Kasema Mhe. Omar Ali Shehe kwamba walipeleka maombi yao bilioni 26 unapewa bilioni 3. Utafanya kazi vipi Mhe. Mwenyekiti, hapo.

Halafu haya yanatokezea kile kiwango cha kushuka kwa bajeti yake hakilingani na kiwango cha kuongezeka kwa huduma zinazotolewa. Kilipoanza Chuo Kikuu cha Zanzibar kilikuwa na wanafunzi 150 leo kina wanafunzi 1,000, kilipoanza kilikuwa na *campus* moja tu pale taasisi leo kina *campus* tatu, Taasisi, Beit el Ras na Tunguu. Sasa katika hali hiyo kweli bajeti hii waliyotengewa Mhe. Mwenyekiti, itatosheleza. Huku tukiambiwa kwamba elimu mwaka huu ni ya pili katika vipaumbele vya bajeti yetu. Nilikuwa naomba kupatiwa maelezo katika suala hilo.

Mhe. Mwenyekiti naliuliza kwa sababu kwa miaka kadhaa sasa inafika miaka mitano bajeti ya SUZA imekuwa ikiranda hapo hapo kwenye bilioni tatu, haipandi haishuki. Matokeo yake Chuo chetu kinaelekea kufa. Itakuwa jambo baya sana kama tumekianzisha kwa vishindo vikubwa halafu tukakiachia kikaporomoka. Kinaweza kikawepo lakini kikawepo jina tu. Kwanza mpaka leo Chuo Kikuu hakina Makamo Mkuu wa Chuo hajateuliwa na kwa hiyo huwezi ukapata uongozi unaohitajikana pale kuweza kutatua matatizo kama haya ambayo tunayataja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ya kukosa bajeti ya kutosha matokeo yake walimu kama wanavyosema malipo yao yamekuwa hayatoshelezi wanatukimbia. Mhe. Omar Ali Shehe kasema hapa mimi nawajua Mhe. Mwenyekiti alikuwepo Dk. Said Ali *Senior Lecturer* katika *Chemistry* kaondoka yupo *UDOM* sasa hivi. Alikuwepo Dk. Hamad alikuwa yupo kwenye *Evironmental Chemistry* sasa hivi na yeye yupo *UDOM* vile vile.

Huyu aliwahi kupelekwa Ujerumani na Japan kutoka Zanzibar. Tulikuwa tuna walimu wana viwango vya juu leo wanatukimbia. Alikuwepo Dk. Mkadam wa *biology* keshafariki lakini kabla ya kufariki alikwisha ondoka kwa sababu hivyo hivyo. Yupo Dk. Twalib kenda kusoma hakurudi tena. Sasa hivi wapo zaidi ya wanane wanafanya *PhD* lakini masuala wanayojiuliza *SUZA* watarudi hawa ikiwa utaratibu ndio huu. Nilikuwa nataka Mhe. Mwenyekiti, tulitizame kwa upana wake kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, kwamba matokeo ya kiwango kidogo badala ya kuajiri watu ni *academic* wa kusaidia Chuo tumeishia SUZA imekuwa kazi yake kuajiri ma-*secretary* tu watu wa utawala. Tumeambiwa kuna ma- *secretary* wengi sana pale kuliko hata yale mahitaji yake. Sasa nikuwa nadhani Waziri akiangalie kwa jichoa la rehma Chuo Kikuu ili yale malengo tuliyoyakusudiwa yaweze kufikiwa. Tunaambiwa walimu waliokuwepo pale wengi ni *part timers* na *part timers* kawaida hawana ufanisi kwa sababu ile *commitment* ya kusomesha pale inakuwa haipo kama yule mwalimu ambaye ameajiriwa kwa muda wote.

Mhe. Mwenyeki, naomba pia Waziri aiangalie maktaba, nilikwenda hivi karibuni kuipitia Maktaba Kuu, sio kabisa ile ninayoikumbuka wakati mimi niko *Secondary* ilipofunguliwa jumba ambalo leo ni Serena. Kuna upungufu, jengo ni zuri, fanisha zimo lakini vitabu kuna upungufu mkubwa sana. Nikitizama bajeti yake imetoka milioni 200 imeingia milioni 237 hakuna ongezeko kubwa. Lakini hapo hapo na mimi niombe maelezo katika kuvamiwa maeneo ya skuli na hasa katika Beit el Ras, kuna taarifa kwamba kuna mfanyabiashara pale anajenga *showroom* ya fanicha katika eneo la skuli. Hebu naomba Mhe. Waziri akija anipe maelezo tunaruhusu vipi maeneo yetu kuchukuliwa yakafanyiwa biashara.

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri mimi na yeye mwaka jana na wewe Mwenyekiti ulikuwepo, tulialikwa katika maulidi ya Shangani Taasisi pale. Mmoja katika watu wanaoheshimiwa sana katika nchi hii walimu wa zamani Maalim Idris wa Mambo Msiige, alitoa wito kwa Waziri akasema kuna hawa Mashekhe zetu wametoa mchango mkubwa sana katika Zanzibar basi hawa kila kitu kinapewa majina kwa majina tunao hapa wanasiasa tu hawa Mashekhe au watu wanaotoa mchango mkubwa katika sekta ya elimu ya dini ya dunia hawawezi kukumbukwa hata kwa skuli kupewa majina yao.

Akatoa mifano akasema kuna akina Sheikh Fatawi bin Issa, kuna Sheikh Shauri, kuna Sheikh Ameir Tajo, Hassan bin Ameir, Said Omar bin Subeit wapo wengi basi hawa katika kukumbukwa hatuwezi kufanya hivyo. Leo Comoro ina noti ambayo ina sura ya Said Omar bin Subeit kwa mchango wake. Huyu katokea Zanzibar, sisi hata kuwakumbuka kuwaenzi baadhi ya skuli kuzipa majina yao. Nimetoa mifano michache lakini wapo wengi Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo nilikuwa naomba nimkumbushe kama lile ombi la Maalim Idriss alilopewa pale na sisi tulikuwa mashahidi mimi na wewe Mhe. Mwenyekiti ajaribu kulifikiria.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, naiunga mkono hotuba hii mia kwa mia kwa mara ya kwanza. Lakini nategemea atanipa maelezo ya kutosha kwa zile hoja ambazo nimeziibua. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana ahsante.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nami kunipatia nafasi hiyo wakati wa Ijumaa ya leo. Awali ya yote sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu (SW) aliyetujaalia uhai, uzima, tukawepo hapa kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu. Baada ya kusema hayo pia nikushukuru tena na wewe kwa kuniona mchana huu kuweza kuchangia bajeti hii iliyomezani wakati huu.

Mhe. Mwenyekiti, sina budi nimpongeze Mhe. Waziri kwa jinsi alivyoiwasilisha hotuba yake hii jana jioni. Pia nimpongeze Naibu Waziri kwa utaratibu mzuri aliokuwa nao wa kujibu maswali hapa Barazani.

Pia nichukue nafasi hii kuwapongeza watendaji wote wa wizara hii. Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, sasa niseme Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni lazima ijielewe hichi ni kiwanda cha kutayarisha wataalamu katika nchi yetu kwa ajili ya maendeleo ya taifa letu kiuchumi. Hivyo basi lazima tufahamu kwamba Wizara hii ndio iliyopewa jukumu la kumtayarishia wataalamu.

Ieleweke kwamba taifa lolote duniani haliwezi kuendelea bila ya kuwa na wataalamu. Ni lazima na sisi tukumbuke kuwasomesha vijana watu ni jambo la msingi sana. aliliona hilo Mwenyezi Mungu (SW) katika Qur-ani yake amesema "**Hawawi sawa wale wanaojua na wasiojua"** Kwa vile sote ni waumini tunafahamu kwamba wale watakaofahamu basi watafanya mambo mazuri zaidi na wale wasiojua wataachwa nyuma kwani hawatakuwa na uelewa wa kutosha juu ya mambo ambayo watakiwa kuyatawala wao katika ulimwengu huu.

Hivyo basi niiambie serikali kwamba sasa umefika wakati wa kuwekeza katika elimu. Baadsa ya maneno yangu hayo nasema kwamba bajeti hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ni ndogo haikidhi haja kutokana na wakati tulionao.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo sasa niende katika mchango wangu katika ukurasa wa 24(44) Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Hapa nianze kusema mithali moja, **"Usimuudhi mchinja mbuzi utakosa mchuzi"** Naisema mithali hiyo nikiwa na maana ya kwamba walimu ndio tegemeo la taifa hili. Walimu hutolewa mara nyingi kwenda kusimamia mitihani bila ya kulipwa fedha zao.

Hiki ni kilio na haya ni malalamiko. Hawa ndio wachinja mbuzi. Endapo tutaendelea na utaratibu huu wizara kufanya walimu hawa wende wakasimamie bila ya kujielewa kupata malipo yao. Malipo yenyewe ni madogo mno,

hayakidhi haja, lakini hata na udogo wake pia hawawezi kupatiwa kwa wakati muwafaka. Hivi tujiulize ni nani anayetaka kufanya kazi bila ya kupata malipo? Mhe. Waziri ni juu yako kuliona suala hili la walimu la kuwapatia malipo yao mara tu baada wamalizapo kusimamia mitihani.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 52, ukurasa wa 26 Idara ya Elimu ya Maandalizi. Nimwambie Mhe. Waziri maandalizi hapa ndipo penye mambo makubwa na utaratibu mzima wa kumuandaa kijana ili aweze kuelekea kwenye msingi hatimaye sekondari na Chuo Kikuu na hatimae kuibua wataalamu ambao wataliongoza taifa hili kwa ajili ya maendeleo. Kwama hivyo ndivyo na tunaamini hayo ningeomba kumwambia Mhe. Waziri hii ni sehemu muhimu sana, ni sehemu ya kuangaliwa na kuzingatiwa kwa kina kabisa. Wizara ipange mpango madhubuti wa kuwasomesha walimu wa maandalizi hasa, ili wajielewe ni ni wanachokifanya. Waelewe wao ndio watakaokua wajenzi na waandalizi na hilo tatifa tunalolihitaji.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niende ukurasa wa 27 kifungu Nam. 53. Idara ya Madrasa na Vyuo vya Qur-an. Hapa waheshimiwa wengi wamesimama lakini sikuwahi kuwasikia kulizungumzia. Mimi hapa ningependa kuzungumza kidogo. ningeiomba wizara ifahamu kwamba kutoa taaluma ya elimu ni majukumu yake, iwe elimu ya dunia iwe ya akhera, tunawakabidhi wao Wizara ya Elimu katika taifa letu. Hivyo aelewe kwamba maandalizi ya mwanzo ya mtoto anapotaka kufundishwa kusema huanza kupelekwa chuoni. Hiyo ndio suna ya Mtume Muhammad (SAW) ambayo sisi sote ndiyo tunayoifuata. Kama hivyo ndivyo tunakuomba Mheshimiwa ufanye juhudi na utaratibu maalum utawafanya kuwapatia hawa walimu pamoja na walimu wapate misahafu, juzuu, iwe ni moja katika utaratibu wako. Kwa kushirikiana na taasisi mbali mbali za kiislamu ili uweze kuwaona walimu hao.

Pia niiombe wizara ifanye juhudi za makusudi au kwa kupitia wafadhili ama matajiri ili walimu hawa na wao angalau wapate sabuni. Hili neno la mwalimu hapa kwetu limekuwa linataja lakini thamani ya mwalimu haijulikani katika pange zote mbili, sio mwalimu wa shuleni, sio mwalimu wa madrasa. Tumewasahau sana katika taifa letu, kwamba huu ndio msingi wa kuweza kuzaa mambo mengi ya maendeleo katika taifa letu. Kupata kheri za dunia na za kesho Kiyama.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 43, kifungu cha 102. Mhe. Mwenyekiti, hapa naizungumzia mamlaka ya mafunzo ya amali. Mamlaka hii ina jukumu la kuona ina unga mkono juhudi za serikali kwa ajili ya kujikwamua vijana wetu katika shughuli za kiuchumi, kuwafunza na kuwapa taalauma na kuona yale

mafunzo wanayoyapata yanaweza kutumiwa vizuri. Au lile lengo la serikali jinsi linavyowapanga vijana hawa kuwapatia hilo na wao wawe wanaliona hilo. Mhe. Mwenyekiti, hapa nina taarifa ya kunisikitisha kidogo, ni kwamba Chuo cha Mafunzo ya Amali Mkokotoni kuna vyumba viwili vimeungua kwa moto kwa sababu za makusudi. Vyumba hivyo vimeunguzwa na vimeteketeza kila kitu. Hili ni jambo la kusikitisha sana kwani nia ya serikali ni kuwaendeleza vijana wake na kuweza kuwakwamua kiuchumi ili waweze kujitegemea. Taifa lina shida kubwa ya ajira kwa ajili ya vijana wake. Hii ni sehemu moja chemchem ya kuzaa vijana watakaoweza kujiajiri wenyewe. Je, wizara inalifahamu hilo? Kama inalifahamu imechukua hatua gani? Tunaomba Mhe. Waziri utakapokuja hapa basi unipatie jibu ili niweze kuelewa.

Baada ya kusema hayo kwa vile mimi nilikuwa ni mmoja kati ya Wajumbe wa Kamati hii nisengekuwa na mengi isipokuwa naunga mkono hoja kwa asilimia mia. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mheshimiwa Mjumbe, lakini naona muda ni mtihani kidogo. Waheshimiwa wajumbe naomba wajumbe waliobakia wataendelea kuchangia wakati wa jioni. Ukitilia maanani kwamba mjadala huu utendelea hadi Jumatatu. Kwa hiyo tutafanya hivyo jioni *Ishaallah*. Lakini tusome matangazo mawili matatu ambayo tunayo hapa.

Hapa kuna tangazo la kuwaombe waheshimiwa wawakilishi wote kesho mechi yetu ya Mabenki itakuwa katika uwanja wa Mau, saa 9 za jioni. Waheshimiwa wote wanaombwa waondokee hapa, saa 8:00 za mchana. Mgeni rasmi katika mechi yetu hiyo ya kesho atakuwa Mhe. Mgeni Hassan Juma ambaye ni Mwenyekiti wetu.

Sasa tutangaze orodha ya wachezaji wenyewe hiyo siku ya kesho.

Namba ya Mchezaji	**Majina ya Wachezaji**	**Majina ya Marizavu**
1	Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Mhe. Machano Othman
2	Saidi	
3	Mhe. Juma Duni Haji	Mhe. Asaa Othman
4	Hamadi	
5	Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Mhe. Hijja Hassanj Hijja
6	Mhe. Abdilahi Jihadi Hassan	Mhe. Ali Salum Haji
7	Mhe. Haji Omar Kheir	Mhe. Mohammed Said
8	Mohammed	
9	Mhe. Omar Yussuf Mzee	Mhe. Saleh Nassor Juma
10	Mhe. Suleiman Othman Nyanga	Mhe. Subeit Khamis

11 12	Faki. Mhe. Nassor Ali Jazira Mhe. Ismail Jussa Ladhu Mhe. Hamza Hassan Juma Mhe. Salmin Awadh Salmin Mhe. Ali Mzee Ali
	Madaktari **Mchuaji wa Misuli**
	Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya Mhe. Asha Abdi

Baada ya maelekezo hayo Waheshimiwa Wajumbe kwa heshma na taadhima naomba kuakhirisha kikao hichi hadi jioni saa 11:00. Ahsanteni sana.

(Saa 11:15 mchana Baraza lilikhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

Makadiri ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012 – Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kama kawaida yetu katika vikao vyetu vya bajeti huwa tuna kawaida ya kupata wageni kwa hiyo leo tuna mgeni wetu ambaye anatokea University of New Cassteller Australia anaitwa Professor Jimm Joes, karibu sana Professor. Wageni wetu wengine ni Emmest Vein Swai ambaye anatoka Fedrick Nowman Foundation huyu ni mgeni wa Naibu Waziri wa Elimu. Karibu sana bwana Swai.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa jioni hii kupata nafasi kuwa mchangiaji wa mwanzo wa bajeti hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwanza nichukue fursa yakumshukuru Mwenyezi Mungu kwa jioni hii kukutana hapa katika shughuli zetu za kawaida za Baraza. Pili, nimshukuru Mhe. Waziri wa Elimu kwa maandalizi yake mazuri ya kitabu chake hiki cha bajeti ya wizara yake. Niseme kwamba mawaziri wetu wote ni watu wazuri, wenye lugha nzuri ya Kiswahili na waliojiandaa vizuri katika maandalizi yao. Kwa hivyo, niwaambie kwa pamoja wote wale ambao wameshatangulia kwamba ahsanteni sana kwa maandalizi yenu mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze kama alivyoanza mwenyewe Mhe. Waziri kwa kutoa shukurani katika utangulizi wake. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu pamoja na yeye pia niishukuru kama alivyosema yeye hatua zilizochukulia mpaka leo ikawa tuko katika Baraza hili katika hali ya umoja baina ya Wajumbe wa Vyama viwili tofauti tuliomo humu ndani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianze programu ya usomaji elimu ya msingi, hapa nitakwenda kwenye sehemu ya majengo kwanza. Mhe. Mwenyekiti, kitabu hiki kimeonesha kuwa hivi sasa yako madarasa kama 280 ambayo yamefika hatua yakuezekwa, hii ina maana wananchi wamejenga kufikia hatua hiyo na hatua iliyobakia yakumalizia ni ya wizara wenyewe. Kwa hivyo, madarasa 280 sio kidogo ni mengi na yanahitaji pesa nyingi kuweza kuyaezeka haya yote pengine katika bajeti hii. Lakini kwa sababu wameyataja nadhani itakuwa wana uwezo wakuyaezeka haya yote.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kama kutakuwa kuna upungufu wa uwezekaji mimi binafsi ningeomba katika jimbo langu angalau waniezekee na mimi kidogo. Kwa sababu pale Skuli ya Kengeja na hasa kwa sababu ipo ahadi ya Mhe. Waziri liko banda la msingi kule lenye madara 7 ambayo Mhe. Rais wa awamu ya sita aliyepita alikuja kulizindua na katika uzinduzi huo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali iliahidi kuyaezeka mabanda yale. Lakini mpaka tunakuja katika kikao hiki bado hayajaezekwa kwa hiyo mimi nawakumbusha wizara hii kuwa katika bajeti hii mabanda yale wayaone na yaezekwe.

Mhe. Mwenyekiti, sio yale ya msingi tu pia na sekondari liko banda moja lenye vyumba vinne, kikiwemo chumba cha maabara nalo pia Wizara ya Elimu ilichukua ahadi yakuliezeka tokea mwaka 2010. Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati mbaya bado halijaezekwa, hivyo ningeomba mabanda yale yaezekwe.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kumetajwa baadhi ya skuli zilizofanyiwa ukarabati ambayo kwa jumla ni skuli tisa. Lakini katika mdororo ule wa skuli tisa nimeiona skuli ya Pemba ni moja tu nayo ni ya Skuli ya Ng'ombeni. Kwa hivyo, katika mwaka huo uliopita katika skuli ambazo zimefanyiwa matengenezo makubwa Pemba ilifanyiwa matengenezo Skuli moja tu nayo ni Skuli ya Ng'ombeni. Mhe. Mwenyekiti, lakini Pemba ziko skuli kadhaa ambazo ni mbovu na zinahitaji matengenezo. Kwa hivyo, katika bajeti hii ningeomba vile vile skuli za Pemba Mhe. Mwenyekiti, ambazo ni mbovu kuliko skuli zote za Unguja na Pemba ni Skuli ya Kengeja.

Mhe. Mwenyekiti, skuli hii ni miongoni mwa skuli kongwe za Pemba, ilianzishwa mwaka 1926. Lakini leo baadhi ya mabanda yake ukipita kwa kweli hudhanii kuwa hii ni skuli, unaweza ukadhania kuwa ni mabanda

yanayofugiwa mifugo tu kama kuku au mbuzi. Kwa kweli kwa wakati huu yale mabanda yamepoteza hadhi yakuwa ni mabanda yakufundishia watoto wa nchi iliyo huru kama yetu. Mhe. Mwenyekiti, katika ziara ya Mhe. Rais Mstaafu mabanda yale Wizara ya Elimu ilipoyaona ikaahidi mawili waliahidi kuyavunja na kuyajenga upya hasa, na mengine wameahidi kuyaezeka lakini yote kazi hiyo haijafanyika. Kwa hivyo, mimi naikumbusha Wizara ya Elimu hilo suala kuwa liko.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ni kwamba hapa kumetajwa mafunzo mbali mbali kwa walimu ikiwemo ya lugha ya Kiengereza. Mhe. Mwenyekiti, hii lugha ya Kiengereza ndio lugha ambayo tumeifanya kuwa ndio *medium* ya *instruction* zetu, lakini ndio lugha ambayo hatuielewi. Nadhani ukiacha Kiswahili wenyewe na masomo ya Dini wanafunzi walipofanya mitihani lugha inayotumika katika mitihani ni lugha ya Kiingereza, lakini pia ndio lugha ambayo hatuielewi vizuri. Kwa hivyo, naiomba Wizara ya Elimu kwamba ilivyosema kuwa inatoa mafunzo kwa walimu, kwa kweli isimalizie kwa walimu tu ikiwezekana hata vipindi vya Kiengereza viongenzwe katika maskuli zaidi madara ya juu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu unaweza ukamkutia mwalimu anasomesha *Chemistry* na *Physics* lakini lugha anayotumia asilimia 80 anatumia Kiswahili zaidi kuliko ile lugha ambayo katakiwa afundishe somo lile. Mhe. Mwenyekiti, lugha ya Kiengereza anaipenyeza mara chache sana ambayo haitakiwi hata neno moja la Kiswahili litumike katika kufundisha masomo yale. Lakini kwa sababu hii lugha hatuielewi basi mafundishaji yetu yote yanaangukia kufundisha katika lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, iko haja ya wizara hii kuliendeleza somo hili la Kiengereza kwa sababu mpaka sasa ndio lilowekwa kuwa ndio lugha ya kufundishia katika maskuli yetu.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na ujenzi mwingi tunaofanya lakini bado katika maskuli yetu kuna matatizo ya vikalio. Watoto unajua wengi katika maskuli mengi bado wanaendelea kukaa chini, na pengine baadae hawa wakapata ugonjwa wa mgongo kwa sababu wakati wote huwa wameinama tu wanapoandika. Mhe. Mwenyekiti, wengi waliozoea hivyo hata ukimpa kikalio kama meza basi kwa sababu hana mazoea yakuandika juu atakwenda kukaa chini akaandika kwani ndivyo alivyozoea.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri hapa umetaja msururu wa meza, viti na madawati lakini bado skuli zilizo nyingi yana upungufu tena mkubwa wa vikalio. Kwa hivyo, ningeomba katika mwaka huu wa fedha pamoja na mengi wizara hii waliyonayo na hili liangaliwe kwa upana mno.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika Idara ya Maandalizi na Msingi, hapa kumetajwa vyuo vya kur-ani ambavyo ni vingi tu zaidi ya 2000 na vikiwa na waliku zaidi ya 8000. Kwa hivyo, ningeiomba wizara pamoja na mafunzo mbali mbali wanayowapatia lakini pia vyuo hivi na madrasa hizi za kur-ani zipatiwe misaada zaidi kama vijuzuu vya kusomea pamoja na misahafu na walimu kupata taaluma ya ualimu ili waendane na mfumo wa sasa wa kufundishia.

Mhe. Mwenyekiti, katika madarasa ya msingi darasa la kwanza hadi la saba zaidi la kwanza masomo yanayofundishwa ni mengi mno, darasa la kwanza yako masomo zaidi ya manane haya ni mengi mno kwa watoto wadogo. Mhe. Mwenyekiti, mimi zamani nimesoma kidogo lakini masomo manane haya niliyakutia nilipofika darasa la saba, leo yako manane darasa ya kwanza. Mhe. Mwenyekiti, mimi sisemi kama ni maendeleo kwa sababu tunampa *information* mwanafunzi mdogo ambaye bado uwezo wake haujakuwa mkubwa.

Mhe. Mwenyekiti, mbali ya hilo ule msongamano mkubwa wa wanafunzi katika darasa moja pia nao unachangia kudhorota kwa elimu. Mimi niliona kitabu wakati fulani kinachoitwa *Teacher in the making* kinachoonesha wastani wa wanafunzi wadogo wanaostahiki kuwa katika darasa moja. Darasa la kwanza kwa kipindi hicho liwe baina ya watoto 15 hadi 20, na wakati wa kuwafundisha usizidi dakika 15.

Mhe. Mwenyekiti, hiyo tuiache kwani imeshapitwa na wakati, lakini leo darasa la kwanza lina watoto zaidi ya 80. Mhe. Mwenyekiti, mwalimu ana uwezo gani wa kuweza kumpitia mtoto mmoja mmoja kumuelekeza kuandika mpaka afahamu kwa kipindi kimoja. Kwa hivyo, baadhi ya watoto wanaoanza darasa la kwanza na darasa la tatu pengine hata kuandika jina lao bado hawajaelewa kutokana na msongamano mkubwa madarasani.

Kwa hivyo, hatimae tunapata watoto waliomaliza madarasa, lakini ile elimu ambayo inahitajiwa waipate kwa kweli hawakuifikia. Kwa hivyo, tunapata watoto waliomaliza darasa la kumi lakini standard ya *form two* huwa bado haijafikiwa. Kwa hivyo, tuna idadi ya wamalizaji wa *form two*, lakini tuna idadi ndogo sana ya watoto kwenye elimu hasa ya form two, pia na *form three* na *form four* nao ndio hivyo hivyo. Mhe. Mwenyekiti, ndio maana vijana wetu wengi wenyewe tunajisifu mara nyengine kuwa tumepasisha wengi lakini wote ni *grade three* na *grade four*.

Mhe. Mwenyekiti, cheti wamepata kweli lakini uwezo wa kuendelea ni mdogo kwa hiyo ili kuondokana na kadhia hii ni kwamba haya madarasa ambayo bado yamefikia hatua ya kumalizwa wizara ijipinde iyamalize ili kujaribu kupunguza huu msongamano katika madarasa.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba mwalimu ni kigezo kwa mwanafunzi na wanafunzi walio wengi mara nyingi wanaiga vile mwalimu alivyo. Kuna kitu katika walimu tulikuwa tunaita *similariesm* kama una tabia fulani unayoifanya katika darasa basi kwenye kusomesha kwako basi wanafunzi wanaiga ile tabia ile kama ni ya kusema, kama ni ya kwenda wanaiga mambo kama hayo wanafunzi. Kwa hivyo, mwalimu awe ni mfano kwa wanafunzi wake na awe ni kigezo kwa tabia, desturi, silka, mila, utamaduni na hata mavazi. Mhe. Mwenyekiti, mwalimu akifanya vizuri katika hayo basi ataweza kumuelekeza na mwanafunzi wake.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hivi sasa tuna matatizo kidogo katika mavazi maskulini, walimu wa kike walio wengi siku hizi usomaji wa dini umekuwa sana. Walimu wanapokwenda madarasani siku hizi wanavaa mashungi yao ambayo nadhani ni katika sehemu ya kujistiri wao wenyewe. Lakini inatokezea baadhi ya wakati vazi lile pengine kiwizara halikubaliki, lakini kwa kuwa yapo malalamiko kuwa hili linatokezea na katika Wilaya ya Mkoani iko skuli moja juzi tarehe 8 kuna walimu wawili wakike walirejeshwa na kwamba kwa siku ile hawana kazi kwa sababu walikuwa wamevaa hilo vazi la shungi. Kwa hivyo, kama hana kazi siku ile ina maana siku ile asilipwe, kama asilipwe itabidi apewe barua rasmi kuwa umekatwa siku, na kama atalipwa itakuwa mwalimu yule kaidhulumu serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kumkata mshahara wake juu ya meza haiwezekani, lazima akatwe kisheria. Lakini je, kuna formula gani ya mavazi iliyokubalika katika nchi mpaka ikawa vazi fulani vaeni na vazi fulani halifai. Ningeiomba Wizara ya Elimu kwa sababu ndio yenye malezi zaidi itueleze ni vazi gani rasmi linalokubalika kwa walimu zaidi wa kike ili kuondoa huu msongamano wa matatizo ya mara kwa mara, tukijua kwamba siku hizi wanawake wanasoma sana.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka kwenye mavazi ni kuwa wizara imezungumza hapa kwamba itapeleka mafunzo ya kompyuta na internet katika maskuli yetu yote ya Unguja na Pemba. Mhe. Mwenyekiti, ni wazo zuri na naomba iwe hivyo lakini bado yako baadhi ya maskuli umeme haujafika hadi leo. Kwa hivyo, hili nalo ni haki yao waipate kwa hivyo wizara ifikirie yale maskuli ambayo hayajakuwa na umeme nayo yapatiwe huduma hii ya umeme ili huduma ya internet ikifika na wao iwafikie.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nije katika huduma za dakhalia. Mhe. Mwenyekiti, hizi kwa kweli kwa sasa ukiacha lile jengo wanafunzi waliopewa kulala hakuna jengine linalopatikana. Kuhusu chakula wanafunzi wanajitegemea wenyewe kupitia kwa wazazi wao na watu wengine mbali mbali. Kwa kweli umekuwa

mzigo mkubwa kwa sisi wazazi pale mtoto wetu anapofaulu, imekuwa ni mtihani kwetu mtoto akifeli ni mtihani, akifauliu pia ni mtihani kwa sababu mzee hulazimika kutafuta mbanjo. Mhe. Mwenyekiti, mtoto huwa anatafute godoro, ndoo ya maji maana yake kila kitu.

Kwa hivyo, kwa hili tumerudi nyuma kwa sababu mimi nilikuwa mwanafunzi wakati fulani, na nilipoingia dakhalia hakuna chochote nilichotakiwa nitoe mimi isipokuwa nilioneshwa kuwa kitanda chako utakacholala ni hiki hapa. Mhe. Mwenyekiti, sijaambiwa nichangie chakula, sikuchangia malazi wala sikuchangia chochote. Kwa hivyo, kwa hili serikali imerudi nyuma, kuna msemo wa Kiswahili unaosema kwamba "mtu anashona koti kulingana na kitambaa chake". Sisi kitambaa chetu ni kidogo lakini tunataka tushone koti hiki kitambaa na hakitoshi, ndio maana baadhi ya huduma sasa hivi tunazirudisha kwa wazazi wenyewe. Kwa vyovyote tutakavyoita sasa hivi elimu imebadilika ikiwa ni kuchangia, ni kulipia vyovyote kama unachangia unatoa pesa. Kwa hivyo, vyovyote ni kuwa bado elimu sasa tunalipia.

Mhe. Mwenyekiti, hata chaki sasa hivi ni kwamba maskuli yajitegemee, hata daftari la mahudhurio inabidi maskuli yajitegemee, kwa kweli wizara hii hapa zaidi ya kuezekwa mabanda na kuwalipa wafanyakazi mishahara hawana jengine hivi sasa wanalochangia. Kwa hivyo, sehemu kubwa ya elimu imeturudia sisi wenyewe wazazi.

Mhe. Mwenyekiti, zamani kila mwisho wa tamu ikiwa tunafanya mitihani na kutoa matokeo, mimi katika mizunguko yangu hapa nilipokwenda nimezungumza na wanafunzi namuuliza darasa la ngapi wewe, ananambia la tano au la sita, namuuliza umetokea wa ngapi Unguja na Pemba jibu lao wanajibu hatujaitwa matokeo mpaka sasa, yaani ni kuwa hawajapewa matokeo. Je, Mhe. Waziri siku hizi hakuna yale mitihani ile ya kila tamu?

Mhe. Mwenyekiti, nilikwenda Mkokotoni kwenye ziara zetu kuna watoto pale nimezungumza nao nikauliza zaidi ya watoto watatu madara mbali mbali kila mtoto ananiambia babu hatujaitwa. Mhe. Mwenyekiti, hii kuitwa imekuwa maarufu Unguja na Pemba. Hii inaonesha pengine siku hizi hii *terminal examination* hazipo tena, na kama zipo kwa nini wanafunzi huwa hawapati matokeo. Nadhani kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, huu ukaguzi kwa kima fulani umepungua sana au takriban haupo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu ikiwa haupo na kwa kuwa wanafunzi ni wengi pengine walimu baadhi ya mambo huwa wanayaacha njiani. Mhe. Mwenyekiti, nadhani dakika zinakaribia kumalizika niseme kuwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali mna kazi kubwa na ngumu na walimu wana kazi hiyo

kubwa na ngumu zaidi kwa sababu wao ndio walioko huko shambani wanakofanya kazi. Kwa hivyo, ningewaombea walimu yale yote ambayo yanawajibika wapate kwa kweli musiwahini, walimu wanapokwenda likizo wanakwenda kwa kupangiziwa kwa mwaka huu baada ya miaka mitatu ndio upate chochote. Mhe. Mwenyekiti, hakuna likizo yakupewa mtu shilingi 50,000 tu. Kwa hivyo, mimi naunga mkono hoja hii, ahsante sana.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, pili nimshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote wa wizara hii, wizara mama. Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kusema kwamba mfumo wa elimu Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii, pili nimshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote wa wizara hii, wizara mama.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kusema kwamba mfumo wa elimu wa Zanzibar na Bara una tofauti, kwa Unguja kuanzia darasa la kwanza mpaka la kumi na mbili tunatumia Sera ya Elimu ya Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, tunapofanya mitihani ya taifa huyu wa Zanzibar serikali inamuwezesha vipi ku-*compete* na huyu wa Bara.

Pia Mhe. Mwenyekiti nimuuulize Mhe. Waziri elimu ya kidato cha nne iko kwenye Muungano? Kama iko kwenye muungano vipi Wizara ya Elimu Zanzibar inashiriki katika maandalizi ya mitihani na matokeo yake. Kama elimu hii iko katika Muungano kuna haja ya kuwepo na kituo Zanzibar kuepuka usumbufu na kasoro zinazojitokeza kama kukosekana kwa nambari za mitihani, baadhi ya wakati matokeo yamekuja sio yako na vile vile *format* ya mitihani ya Bara inachelewa sana kufika hapa kwetu. Ingesaidia sana kuwepo kwa tawi hapa kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikutoa ujumbe huu kwenu ambao juzi tu niliitwa kuwa Mgeni Rasmi katika kituo kimoja cha *American Corner,* kituo ambacho kinafadhiliwa na Mmarekani chini ya Chuo Kikuu cha Taifa, (*SUZA*). Lengo la kutoa habari sahihi kuhusu Marekani, sera za Marekani, mila na masuala mazima ya elimu kwa nia ya kuisaidia Zanzibar na Tanzania.

Mhe. Mwenyekiti, iko haja ya makusudi ya kuunganisha elimu, kituo hiki kinaunganisha elimu na taasisi mbali mbali za maendeleo kwa nia ya kusaidia kusambaza elimu. Kituo hiki kwa kushirikiana na *NGOs* tofauti kimeshaandaa *program* za elimu ya UKIMWI, Madawa ya Kulevya, Mtoto wa Afrika, Siku ya Wanawake na kadhalika. Ningewaomba wananchi na hasa vijana kutumia

huduma za *internet* kujisomea vitabu, kuangalia *CD* na *DVD* zinazoonesha maisha ya Marekani na njia waliyotumia ya kuendeleza elimu.

Mhe. Mwenyekiti, kituo hiki ni muhimu, mwezi uliopita kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, Idara ya Bajeti waliandaa *public lecture* kuhusu maandalizi ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na changamoto zake, watu walielimika kupitia njia hii. Kituo hiki kimeanzisha *American Corner English Club* ni jukumu letu kuhamasisha vijana wetu kujiunga na kituo hiki ambacho kinatoa mafunzo mbali mbali na uanachama ni bure.

Pia Mhe. Mwenyekiti, ni wakati muafaka kwa Baraza la Wawakilishi kutumia kituo hiki katika kuelimisha masuala ya uendeshaji wa kituo kwa shughuli za Baraza ili *American Corner* ichukue elimu hiyo na kusambaza kwa wananchi wa kawaida. Mhe. Mwenyekiti, ipo haja ya kujisaidia moja kwa moja ili navyo viongeze viwango vya elimu Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kituo cha sheria ambacho amekianzisha Prof. Haroub ambaye sasa ni Marehemu Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema, naiomba wizara ielewe na ifuatilie mambo yanayoendelea katika vituo hivi ni mazuri na makubwa kwa maendeleo ya taifa letu. Ningemshauri Mhe. Waziri kupitia Idara ya Sera, Mipango na Utafiti ikifanya utafiti zile program zinazoendelea ili ziendelezwe na kuvifanya vituo hivi view endelevu.

Kuhusu maktaba wizara ingechukua jitihada za makusudi kuanzisha maktaba za wilaya ili huduma hii isogee karibu kwa wale wenye kuhitaji huduma hii, tukielewa nayo ina mchango mkubwa kielimu kwa kujisomea vitabu pia kuweka teknolojia ya kompyuta ili watu waweze kujifunza mengi kupitia maktaba.

Mhe. Mwenyekiti, nije kuhusu msaada wa vitabu kutoka Marekani, wizara inawawezesha vipi walimu ili kuvifundishia vinavyotakiwa. Kupitia hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2011/2012 niseme kwamba imeeleza mengi na mengi ni ya kupigiwa mfano.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia kwenye michezo kweli ni ajira na michezo inakuza akili. Kwa hivyo, pia niipongeze wizara hii kwa kuwashirikisha watoto kwenye michezo, kwani michezo inakuza akili kama nilivyosema.

Pia ningeiomba wizara hii iwe inafanya mashindano na *valuation* pale tunapofanya vizuri kitaifa na tunapofanya vibaya basi tutafute ni sababu gain ambayo imesababisha kufanya vibaya.

Mhe. Mwenyekiti, sitaki nichukue muda wako mwingi nasema bajeti ya wizara hii wizara yangu mama, kufika kwangu hapa katika safari yangu nilitokea pale kwa hivyo naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu (*SW*) mwenye kutuwezesha mchana huu tukaweza kurejea tena katika Baraza lako hili tukufu na kuweza kuchangia kidogo angalau yale yaliyomo.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza kwanza Mhe. Waziri na watendaji wake wote, manaibu waziri, makatibu wakuu mpaka wakurugenzi kwa kazi nzuri waliyoifanya. Mhe. Mwenyekiti, penye nia pana njia, mimi nitazungumza kidogo tu sitaki niharibu wenzangu waliyokwishayazungumza sana nije katika Elimu Mjumuisho.

Mhe. Mwenyekiti, elimu mjumuisho kwa vile elimu ndio uti wa mgongo wa binadamu na watu wote tulioko huku ulimwenguni tunataraji elimu ikiwa ya dunia au ya akhera. Elimu mjumuisho tulipoipata tulikaa hapo kitako ili kuitathmini na hapo tuliona tutaondokewa na mzigo mkuwa wa kusomesha watoto wetu. Watoto hawa wa elimu mjumuisho ni makundi ya aina mbali mbali ambayo kuwa ni walemavu wa aina mbali mbali.

Katika elimu hii kuna wenzetu ambao ni walemavu hawa ndio waliokuwa na tatizo kubwa sana la kuweza kupata elimu na wakawa hawafahamiki. Kwa sababu hapa pana wenzetu wa *ZPDD* ambao ni watoto wenye ulemavu wa akili, hawa Mhe. Mwenyekiti, ni watoto wagumu sana kufundishwa, sasa tunalolisikitikia katika serikali ni kuwa hatuna walimu wanaoweza kuwafundisha watoto hawa, kwa sababu watoto hawa elimu mjumuisho mpaka wapatikane walimu maalum na wenzetu hawa waliokuwa hawaoni nao vile vile wana mashine maalum za kusomea za nukta nundu.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, tukitembea katika skuli nyingi nilimotembelea naweza kukuta skuli mbili tatu nikakuta moja tu ndio yenye kifaa hicho. Lakini ukiuliza unaambiwa mwalimu hapana wa kutumia kifaa kile ina maana inazidi kurudisha nyuma kwa wanafunzi hawa wenye ulemavu.

Watu wenye ulemavu wa viungo Mhe. Mwenyekiti, hawa ni watu ambao wana akili zao isipokuwa wana mabadiliko tu ya viungo, lakini wanafahamu kinachoelezwa pale lakini wenzetu hawa mpaka tupate ile elimu ya ishara, wale wenzetu wengine kama hawajapata lugha ya ishara bado wao hawawezi kufahamu chochote. Walimu wana usumbufu mkubwa kwa watoto hawa katika skuli.

Juzi nilipouliza swali la nyongeza Mhe. Naibu Waziri alinambia skuli ya watoto hawa iko Michakaeni. Nakubali kuwa iko Michakaeni nimeshatembelea mara mbili, nimeshakwenda semina mara mbili, lakini Mheshimiwa sasa tutizame watoto hawa mikoa miwili tuliyonayo Pemba kila mkoa watoto walemavu wapo, kila wilaya watoto walemavu wapo, mama mzazi au baba mzazi ataweza vipi kuweza kuwachukua na kuna familia nyengine Mwenyezi Mungu atusamehe ni mwenyewe kadri zake, kuna watoto ambao familia moja ni wawili au watatu na wana maradhi haya ya akili, tumeshakwenda majumbani kuhamasisha, tumeshakwenda kuwaona, bado watoto hawa elimu haijawafikia hawezi mama mzazi yule kuchukua watoto wale kituo ni kimoja tu kiliopo Michakaeni tukasema tunataka tuwapeleke. Ikiwa tuna uwezo wa kuwapeleka basi pale mabanda yale mawili yangelijaa na watoto wasingepata pakukaa, lakini watu hawawezi kupeleka watoto kule, watu ni dhaifu ukiwa na mtoto mlemavu uwe una gari ya kumpeleka na kumrudisha au mtu, huwezi tu yule kumtia kwenye gari ukamwambia ende Michakaeni.

Sasa tulipokuja kupata elimu mjumuisho hapa tukaona ndio tumeshaondoa tatizo letu, skuli zinafurika watoto kupelekwa tunapita kuhamasisha na watoto tayari wanapelekwa skuli, lakini bado elimu mjumuisho haijakidhi haja juu ya wenzetu hawa. Tunamuomba Mhe. Waziri kwenye kitabu chake tumeona humu walimu aliyosema watafundishwa masomo haya kuanzia ndani na nje tuweze kupata walimu katika skuli juu ya kuweza kuwakwamua wenzetu hawa na wao kupata elimu yao.

Halafu Mhe,. Mwenyekiti, niendelee hapo hapo katika skuli. Jamani skuli ni masomo ya kila mmoja na kusoma ni uti wa mgongo lakini kabisa wenzetu walimu wana matatizo ya hali ya juu. Skuli nilizozitembelea nimeshawahi kuitwa kwenye kamati za wazee na skuli kuna matatizo ya watoto wa skuli kuwa hawawezi kuheshimu walimu wao. Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema moto aliyekuwa yuko darasa la kumi na kuendelea huyu si motto, sasa hapa hawa wanatumia tulipokuja kuweka kigezo ya sheria ya motto wanawaadhibu walimu. Mh. Mwenyekiti, watoto hawa wakitoka madarasani hawarejei tena, mabuku hawapeleki kusahihishiwa na hata kupiga wale walimu wao. Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Waziri haya uwe nayo kwa makini tusilaumu walimu hawasomeshi watoto wetu kumbe wana matatizo.

Halafu katika skuli yangu ya Ole tuna banda pale nguvu za wananchi limejengwa nafikiri kama miaka miwili kupita, bado banda lile mpaka sasa hivi Wizara ya Elimu haijatuona kutuezekea tukaondoa msongamano wa watoto wale banda liko vile vile na nguvu za wananchi nyingi zimekwenda kwa pesa walizotoa. Namuomba Mhe. Waziri atuone kwa jicho la huruma skuli ile iezekwe na wakabidhiwe walimu.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, hatuna vifaa vya sayansi hasa *lab*, watoto kuweza kujifundisha kwa vitendo na tunakabiliwa na mtihani mwaka huu watoto wa sayansi lakini hakuna vifaa. Hivyo tunamuomba Mhe. Waziri aweze kufanya jitihada zake tuweze kupata vifaa vya sayansi watoto kuwez kujifundishia skuli.

Mimi nasema walimu wana mzigo mzito, mwalimu anaweza kuwa anakaa mjini lakini anapangiwa kuja kusomesha skuli ya Ole na anatakiwa afike mapema skuli hana kipando wala chochote, Mheshimiwa huu ni mtihani mkubwa sana wa walimu. Tumeshapita katika skuli na wenzetu wanatulilia sana katika kadhia hii. Lakini tunaomba tu, zile nauli wanazopewa waongezewe kwa sababu mtu kumtoa mbali na kusomesha mtu anatoka Wete anakujakusomesha Mchangamdogo, mtu anatoka Mchangamdogo pengine anakwenda kusomesha Wete ni mtihani. Tunaomba walimu hawa Mhe. Waziri awaone na kuweza kupewa mafao yao mazuri kwa kupata mahitaji tunayoyakusudia.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa sina mengi, nilitaka nizungumze kidogo tu katika wizara hii waziri wangu asije akasema tumenyamaza kimya. Kwa hivyo, naunga mkono mimi na wanawake wenzangu na makundi yote maalum kwa asilimia mia moja na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu amjaalie atamuwezesha tuweze kukwamuka katika kadhia hii.

Mhe. Nassor Salim Ali (Aljazeera): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi hii ndogo kuweza kuchangia japo kidogo hotuba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali mzee wangu Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban. Kwanza nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa kuweza kuandaa mambo mazuri ambayo yamo katika kitabu hiki na nina imani kwamba mambo haya katika kipindi hiki cha mwaka 2011/2012 basi yatatekelezwa kwa ajili ya kuwajenga vijana wetu kielimu na kuinua hali ya kielimu katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, halikadhalika nachukua fursa hii kumpongeza Katibu Mkuu pamoja na Wakurugenzi wote wa Wizara ya Elimu inaonesha kwamba nikiwa kama mjumbe wa kamati ya wizara hii nimeona vile ambavyo makatibu, wakurugenzi pamoja na naibu waziri walivyokuwa bega kwa bega katika utendaji wao katika kutekeleza na kuinua masuala ya elimu katika nchi yetu. Nawapongeza sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina mchango wangu kidogo tu kwanza nitaanzia katika skuli za maandalizi. Mhe. Mwenyekiti, katika taarifa yake Mhe. Waziri hapa ametwambia kwamba katika skuli za maandalizi mimi nasema skuli za

maandalizi ndio skuli za msingi kwa elimu yetu tuliyonayo hivi sasa kutokana na sayansi na teknolojia ambayo tunayo ya elimu. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, skuli za maandalizi kwa kweli ni skuli ambazo tunatakiwa tuzitilia mkazo serikali, wananchi ili kuweza kuinua viwango vya elimu vya watoto wetu.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, katika hotuba hii kwenye skuli za maandalizi serikali ina skuli 29, lakini katika sekta binafsi kuna skuli 215. sasa nataka kumuuliza Mhe. Waziri aliangalie kwa kina suala hili kwa nini serikali au wizara inashindwa kuongeza skuli hizo kwa ajili ya kuinua vipaji vya watoto wetu ili kuwajenga kielimu kwa faida ya nchi yetu hapo baadae. Hata ukiangalia katika asilimia hata 50 au 25 hatujafika, kwa sababu ni skuli 29 ambazo ndizo zimeanzishwa na Wizara ya Elimu na skuli 215 zimeanzishwa na watu binafsi. Mimi nina imani kwamba wizara itakapotilia mkazo kuanzisha skuli nyingi zaidi za msingi basi elimu ya watoto wetu itakuwa na nguvu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika skuli za msingi. Katika Skuli za Msingi katika jimbo langu la Rahaleo jimbo mama hili ningemuomba Mhe. Waziri pale katika jimbo langu katiak sheria ya Makadara wananchi wa Makadara kwa kusaidiana na viongozi wao wameweza kujenga jengo la madarasa ambalo sasa takriban lina miaka mitano lakini wizara haijaona umuhimu au nguvu za wananchi wa Makadara au Rahaleo katika kutia nguvu na wao kuweza kulimaliza darasa lile. Wananchi wamelijenga darasa lile kwa nguvu zao pamoja na kushirikiana na viongozi wao lakini Wizara ya Elimu mpaka sasa haijaliona au haijatilia mkono kuweza kumaliza darasa lile. Sasa ningemuomba Mhe. Waziri hata kama si katika kipindi hiki cha bajeti hii ya mwaka 2011/2012, lakini katika bajeti ijayo ya mwaka 2012/2013 basi aingize pale ili kuweza kusaidiana na wanani pamoja na viongozi kuweza kumaliza madarasa yale.

Halikadhalika katika skuli ya Rahaleo, Mwembeladu, Mwembeshauri ambazo zote hizi zimo katika Jimbo la Rahaleo na nina imani kwamba Mhe. Waziri anafahamu fika historia ya skuli ya Mwembeshauri hata Mhe. Waziri wa Nchi, (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hapa alisoma skuli. Sasa Mhe. Mwenyekiti, skuli ile mimi Mwakilishi kwa kushirikiana na Mbunge tumeweza kuchangia pale lakini bado hadhi yake iko chini, ningemuomba Mhe. Waziri aweze kuwasaidia na kuweza kuiboresha skuli ile pamoja na Skuli ya Rahaleo.

Mhe. Mewnyekiti, ukienda katika skuli ya Rahaleo inavuja, madarasa yale hayakaliki vumbi tupu mpaka tumefika mimi pamoja na mbunge kuweza kuchangia pale shilingi 25 milioni katika skuli ile ya Rahaleo, Mwembeladu na Mwembeshauri. Lakini haitoshi hata kama tumetoa pesa pale kuweza kununua

saruji, matofali, na vifaa vingine pamoja na madeski, lakini bado havitoshi. Ningemuomba Mhe. Waziri zile skuli bado zinavuja na ningemuomba afanye ziara hasa ya kwenda kuangalia, kuna maeneo yanavuja kule, watoto siku za mvua hawakai. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri aangalie kwa jicho la huruma katika skuli zangu hizo za Jimbo la Rahaleo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimpongeze sana Mhe. Waziri na wizara nzima katika kukuza suala la michezo katika skuli. Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 73/74 hapo nitaogelea kwa sababu ni fani yangu hii. Mimi nimefurahi sana kuona taarifa ya kwamba Zanzibar tumeweza kupata ushindi wa kwanza katika mashindano ya Mpira wa Pete, vile vile kupata ushindi wa pili katika Mpira wa Meza na kupata nafasi ya tatu kwa ushindi wa kanda katika kanda hizi 12 kwa hivyo Zanzibar tulipata mshindi wa tatu. Halafu vile vile kuweza kuchagua mchezaji bora au *goal keeper* bora wa skuli zote katika kanda 12.

Kwa hivyo, nampongeza sana Mhe. Waziri na ningemuuliza huyu mtoto ambaye kachaguliwa kuwa mchezaji bora katika mashindano haya amempa zawadi gani ili kuweza kuendeleza kipaji chake na kuthamini ule mchango wake mpaka kuwa mchezaji bora. Mhe. Waziri nataka kujua zawadi uliyompa, hata kama ya kumsomesha au kumpa elimu zaidi, kumruhusu kusomeshwa bure nataka kujua. Kwa sababu ni sifa ambayo kailetea Zanzibar, kwa hivyo ipo haja ya kumpongeza, kumlinda na kumuengaenga ili kuendeleza kipaji chake hiki ambacho ameiletea sifa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo sitaki nizungumze sana kwa sababu mengi yameshazungumzwa, lakini nasema kwa asilimia mia mbili mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Rahaleo naunga mkono ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kuweza kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia Bajeti hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwa leo sina mengi sana ya kuchangia katika wizara hii isipokuwa ni kumpongeza Waziri wa Elimu kwa kuweza kupanga mipango mizuri ya bajeti yake na sisi kuweza kuichangia kwa hivi sasa.

Kwa kweli sina michango mimi isipokuwa nichangie kidogo kuhusiana na Jimbo langu la Koani kwamba lina matatizo mengi kuhusiana na Wizara ya Elimu. Hivi sasa jimbo langu lina matatizo makubwa ya kupatiwa walimu wa sayansi, katika skuli za jimbo langu nyingi utakuta matatizo makubwa ni walimu wa sayansi ukichunguza katika kila skuli utakuta mwalimu mmoja au hamna mwalimu kabisa wa sayansi. Kutokana na matatizo hayo namuomba Mhe. Waziri aweze kutusaidia katika jimbo hili ili tuweze kuwa na walimu

wengi wa kuweza kusomesha sayansi pamoja na vyombo vyenyewe vya kusomeshea sayansi.

Jengine ambalo nataka kuchangia ni katika ukurasa wa 64 kuhusu matatizo ya vikalio vya skuli ya jimbo la kati, jimbo langu la kati hivi sasa skuli zangu nyingi zina matatizo ya vikalio. Ukiangalia katika skuli yangu ya Uzi Ngambwa utakuta darasa moja tu na hivi juzi yeye Mhe. Waziri alikwenda kutufungulia hivyo, alikuta madarasa ambayo hayana vikalio ni mengi sana. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atuangalie sana katika jimbo hili lina matatizo sana ya vikali katika skuli zetu.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri aangalie katika uhamisho wa walimu wanapohamishiwa katika wilaya ama mikoa, apunguze nafasi kubwa ya kuhamisha walimu wa kutoa mikoa kwa mikoa iisipokuwa ahamishe katika wilaya na wilaya kwa usumbufu kwamba wakitoka mikoa kwa mikoa, walimu wengi wanapata matatizo ya mahala mwa kukaa.

Skuli nyingi zimejengwa lakini utakuta hizo skuli hazina nyumba za kukalia walimu. Suala hilo linawapa usumbufu mkubwa walimu kuweza kufika sehemu zao wanazosomeshea na wakenda kwa usafiri wa daladala basi anaweza mwalimu kufika saa 5:00 na saa 7:30 au 9:00 ikifika anatakiwa aondoke. Utakuta wanafunzi muda mdogo wanaoupata wa masomo kuliko muda ambao wanakaa bila ya kupata walimu. Hivyo naomba wanapohamishwa walimu katika skuli iwe ni wilaya kwa jimbo au jimbo kwa jimbo isiwe kutoka mkoa kwa mkoa. Inakuwa ni usumbufu kwa sababu ya usafiri unakuwa ni mkubwa.

Vile vile namuomba Mhe. Waziri katika bajeti yake aichangie na wilaya aweze kupata bajeti ya wilaya hata majimbo. Kwa sababu katika wilaya zetu tunapata matatizo sana ya kuweza kuchangia mambo madogo madogo. Inawezakuwa wilaya haina pesa hata kidogo za kuweza kuchangia jambo lolote, hata kama wana sherehe yoyote au michezo kuweza kuboresha michezo katika wilaya au majimbo. Mhe. Waziri ningeomba na wilaya waweze kupata bajeti ya kuweza kuchangia katika wilaya zao mambo muhimu ambayo yanahitajika.

Mhe. Mwenyekiti, pia namuomba Mhe. Waziri aangalie sana suala la kupata wanafunzi kuweza kufanya michezo katika maskuli. Hivi sasa michezo imeanguka sana katika maskuli sio kama hapo zamani, wakati ilikuwa serikali inategemea sana michezo mingi kutoka kwa wanafunzi na ushindi mwingi tulikuwa tunapata kutoka kwa wanafunzi. Siku hizi hakuna michezo kama ile iliyokuwa ya kawaida kama kufanya mbio nyingi au mipira.

Mara nyingi utakuta mambo ya kukuna nazi ya kinamama na michezo midogo midogo, wakati hakuna katika kimataifa. Wakati tumezowea mambo ya kimataifa ni ile michezo ya mbio au mpira tu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri katika bajeti zake aweze kutoa kipaumbele katika maskuli iwepo michezo kama ile ya zamani iliyokuwepo.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atupatie maelezo ya kuhusu mikopo ya fedha ambayo wanakopa wanafunzi. Kwa sasa utakuta wanafunzi wanakopa mikopo mingi lakini hawapati kupewa hata maelekezo ya vipi watalipa malipo hayo. Hivi sasa kuna mikopo ya zaidi ya milioni 400 imekopwa, lakini bado imeshindikana kurejeshwa kwa serikali kwa sababu wanafunzi hawajapewa mipango mizuri ya kuweza kukopa au kulipa fedha hizo. Hivyo namuomba Mhe. Waziri atakapokuja kufanya majumuisho yake, atueleze ni jinsi gani wanafunzi wanaweza kurudisha mikopo yao ambayo wamekopa kwa muda mrefu haijarejeshwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna wanafunzi wanakwenda *scholarship* nje, fedha ile ambayo ingekuwa inarudi kwa wakati basi kusingekuwa na sababu ya kupelekwa wanafunzi kwenda nje, wakati *scholarship* zile zingefanywa hapa hapa nchini na masomo yale pia yanapatikana hapa nchini, basi ingekuwa hakuna sababu ya kupeleka wanafunzi nje kwenda kupata masomo mengine, wakati hapa tunaweza kusomesha na tumeshafungua vyuo vikuu vingi tu hapa na fedha ile ingebakia hapa kwa faida ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, zaidi ya hayo sitokuwa na michango mingi. Naomba kumuambia Mhe. Waziri kwamba mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Koani tunakubali bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii saa hizi ili nichangie machache katika wizara hii yetu tukufu ya elimu. Kwanza nampongeza Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa hotuba yake nzuri iliyojaa ufasaha mwingi.

Vile vile nampongeza Mhe. Naibu Waziri kwa kutujibu maswali yetu vizuri hapa. Pia nawapongeza na watendaji wote wakuu wa wizara hii na watendaji wote kwa njia moja au nyengine, walioweza kumsaidia Mhe. Waziri kuiandaa bajeti hii nzuri na kutuletea hapa leo tukaweza kuichangia.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwenye *point* basi. Nianze kwenye ukurasa wa 21 unaohusu kujenga skuli za sekondari za ghorofa. Mhe. Mwenyekiti, naipongeza serikali kwa hatua yake hii kubwa ya kuweza kujenga skuli za ghorofa kwenye majimbo ya Kiembesamaki, Kwamtipura, Mpendae

naomba nirudie tena Mpendae pamoja na Kibuteni kwa Unguja. Hii inaonesha wazi kuwa wizara tayari inatekeleza ilani ya chama cha Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kidogo ninukuu hii ilani ya chama cha Mapinduzi katika ukurasa wa 128 kifungu kidogo (7).

Kifungu kidogo (7)

> "kujenga skuli mpya 21 za kisekondari kwa Unguja na Pemba"

Naomba nizitaje zile za Unguja tu.

> "Mhe. Mwenyekiti, zitajengwa skuli za sekondari za Muwanda, Matemwe, Chaani, Dole, Uzini, Paje, Tunguu, Dimani, Kiembesamaki, Kibuteni na Mpendae".

Hili ni jambo zuri na sifa kwa serikali yetu, kwa sababu Jimbo la Mpendae ni jimbo kubwa sana, lakini halina skuli hata moja. Mimi nilikuwa nasema serikali imeliacha yatima jimbo lile halina baba wala mama. Leo nimepata faraja kubwa kwa Mhe. Waziri kulitaja kwenye kitabu chake hapa, basi akija nitamuomba anieleze ni lini jengo lile litaanza, kwa sababu afikirie Jimbo la Mpendae halina skuli ya *primary* wala *secondary*. Hapa angalau serikali itaona imefanya jambo kubwa kwenye jimbo hili ya kutujengea skuli hii. Atakapokuja Mhe. Waziri aniambie ni lini ataweza kunijengea hapa, ili na mimi nikitoka hapa niweze kuwaeleza wananchi wangu kabla sijaitoa ile pesa ndogo ya asilimia sitompa asilimia zote, sitochangia hivyo nitawaachia kidogo wananchi wa Jimbo la Mpendae mpaka atakaponieleza lini ataweza kunijengea ile skuli yangu.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 49 kuhusu taasisi ya elimu ya juu. Mhe. Mwenyekiti, tunaishukuru sana serikali kwa kutufanyia kila njia na kuweza kupata vyuo vikuu vitatu hapa kwetu Zanzibar. Tunadhani chuo cha Chwaka kiko katika matayarisho makubwa ya kupata kuingia katika Chuo Kikuu, nacho vile vile Mhe. Waziri tunakiomba kwa jitihada zako zote ujitahidi ili tuwe na vyuo vikuu vinee, basi angalau na sisi Zanzibar tuwe tunakosha uso wetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye vyuo vikuu pale pana wahadhiri na wahadhiri wale wengine wanafanyakazi kwa muda mwingi, pengine miaka mitano au miaka 10. Sasa tunamuomba Mhe. Waziri labda iundwe *policy*, wanaweza walimu wale kufika miaka mitano au 10 bado tu tunaita ma-*lecture*. Sasa iundwe *policy* basi ili ivilazimishe hivi vyuo kuweza kuwa-*promote* hawa walimu, angalau kuwe na *senior lecture*. Katika vyuo vyetu vingi utaona *lecture*, lakini hakuna

senior lecture. Lakini ukitizama mwalimu huyo anafundisha mpaka miaka 10, sasa huo u-*senior* unatokea wapi. Mhe. Waziri atakapokuja atupe vigezo vya mtu vipi anaweza kuwa *senior lecture*.

Mhe. Mwenyekiti, katika Zanzibar University palikuwa na *course* moja pale inayoitwa P University. Hiyo iliandaliwa mafunzo ya mwaka mmoja kabla ya kuingia University, nafikiri wale Zanzibar University walikuwa wanatujua hasa, kama matokeo yetu ya kidato cha sita ni yaumulshaka. Matokeo mengi sio mazuri, wanapata *point* ndogo wanafunzi wengi.

Sasa programu sasa hivi imefutwa, atueleze basi Mhe. Waziri ni hatua gani zilizochukuliwa hata ikafutwa programu ile. Mimi nataka kusema kuwa hizi bodi imekuwa tayari TCU inaanza kutuchezea akili zetu, itakuwa tayari tuna ndoana hapa kwenye roho yetu.

Mhe. Mwenyekiti, vyuo vyetu vingi vikuu vinahitaji kuwa na walimu wengi na walimu wengine wanatoka nje. Lakini hatujaona mpaka sasa hivi sifa gani ya walimu kutoka nje ambao wanakuja hapa. Wengi wa walimu wale hawalipi *tax*. Kwa fununu tulizokuwanazo sasa hivi mbele ya meza ya Mhe. Waziri, kuna barua ambayo hatuna ushahidi, hizo ni fununu tu. Kuna barua ambayo hatuna ushahidi hizo ni fununu tu, imekwenda kuomba *exemption* ya kutokulipa *tax*. Sasa ikiwa wahadhiri wa kawaida wanalipa *tax*, kwa nini hawa walimu wa kigeni wasilipe *tax*.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu Chuo cha Kiislamu ambacho sasa hivi kimepoteza aiba yake, kimebadilishwa jina na kuondolewa kabisa wahadhiri waliokuwa maarufu pale, hatujui sababu gani hata wahadhiri wale wameondolewa. Tunamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atuambie basi kwa nini hiki Chuo cha Kiislamu kimebadilishwa jina na kimepoteza haiba kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, tunahitaji kupata elimu bora, hatuhitaji kupata bora elimu. Sasa tunahitaji tunahitaji tuelekee katika mfumo wetu bora wa elimu ili kuwanyanyuwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nakuja kwenye ukurasa 57, bodi ya elimu ya juu. Mhe. Mwenyekiti, tuna aina nne za bodi. Tuna (*TCU)*, *Tanzania Commission of University*, tuna NATE, tuna *NECTA* pamoja na bodi ya elimu ya juu ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, tunamuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze ni uwiano gani wa wajumbe wanaoweza kuunda bodi ile ya TCU na wajumbe

gani wanaweza kuunda ile bodi ya TATE pamoja na NECTA. Tunataka tupate uwiano huu ili tujuwe Zanzibar ina faidika vipi katika bodi hizi tatu.

Mhe. Mwenyekiti, NECTA ilipewa kiwanja hapa Zanzibar, iliomba kiwanja ili ijenge ofisi zake Zanzibar, kiwanja kile kilifutwa hatujui vipi. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri atujibu hili NECTA ambayo tulitegemea sana tukipata ofisi hapa, basi wananchi wetu wengi ule umaskini waliokuwa nao wa kufuata vyeti Dar es Salaam na mambo mbali mbali Dar es Salaam utapungua na watatumia ofisi ya Zanzibar. Kwa hivyo, tumesikia hiki kiwanja kimefutwa. Sasa Mhe. Waziri kama ana taarifa hiyo basi aje atueleze kilifutwa kwa nini na lini watapewa tena.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile *Open University* walipewa kiwanja hapa Zanzibar cha kuweza kujenga wameomba tayari, lakini mpaka sasa hivi bado hawajapata kiwanja hichi. Tunahitaji basi kuweza kupata kiwanja cha kuweza kujenga hii *Open University*. Mhe. Mwenyekiti, majengo yakijengwa kuna vitu vingi vinatunufaisha, pamoja na ajira kwa watu wetu. Pia kutakuwa na ofisi nyingi ambazo matawi yake yako hapa.

Mhe. Mwenyekiti, niingie kwenye *vocation training*, kuna vyuo vingi sasa hivi. Sijui wizara ina *policy* gani, kwa sababu vyuo hivi vya mitaani vimekuwa kama utitiri kila kona utakayopita. Mimi jimboni kwangu vinafika vitatu na sisi tunahitaji elimu bora, kweli wizara inafanya utafiti hapa. Basi tunaomba wizara itueleze kuhusu hivi vyuo, kwa sababu vyengine vinatoa diploma. Sawa tunakubali, lakini diploma ya mwaka mmoja haikubaliki.

Mwanafunzi yule hatuwezi kumsaidia kwa diploma ya mwaka mmoja, akishachukua diploma atataka kwenda juu zaidi na *principle* hizi za TCU zinakataa diploma ya mwaka mmoja, tutakuwa hatuwasaidii tunawabomoa. Kwa hivyo, tunaomba akija hapa Mhe. Waziri atueleze ni *policy* gani ambayo inaruhusu vyuo hivi kutoa diploma ya mwaka mmoja na vyengine kutoa chini ya hapo, tunataka tupate elimu bora sio bora elimu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kuna sehemu ya uajiri wa walimu. Kuna Skuli ya Mwachealale. Mhe. Mwenyekiti, ile ni aibu kubwa, skuli ile ila darasa anasomesha mwalimu mmoja, akiumwa basi umeshakuwa mtihani. Sasa kweli kwa njia hii inapatikana ile *quality education*. Mhe. Waziri hebu tuangalie hili, halafu ukija hapa katika majumuisho yako utuambie ni kitu gani unaweza kufanya na vipi utaweza kumsaidia mwalimu mkuu yule wa Skuli ya Mwachealale, ili tuweze kupata hii elimu yetu bora katika kisiwa chetu hiki cha Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nichangie katika ukurasa wa 73 kama alivyochangia ndugu yangu Jazira hapa, nimeona fahari kubwa kwa wanamichezo. Hii taasisi ya michezo kuingizwa katika elimu, hii ndio tuliokuwa tunaitarajia hasa kwa sababu kitu chochote tunaanza *foundation*, hata nyumba tunaanza *foundation*. Kwa hivyo, tumefarajika sana kuona tayari Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ina kitengo cha michezo, tunajua kabisa kwamba tutapata wana michezo bora sasa, wenye hadhi ya juu watakaoweza kuondoa ule ukame wa taifa letu la kukosa wana michezo bora.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni ilipelekwa timu kule Dar es Salaam. Katika kanda 12 sisi tulikuwa wa 3. Hili ni jambo la kururahisha, niipongeze sana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa uamuzi wake huu bora na imara zaidi. Lakini changamoto kubwa ambayo imeikuta hapa, hii timu ilikabiliwa na uhaba wa fedha ilikuwa imekuwa kama yatima inaomba omba tu. Hata wale maofisa wake walisamehe posho ili kuiboresha hii timu. Baada ya kupata ushindi huu mnono, sijui wizara itatuambia imewafikiriaje wale wanamichezo wenyewe pamoja na wale maofisa ambao waliambatana na timu hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo basi nitakuwa sina zaidi ya kuendelea na mimi niunge mkono hoja hii kwa asilimia 90, asilimia 10 nawapelekea wananchi wa Jimbo la Mpendae mpaka nitakapopata majibu ya kuridhisha, basi nitampa swahiba wangu babu Rama hizi asilimia 10 zilizobaki. Nakushukuru sana naunga mkono hoja kwa asilimia 90, ahsante sana.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia mchango mdogo sana katika hotuba hii ya Mhe. Waziri, nikiwa mwakilishi, lakini pia nikiwa Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kusema kwamba naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. Naunga mkono sio tu kwa sababu ya babu Rama, lakini ni kwa sababu ni Makamo Mwenyekiti wa Kamati hii na tunajitahidi kuiboresha hotuba hii, sina haja ya kuikataa kwa sababu mimi ndio niliyemsaidia kuiandaa. Kwa hivyo, naunga mkono kwa asilimia mia kwa mia na nawaomba wajumbe wenzangu waiunge mkono na hata buti zipunguwe sana.

Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba michango ya elimu kwa maendeleo ya Zanzibar na dunia kwa ujumla hapana asiyejua. Elimu ndio kitu ambacho kitasaidia maendeleo yetu na maendeleo ya dunia hii. Kwa hivyo, serikali zote duniani zinawekeza kwenye mchango mkubwa kwenye elimu na ndio maana hata wenzetu nchi za Afrika zikatoa matamko mbali mbali kama yale ya Abuja

kwamba elimu ni lazima ipewe kipaumbele kwenye nchi nyingi na kwenye bajeti zetu za serikali zetu.

Mhe. Mwenyekiti, niishauri serikali kwamba kuna haja sasa yale maazimio ya dunia, kama yale maazimio ya Afrika kule Abuja yangeangaliwa zaidi katika kipaumbele kwamba mchango wa bajeti ya elimu, basi ufikie hiyo asilimia 20 ambayo sasa hivi dunia inaelekea huko. Kuipangia bajeti ya serikali kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ikawa ndogo kiasi hiki, kwa kweli hatuwezi kuwasaidia wenzetu hawa kwa yale malengo ambayo wamejipangia. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naishauri Serikali Kuu kabisa kwamba waendelee kuwekeza zaidi kwenye masuala ya elimu kama ambavyo Mhe Abdalla amesema kuwa sote humu tunatokea kwenye elimu na kama sio elimu basi tusingefikia kwenye maeneo haya tuliyo hapa.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili la elimu linahitaji sana mashirikiano ya jamii, walimu, wanafunzi na serikali. Kwa msingi huo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ina haja sasa kujipanga zaidi kujenga mashirikiano ya wazee, walimu, wanafunzi na jamii kwa jumla kwa ajili yakufikia maendeleo ya kielimu. Katika elimu Mhe. Mwenyekiti, nianze na muundo mzima wa kamati za skuli.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimshauri Mhe. Waziri kwamba tumezowea kamati za skuli kuchaguliwa na wananchi wenyewe, sio jambo baya. Lakini kamati hizi ndizo ambazo zinashauri maendeleo ya skuli na maendeleo ya elimu katika maeneo yetu ya vijijini. Kwa hivyo, nimshauri Mhe. Waziri kwamba kuna haja sasa ya kutoa muongozo maalum kwamba angalau wajumbe wa kamati ya skuli wawe na mwelekeo wa masuala ya elimu, ili waweze kushauri vyema uongozi wa skuli na washauri vyema maendeleo ya skuli kwa maana kwamba wao wawe na uwezo wa kielimu waweze kushauri vizuri kwenye maendeleo ya skuli.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimuombe Mhe. Waziri kwamba kuna haja sasa kwa sababu polisi jamii imekuwa ni muhimu sana kwenye jamii yetu, kwa hivyo kuna haja ya polisi jamii sasa kutolewa muongozi kuwa baadhi yao kuwa wajumbe wa skuli. Kwa nini nikasema hivyo, kwa sababu maskuli yetu yanakabiliwa na changamoto nyingi, inakabiliwa na utoro wa wanafunzi, inakabiliwa na uharibifu wa maeneo na inakabiliwa hata na uharibifu wa mazingira kwa maana ya kutupwa kwa vinyesi na mambo mengine.

Sasa tukiwachanganya polisi jamii nadhani watasaidia uongozi wa kamati ya skuli kuweza kuondosha matatizo haya madogo madogo. Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba tumekuwa na safari za maskuli yetu ambazo wanafunzi

wetu hutoka nje ya maskuli yao na kufanya ziara za kimichezo au ziara za kimasomo, kwa umaarufu wanaziita *study tour*.

Mhe. Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Mhe. Waziri safari hizi ni vyema zingepangiwa ratiba maalum, zikaratibiwa na wizara zikajulikana kwamba skuli gani leo itakwenda *study tour* na tarehe fulani itakwenda skuli fulani. Kwa nini nikasema hivyo. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kuwaachia tu walimu wakapanga *study tour* pasipo na utendaji, nadhani patakuwa na madhara kwa masomo, lakini pia zinaweza zikachangia mmong'onyoko wa maadili ya watoto wetu.

Mhe. Mwenyekiti, namshauri sana Mhe. Waziri kwamba kuwepo na mpango maalum wa safari za masomo ya skuli yetu tena ziratibiwe na uongozi mzima wa skuli, zijulikane kwenye kalenda ya skuli kwa mwaka. Tusiwaachie wanafunzi wetu na walimu wetu wakajipangia safari hizo za kimasomo ambazo zinaweza zikasababisha matatizo mengi.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, ambalo napenda kumshauri Mhe. Waziri ni kwamba kuna haja ya kutoa motisha kwa masomo ya sayansi tena kwa walimu wetu wa sayansi na hata wanafunzi. Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nitowe mfano. Mimi nilipokuwa mwanafunzi nilishiriki kwenye masomo ya sayansi katika skuli yangu na mara ya mwanzo katika Skuli ya Mwambe nilichangia mimi kwa kupewa zawadi ya kushinda masomo haya ya sayansi.

Kwa hivyo, tukiendelea kushajihisha wanafunzi wetu na walimu kutoa motisha na mashindano ya sayansi ni kusema kwamba tunajenga ari ya masomo ya sayansi katika maskuli yetu. Mhe. Mwenyekiti, namshauri sana Mhe. Waziri kwamba mashindano ya masomo ya sayansi kwa maarufu sayansi *cup* zingejengwa kwa Unguja na Pemba zikazidishwa ili tukapata mashindano ya wanafunzi wetu kwa ajili ya kuongeza ari ya mashindano haya ya masomo ya sayansi kwa Unguja na Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo ningelizungumza kwa ufupi naomba kujua tu, kumekuwa na ongezeko kubwa sana Zanzibar kwa maskuli haya yanayopewa majina ya *International School*. Naomba kujua ni nini utaratibu wake wa usajili. Kwa sababu sasa hivi kila ambaye anaanzisha skuli anaipa jina hili kuwa hii ni skuli ya *international*.

Kwa hivyo, naomba kujua ni nini utaratibu wake na kweli maskuli haya yanafikia hadhi ya kuitwa *international school*. Je, viwango vya fedha ambazo Wazanzibari wanalipia vinastahiki au vinalingana na viwango vya maskuli yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu tumegundua kuwa kuna maskuli ambayo yamepewa majina makubwa, lakini hayana maabara, hayana walimu wa kutosha na wala hayana viwanja vya michezo. Lakini majina yetu ambayo tumeyapa skuli hizi ni makubwa na Wazanzibari wetu wanachangia fedha nyingi kwa ajili ya kusomesha watoto wao.

Mhe. Mwenyekiti, wasi wasi wangu ni kwamba mwisho wa siku Wazanzibari watachangia fedha nyingi, lakini kiwango cha elimu kitakuwa ni kidogo sana. Kwa hivyo, Mhe. Waziri ungesimamia maskuli haya ambayo yanatoa majina makubwa, lakini viwango vyake vya kusomesha na hata mazingira yake ni madogo sana.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, ambalo ningezidi kulichangia ni maendeleo ya vyuo vya Kurani. Tumekuwa tukishauri hapa kwamba serikali ifikie wakati sasa walimu na wanafunzi wa vyuo vya Kurani nao kupewa kipaumbele. Tunajua kuwalipa mishahara ni jambo gumu kidogo kwa sababu ni vyuo vingi, lakini angala mngechagua baadhi ya vyuo kama ni *priority project* wakaanza kuwafidia baadhi ya walimu.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu vyo vya Kurani wanatoa mchango mkubwa sana kwa maendeleo ya elimu Zanzibar na hata kwa maendeleo ya dini yetu. Ukiangalia matokeo mengi ya wanafunzi Zanzibar, wanapasi masomo ya dini na Kiarabu. Huu ni mchango wa walimu wetu wa Kuran. Kwa hivyo, kuwaachia walimu hawa bila ya kuwasaidia angalau sababu, kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, bado hatujafanyakazi na naomba serikali iangalie suala hili.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, wanafunzi wetu wamekuwa wakifanya mashindano ya Kuran na wamekuwa wakihifadhi vyema Kuran, lakini baada ya kushinda mshindi wa kwanza, wa pili na watatu na kupewa zawadi pengine baskeli au redio, hapo hatuwezi tena kuwaendeleza. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nadhani hii wizara ingewachukuwa wale wanafunzi wote ambao wanashinda mashindano ya Kurani, wakawapa kipaumbele na wakawaendeleza ili wawe wasomaji wazuri wa Kurani na kwa maslahi ya Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo ningechangia ni suala zima la SUZA. Mhe. Mwenyekiti, tuseme ukweli kwamba kama tunahitaji maendeleo ya kielimu Zanzibar ni lazima tuwekeze katika Chuo chetu Kikuu cha Taifa. Kama serikali inashindwa kuwekeza SUZA ni kusema kwamba serikali imeshindwa kuwekeza kwenye maendeleo ya elimu, bila ya SUZA itakuwa hatuna elimu, kwa sababu SUZA ndio Chuo chetu cha Taifa na ndio ambacho ni tegemeo la Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, bajeti ambayo imepangiwa SUZA ni ndogo, kamati imeona hivyo na hata uongozi wa wizara wameona hivyo, lakini serikali kuu bado haijaamua kuwekeza kwenye SUZA. Mhe. Mwenyekiti, mimi nashauri kwamba bajeti zijazo hii tayari imepita, lakini Wizara ya Fedha na serikali kuu kwa jumla izingatie umuhimu wa kuendeleza *SUZA* leo *SUZA* wanashindwa hata kuajiri walimu wenye sifa, wanashindwa kupata hata *field* mbali mbali kwa sababu hawana fedha za kutosha.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hilo nishauri basi kwamba tafiti zote za serikali nadhani wangeshirikiswa *SUZA* wakazifanya badala ya kutafuta watafiti wengine kutoka nje ya Zanzibar wakapewa jukumu hilo la *fild*, Zanzibar nadhani *SUZA* ndio chuo pekee ambacho kingesaidia serikali hiyo ya kufanya tafiti ambazo zingeleta matunda mazingira na maslahi ya Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti nimalizie kusema tu kwamba Mhe. Waziri bajeti ya mwakani tukijaaliwa nikuombe sana ujenge hoja, ukae na wataalam wako mujenge hoja serikalini kwamba *SUZA* ndio chuo chetu, leo tunaambiwa Zanzibar hatuna walimu wanawake wenye *PHD holdes.* Tumeshindwa kuwapata walimu wanawake kwa nini kwa sababu tumechelewa kuwapata kuwasomesha na hadi hii leo hatujawekeza *SUZA* kwamba lengo ni wanawake kuendeleza, Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Waziri kwamba mwakani ajenge hoja na kamati yetu ipo itaisadia kwamba *SUZA* ipewe kipaumbele kwenye bajeti ya maendeleo na bajeti ya miradi, kwa ajili ya kunyanyua chuo hiki cha Maendeleo Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo niombe kwamba mimi kwa niaba yangu na wananchi wa Zanzibar wa Jimbo la Kiwani niunge mkono bajeti hii mia kwa mia, niombe na wenzangu waunge mkono mia kwa mia Mhe. Waziri awezeshwe ili aweze kuendeleza maendeleo ya elimu Zanzibar. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nimi nikushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii niweze kuchangia macheche katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa hotuba yake nzuri aliyotuletea na kuisoma kwa ufasaha na kuijua Mheshimiwa tunakupongeza sana.

Mhe. Mwenyekiti hakuna asiye fahamu kwamba elimu ndio msingi wa maendeleo na bila ya elimu hakuna maendeleo, niende moja kwa moja katika mchango wangu kwenye ukurasa wa 24 Idara ya Uendeshaji na Utumishi, kwa kweli Idara hii ina majukumu kakubwa sana lakini katika majukumu yake ni kusimamia maslahi ya walimu, Mhe. Mwenyekiti maslahi ya walimu bado ni

madogo sana pamoja na kupandishiwa asilimia 25 kwa watumishi wa umma lakini kwa walimu bado ni tatizo. Tunamuomba Mhe. Waziri awaangalie kwa jicho la huruma.

Mhe. Mwenyekiti, katika Idara hii walimu wamekosa hata vitendea kazi yaani muongozo wa kufundishia, naomba Mhe. Waziri angalau awatafutie hawa waalimu muongozo wa vitabu vya kufundishia ni tatizo kwao, vile vile kuna walimu waliomaliza masomo yao ya ngazi ya cheti, Diploma na Degree na mpaka leo hii hawajabadilishiwa mishahara yao pamoja na maposho yao, hili nitatizo naomba muliangalie kwa jicho la huruma kwa sababu wengine wamechelea mpaka kukata tama na wanaopata aelimu yao kama hiyo huondoka katika nchi yetu na kwenda kufundisha kwengine ni hasara kwa taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, walimu wa sayansi ni tatizo kubwa sana katika maskuli yetu mfano kama skuli ya Kisiwani Kojani Jimbo la Kojani, kuna mwalimu mmoja anayefundisha sayansi tena mwalimu huyu anatoka sehemu za Mchanga Mdogo na anakuja kwa zamu, anakuja siku ya Jumanne na Ijumaa, pengine upepo ukikaza kwenye kivuko pale haji kabisa hili naomba Mhe. Waziri naomba ulichukullia na utupatie walimu wa kudumu pale katika Skuli ya Kojani, ndani ya Wilaya ndogo ya Kojani.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine na hili ni tatizo zinapotoka fursa za kwenda kusoma nje basi hutolewa kwa upendeleo, hasa wanazingatia upande mmoja kwa kweli watu wa Pemba hunyimwa sana fursa hizi, tunaomba katika serikali hii ya Umoja wa Kitaifa ni serikali ya wananchi ambao wana matumaini makubwa wawaangalie na wawachague watu wenye sifa ya kwenda sio kwa upendeleo tu, wanaachwa watu wenye sifa na kuchukuliwa watu ambao hawana sifa hizo. Kwa hivyo tunaomba hili liangaliwe kwa kina

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, mimi na wamanchi wangu wa Jimbo la Kojani mia juu ya mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Ali Mzee Ali: Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia afya njema na kurudi tena ndani ya Baraza hili tukufu, napenda nichukue nafasi hii kumpongeza Mhe. Spika, na wasaidiziri wake Naibu Spika, na wasaidizi wake na wenyeviti wawili wote kwa kuwa ni viongozi wa baraza hili jipya. Vile vile napenda kumpongeza Makamo wa Pili wa Rais ndugu yangu na rafiki yangu Balosi Seif Iddi kwa kuwa ndio kiongozi wa shughuli za Baraza, nawapongeza wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wote wapya, na nawapongeza wajumbe wa Baraza waliorudi tena wote.

Mimi sitokuwa na maneno mengi lakini nitachangia kwa kiasi kidogo, Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali nakupongeza wewe na Naibu Waziri wako na wasaidizi wako wote, Mhe. Waziri wa Elimu ni mtu mzoefu katika serikali yetu hii amekuwa na wizara nyingi sana kama sikosei aliingia humu ndani mwaka 1980 sasa ni miaka 31 yumo ndani ya Baraza hili akifuatiwa na Mhe. Zainab Omar Moh'd nae ni miaka 31 waliobakia wote hawajafika, kwa hivyo ni mtu mzoefu.

Mhe. Rais aliona busara na hekima amkabidhi Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na yeye mwenyewe ni mwalimu, naomba tumsaidie bajeti yake tuipitishe na tumpe kila msaada. Sasa nataka kwenda kwenye mada moja kwa moja.

Katika hotuba ya Mhe. Waziri ukurasa wa 66 ambao unazungumza Kitengo cha Elimu majumuisho ya *feasibility stud* lakini juu kuna kitengo cha uratibu wa Elimu ya Juu, Elimu ya Juu kwa mujibu wa Katiba ni mambo ya Muungano jaduweli ya Katiba 14 elimu ya juu ni ya Muungano, lakini kivitendo elimu ya juu haijafaidika na muungano imekuwa na mzigo Zanzibar kwa miaka yote. Hata tulipoanzisha hiki chuo cha *SUZA* tulianzisha chuo hiki kwa sheria na Baraza la Wawakilishi ndio waliopitisha sheria hiyo, sasa chuo cha *SUZA* ndio Chuo cha taifa wenzetu wa Kenya wakoloni walipoondoka waliwaachia vyuo vikuu, Uganda waliachiwa vyuo vikuu, Tanganyika waliachiwa Vyuo vikuu lakini Zanzibar mapinduzi ya mwaka 1964 Zanzibar kulikuwa na skuli za sekondari 4, mbili za serikali na mbili za kibinafsi.

Sasa tukitaka kupima hatua tuliyofikia tuanzie hapo leo Zanzibar tuna vyuo vikuu vinne lakini chuo chetu kikuu cha taifa ni *SUZA* tuna haki ya kujivunia, tuna haki ya kujiona sana wengi waliomo humu ndani wamesomeshwa baada ya Mapinduzi. Kwa hivyo nyote mliomo ndani wengi elimu zenu mlizipata baada ya Mapinduzi na leo watoto wetu wanasoma katika vyuo vyetu. Sasa *SUZA* kinajitahidi sana lakini chuo hiki bajeiti yake imejenga chuo kipya, kwanza jumbe lile la *SUZA* ilikuwa ni skuli ya Agakhan jumba la wenyewe Agakhan tumelichukua pale, lakini leo serikali inajenga chuo chake na Ishaalla Karibu kitafunguliwa.

Sasa chuo kile katika bajeti yao waliomba bilioni 26 kweli hali ya Serikali ya bajeti ngumu lakini wamepewa 3.6 bilion hizo ndizo walizopewa kibajeti, lakini mwaka jana waliomba bajeti 7.2 bilioni wakapewa 3.4 bilion katika baraza, lakini walichopewa kwa mwaka mzima *SUZA* 2.8 bilion. Wakati Chuo Kikuu cha Dodoma kinajengwa serikali ya Muungano kule ilisema vyuo vyote vikuu vya Bara pale waliwapunguzia bajeti wakazipeleka Dodoma, Dodoma ikakua sasa kama tunataka chuo hiki kwenda hatuwezi kutoa zote 26 bilion

lakini kuna mambo muhimu ambayo lazima Serikali isaidie, sasa hivi bajeti ile ina kasoro *lecture theater* hakuna upanuzi wa *laboratory, conference room, training* za walimu. Sasa naomba serikali isaidie sana.

Lakini *SUZA* mkubwa wake Rais halafu baraza la Chuo wajumbe wake ni Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Katibu Mkuu Mipango, Mjumbe wa Baraza, sasa nafikiri waziri watumie hao na watumie hao wakusaidie na waelewe sisi tumesema, Mhe. Balozi Seif Ali Iddo kwa hapa atatusaidia, Mhe. Omar Yussuf Waziri wa Fedha atatusaidia haya wayaone *special* nataka kusema hilo.

Halafu Makamo wa Pili wa Rais nimefurahi sana na naomba wasaidie mambo ya lugha za kiarabu mimi naunga mkono wazo zuri, lakini *SUZA* inasomesha kiingereza inatoa Diploma na Firs Degree, Arabic Diploma na First Degree, Kirenu Diplomanish Diploma, Kijerumani Diploma, Kifaransa Diploma na Kiswahili kwa wageni. Sasa mimi nasema balozi unawajua watu wengi tumia ubalozi wako, tumia Afisi yako kusaidia *SUZA* kwa njia mbali mbali. Na naamini unao uwezo *(Makofi)*

Mhe. Waziri niliona nikusaidie hapo kidogo niseme hilo lakini jengine katika kitabu cha Mhe. Waziri, kidogo kwenye ukurasa wa 51 nasema 120 kinasema "*Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kiliandaa sherehe rasmi za kumtawaza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Ali Moh'd Shein kuwa mkuu wa chuo cha Zanzibar siku ya tarehe 29 March, 2011, pia Rais amechagua Baraza jipya la Chuo kutokana na Baraza lililopita kumaliza muda wake".* Nafikiri hapo kidogo imekosea iseme Waziri kwa sababu Rais kisheria hawezi kuchagua Baraza la Chuo naomba hapo wafanye marekebisho.

Lakini jengine suala hili la *TCU* hii ina sheria yake namba 5 ya mwaka 2005 mimi ninapata kidogo utata kisheria kwa *TCU* sheria ya *TCU* inasema hivi:-

"*This Act shall apply to Mainland Tanzania as well as to Tanzania Zanzibar".*

Hii ni sheria Namba 5 ya 2005 lakini sheria hii imefuta sheria za vyuo inayosema *This Act 1928* imefuta vyuo vifuatavyo, *Muhimbili University College of health and science Act 1991 na Mzumbe University Act 2001 open University Act 1992, Sokoine University 1984.*

Lakini hawajaweka sheria ya kufuta lakini wanasema sheria hii ina *apply* ya Zanzibar wakati *SUZA* tuna sheria yetu sisi Zanzibar ambayo sasa nimeona mle ndani kunatakiwa serikali ya Muungano au *TCU* ifanye marekebisho katika sheria yake ili itowe utambuzi fulani kwa Rais wa Zanzibar, hili suala la siku nyingi. Sasa wakati umefika Mhe. Waziri hili suala limalizike.

Mhe. Mwenyekiti, kuna Mjumbe hapa kauliza *TCU* ina wajumbe wangapi *TCU* ina wajumbe 18 katika wajumbe 18 wanne tu ndio wa Zanzibar sio haki, lakini sio suala la msingi hili suala la muungano ndio limeandikwa lakini kwa maneno tu kama nilivyosema mambo ya bandari, sasa muhimu serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye umoja wa kitaifa sisi tuishughulikie *SUZA* tujikomboe nchi yetu na elimu yetu kwa faida ya watoto wetu. Na hili jengine wakati umefika sasa niliona hili suala la *TCU* niliweke wazi.

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nafuatilia sana mjadala miezi minane niliyokuwa nje nikasikia wanazungumza hapa baba wa taifa, lakini kuna kitengo kuna *Institute ya* sayansi ya Karume, sasa hivi juzi miaka miwili nilimsika Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais wanataka rekodi na kumbu kumbu za Muungano, wametaka hotuba za Rais wakaambiwa waende *archive* lakini hakuna kule zinakaa nyaraka za serikali. Lakiini iko haja sasa Chuo Kikuu cha *SUZA* na kile cha *Institute* ya Karume kuweka kitu kinachoitwa Kigoda.

Mhe. Mwenyekiti, juzi DK. Moh'd Gharib Bilal alifungua kigoda cha Mwalimu Nyerere pale Chuo Kikuu, kigoda maana yake ni *research* sasa iko haja *SUZA* na *Institute* kule kuanzisha kigoda cha Karume, ampapo pale patafanywa *research* ya Mapinduzi, histroria. Sasa hili naliomba Mhe. Waziri tufungue hivi vitu ili watu wajue historia, sasa kwa sababu nimeona humu leo historia haipo ni miaka 47 ya muungano wetu na miaka 47 ya Mapinduzi sio muda mdogo. Historia lazima muisomeshe tena historia ya kweli leo historia inapotoshwa wazee ndio sisi mimi leo nina miaka 70 nakwenda zangu. Kwa wenzangu humu niliokuwa nao mwaka 2000 wangapi wamekufa kwa hivyo tunaondoka sisi.

Kwa hivyo iko haja Wizara ya Elimu kutengeneza utaratibu kuwa na historia na serikali iweke historia, watoto wetu wajue historia wajue muungano wetu umekuja je, mapinduzi yetu yamekuja je, ukombozi wetu umekuja je. Juzi nilifurahi sana nilikuwa na yule Mfalme wa Ghana sisi na Ghana tulianza zamani tangu mwaka 1958 lakini anasema ameridhika na mfumo wetu huu wa serikali ya kitaifa. Tuone fahari Ghana ndio waliotupatanisha mwaka 1958 ndio wametupatanisha Afro Shirazi na Hizbu ndio Ghana walipatanisha, leo Ghana wenyewe mara kumi wamepinduana sisi leo tuna serikali ya maridhiano na yeye anaridhaia tumefika mabli tushukuru na tuone fahari kubwa, *(Makofi)*

Hivi karibuni mimi nilikuwa Uingereza na Marekani wanasema watu waende Zanzibar wakajifunze, sasa haya yanataka kuenziwa. Kwa hivyo Mhe. Waziri wa Elimu mimi niliona nisaidie kidogo kwenye hizi nyanja mbili tatu ambazo nimeona *sensitive* na serikali yetu ni sikivu na wewe Mhe. Waziri ni mwalimu.

Sasa ndugu zangu wajumbe hii awamu ya sasa hivi baraza hili la sasa hivi hili la miezi minane hizi bajeti zote walizikuta, sasa tuzipitishe tuzihoji, tuzikosoe lakini tuzipitishe. Sisi tuwangojee bajeti ya mwaka 2012/2013 huko ndio tutawahoji, sisi sote humu ndani mfumo huu ambao zamani tulikuwa tunakaa serikali huku na wapinzani kule hata baraza hili tulipolifungua tulikaa hivyo.

Leo ni mara ya mwanzo mimi nilishtuka nikauliza nikae wapi mara nimemuona Mhe.Said Ali Mbarouk amekaa na Mhe. Ali Juma Shamhuna watu walikuwa wako hivi, lakini huu mfumo sisi tuliuona huko mbele yetu watu wakae hivi sasa huku mbele hawa ni Mawaziri sisi ni *back bencher* sote kitu kimoja, wao wajue sisi niwenzao na sisi tujue wao ni wenzetu, tusiwadharau wasitudharau sote ni kitu kimoja inawezekana miaka miwili hii wale wa mbele wakaja nyuma na wa nyuma wakenda mbele inawezekana hiyo*(Makofi)*

Lakini nasema hivi tupendane tuache majungu tujenge nchi yetu nyie ni vijana mmekabidhiwa wananchi wanasikiliza nje huko, kwa hivyo nakuombeni sana mimi kama mzee wenu tukae hapa kwa pamoja tusaidiane na Waziri kuna nafasi nafasi muwape wenzenu, vile vile hii serikali ni mpya wafanyieni safari hao wajumbe wakaone, Ujerumani, Uingereza wakaone mambo yanavyokwenda sio nyinyi peke yenu tu. Baraza lililopita wajumbe walikuwa na *passport* zinakaa miaka kumi hazitumiki ukenda Pemba hakuna mhuri, ukenda Dar es Salaam hakuna mhuri. Akina Moh'd Ali Salim (Mulla) waliuliza *passport* za nini wamekaa nazo miaka kumi hawajenda popote. *(Makofi)*

Naamini chini ya uongozi wa viongozi wa Baraza atatufanyia utaratibu kila watu wakienda mmoja mmoja kwenda kuona ndio kusoma ninamini sana namjua sana naamini atafanya hivyo, lakini subra kwa ufupi sasa nakuombeni kuanzia leo tupitishe bajeti tuzikosoe, tuwaambie lakini mwisho wake tuzipitishe na tushauri lakini tujue kwa hawa tuwangojee huko mbele. Sasa inawezekana huko mbele mwakani unamvizia unakuwa wewe, mimi niliona nipige bashraf kidogo kwa hayo tu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja hii na hotuba hii mia chini ya mia. *(Makofi)*

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Pia nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake kwa hotuba nzuri ambayo wametuletea katika kitabu hichi.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kabla sijaanza kuingia katika mchango wangu naomba nimuhakikishie mzee wangu Mzee Ali Mzee kwamba *indeed backbenchers we are one* na *indeed* tunapenda kwa hilo asiwe na wasiwasi.

Mhe. Mwenyekiti kwa kuendelea nitachangia elimu kwa ujumla. Kwanza kabisa naipongeza wizara kwa *improvement* nzuri ambayo inafanya katika sekta hii ya elimu. Nilikuwa naangalia viambatanisho vya matokeo ya *annually* kila mwaka ninaoangalia naona kuna *improvement*, naipongeza sana wizara.

Pia nikiendelea na mchango huu wa jumla katika elimu naipongeza pia wizara kwa azma yake ya kutaka kuzipatia skuli kompyuta. Pia naiyomba wizara sambamba na hilo isogeze huduma za umeme katika shule ambazo hazina umeme, katika miji yetu na vijiji.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia niipongeze wizara pamoja na Mhe. Waziri kwa kipaumbele ambayo inatoa kwa masomo ya sayansi. Lakini pia wangeliangalia sombo la English wakalipa kipaumbele kwani inaonekana watoto wengi wa kidatu cha nne na sita hufeli kwa sababu hawana lugha. Mimi kwa bahati nzuri nimesoma elimu ya Tanzania hapa Zanzibar ya primary lakini sekondari nilisoma nje ya Tanzania. Lakini hukaa na hawa wanafunzi mara moja moja nikabadilishana nao mawazo. Kwa muono wangu niliouona kwamba wanafunzi hawa hufeli sana kwa sababu masomo yao hawasomi kwa kuelewa husoma kwa kukariri. Ambalo hili ni tatizo.

Lakini kubwa kukariri kwao huwapelekea kutokana na wao kutokujua somo la *English* vizuri au kutokujua kiingereza vizuri. Kwa hivyo naomba wizara iliangalie hili ili wanafunzi wetu wafaulu katika mitihani ya kidatu cha nne na kidatu cha sita.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo naomba niingie katika vyuo vya Madrasa. Mhe. Mwenyekiti, tunaambiwa kwamba elimu ya dunia ni muhimu lakini ya Akhera ni muhimu sana, kwa sababu digirii na *PhD* zetu tutaziacha hapa hapa na *destination* yetu itakuwa *determine* na ile elimu ya Akhera ambayo tunayo. Kwa hilo naiyomba Wizara iangalie kwa jicho la huruma angalau kwa vile vyuo ambavyo viko *register* walimu wetu wa madrasa wanafanya kazi kubwa kuwaelimisha watoto elimu ya Akhera. Lakini pia wanafanya kazi kubwa kuelimisha watoto maadili mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba wizara ingeandaa utaratibu maalum au namna ya kuwaona walimu wetu wa madrasa angalau wengingeanza na hivi vyuo ambavyo vipo *register* wakawa *at list* wanalipwa kitu kidogo. Kwa sababu walimu hawa mbali na kazi wanayoifanya hamna chochote

wanachopata, mchango wa mwezi shilingi mia mia, ananua sabuni anafua kazu. Nilikuwa naomba Wizara hili waliangalie.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niingie kwenye Chuo Kikuu cha Zanzibar, *Zanzibar University.* Nakipongeza sana Chuo Kikuu cha Zanzibar kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya na hii leo Zanzibar tuna *graduate* wengi sana. Lakini siku hizi chuo hiki kinatabia ya kuwatoza wanafunzi in US$, wanafunzi hawa wanapata tatu sana. Wanafunzi hao wanapata tabu sana, hii dola huwa inapanda na kushuka, ikishuka ndio afueni yetu lakini ikipanda huona kama wanalipa kiasi zaidi ya kile ambacho wangekuwa wanalita TZ *Shillings*.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naiyomba wizara iliangalie hilo. Kwanza iangalie kwa nini chuo kina *charge in US$*. Pia kana kuna uwezekano wa chuo hichi kuchukua *fees in TZ shillings* basi wangefanya hivyo, kwa sababu watoto wetu wanasumbuka sana huko mitaani.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nilikuwa nataka nichangie kidogo kuhusu kesi za Ujauzito na ndoa. Mhe. Waziri tunaomba wizara kulisimamia ipasavyo suala hili hasa kwa upande wa watu wa kawaida. Yaani wale watu wa nje ambao wanawapa ujauzito wanafunzi. Tulikuwa tunaomba wizara ichukue hatua kali juu ya watu hawa ili kukomesha vitendo viovu hivi. Kwani tabia hii inarudisha nyuma elimu ya watoto wa kike ambao hupata ujauzito. Sisi tunaamini kwamba ukielimisha mwanamke umeelimisha jamii.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nilikuwa naomba wizara ipige vita sana kwa wazazi ambao huwaozesha watoto wao kabla ya muda. Hili linawanyima haki sana watoto wa kike, haki yao ya elimu na hivyo wanarudisha nyuma jamii.

Mhe. Mwenyekiti, Ahsante sana naunga mkono hoja.

Mhe. Naibu Waziri Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali.

Kwanza kabisa nianze kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri na Katibu Mkuu wake, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikumpongeza Mhe. Waziri. Kwa sababu ya kusema hivyo kutokana na kuwa na mimi natokea Wizara ya Elimu.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu Chuo cha Kiislamu Micheweni. Kwa kweli nimefarijika sana kuona chuo cha Kiislamu Micheweni tangu kilipoanzishwa wanafunzi wengi wanafaulu. Kwa kusema hivyo nampongeza

Mhe. Waziri pamoja na serikali pamoja na watendaji wake wote. Pia nimpongeze Afsa mdhamini Pemba, kwa kuweza kuandamana pamoja na wanafunzi wapo Chuo cha Kiislamu kuweza kuwaelimisha walimu juu ya kusoma kwa uhakika na kupata kufaulu vizuri.

Mhe. Waziri nakupongeza kwa kutembelea mkoa wa Kaskazini Pemba, skuli baada skuli na kutoa elimu inayoweza kuleta maendeleo kwa serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu waheshimiwa wengi wamechangia kuhusu michezo kwa kweli nawaomba waheshimiwa wawakilishi wenzangu wajue kwamba michezo ni afya na michezo ni ajira. Nawaomba waheshimiwa wawakilishi wenzangu kwa kuungana na Mhe. Waziri wa Elimu na Kuungana na Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, suala hili tulipe umuhuhimu mkubwa sana. Kwa sababu ya kusema hivyo juzi tu, tunae mtoto wetu mlemavu wa akili amekwenda nje na kwa kweli amefaulu vizuri kwenye michezo hiyo na amepata nishani ya dhahabu.

Nawaomba waheshimiwa wawakilishi wenzangu tuwe pamoja na Wizara ya Habari, Utalii na Michezo, tuweze kushirikiana pammoja ili kuendeleza michezo yetu Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, kama alivyosema Mhe. Mzee Ali kwa sababu ni mzee wetu, kipindi kilichopita alikuwa anatupa nasaha waheshimiwa na mimi nilikuwa *back benchers*.

Namshukuru sana kwa maneno aliyoyasema, nawaomba waheshimiwa wenzangu kama maneno aliyoyasema mzee wangu tuwe pamoja waheshimiwa, tushirikiane tupitishe bajeti yetu ya Wizara ya Habari, siku ya Jumaane mpaka Jumatano kwa vizuri. Waheshimiwa wenzangu nawaomba sana kwa heshima na taadhima mulipokee ombi hilo la Mhe. Ali Mzee kwa sababu ni mzee wa busara.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kusema hayo mimi pamoja na wananchi wangu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba naipongeza hotuba hii mia kwa mia, ahsante.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nashukuru sana kupata nafasi hii ya kuchangia kidogo tu kuhusu hotuba ya bajeti ya Wizara ya Elimu na Mfunzo ya Amali kwa mwaka wa Fedha 2011/2012.

Kwanza nianze kumpongeza Mhe. Waziri wa wizara hii, Naibu wake na watendaji wake wote kwa umakini walioufanya katika kutuletea kitabu hiki cha bajeti kilichoandikika na kilicho someka na kilichoingiza kila kitu. Hii ni kuonesha kuwa ni wizara ya kitaalamu na ndio wakaweza kutoa kitabu cha kitaalamu kama kile.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo mimi naomba kuchangia kidogo tu. Mhe. Mwenyekiti, tunasomesha watoto wetu tokea madarasa ya chini mpaka madarasa ya juu. Hatimaye tunakuwa na mtihani wa taifa wa Tanzania kuanzia kidatu na nne na mtihani huu unakuwa wanafanya masomo yote, tunasema masomo ya art na masomo ya sayansi.

Mhe. Mwenyekiti, uzoefu wangu katika kuangalia matokeo pamoja na watoto wetu wanachukua masomo yote wanapokuwa mashuleni, lakini matokeo huwa wanapasi sana masomo haya ya art na hasa Kiswahili, kiarabu na siasa. Lakini kwa masomo ya sayansi wanaopasi ni wachache sana na skuli nyengine huwa hazipasishi kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, ninaelewa kuwa Mhe. Waziri hataki apate sifa hii ya kutokuwa na watoto wengi wanapasi masomo ya sayansi kama ilivyokuwa hapo zamani. Lakini kwa makusudi kabisa kwa kuifanya elimu ya darasa la 12 iwe inapatikana kwa kila mwanafunzi tukaongeza madara haya na tukasomesha masomo. Kwa bahati mbaya hatukujitayarisha kuwa na vifaa vya kutosha tunaposomesha masomo haya kama ilivyokuwa hapo zamani.

Matokeo yake watoto wetu wanapofanya mitihani na hasa hivi sasa wanavyofanya *practical* yenyewe sio *alternative* huwa wanafanya mitihani bila yakufanya mazoezi ya yale masomo ya sayansi ambayo wataingia katika mitihani kwa sababu ya ukosekanaji wa vifaa na hivyo husababisha watoto wetu kutokufanya vizuri. Kwa maana hii tunarudi nyuma.

Mimi simlaumu Mhe. Waziri kwa ughali wa vifaa vilivyo hakuna la kufanya. Hivi sasa karibuni watoto wetu wataingia tena katika mitihani. Hivi sasa kuna madarasa yameshafika madara ya 12 na ndio mara ya mwanzo wanafanya mtihani hivi sasa hawajui aina yoyote ya kifaa cha sayansi iwe ni *chemical* au *apparatus* kwa jina hata kwa kuona.

Basi sijui kwa sababu tulisikia hivi karibuni katika hotuba ya Mhe. Rais humu humu katika Baraza letu kuwa kulikuwa kuna makontena ya vifaa vya sayansi vinaletwa. Basi sijui kutokana na ufungufu huu Mhe. Waziri nafikiri yale makontana yameshafika ameyagawa vipi kwa kueneza vifaa hivyo hivyo kwa skuli zilizokaribu, anagalau watu waweze kuvitumia kwa urahisi. Mhe. Mwenyekiti, tumeambiwa kuwa kutakuwa na skuli za sayansi kila wilaya, itakayochukua wanafunzi wengi. Suala ni kuwa skuli hizi zitakapokamilika kujengwe na kufunguliwa hivi vidatu vya nne tulivyokuwa navyo kwa makusudi tulizozifungu katika majimbo mbali mbali ndio zitakufa au watakaoingia katika skuli zile maalum watakuwa ni wanafunzi gani. Hilo naomba nipate jibu.

Mhe. Mwenyekiti, ili tuweze kufanikiwa katika masomo yetu ni pamoja kuona kuwa wanafunzi wanasomeshwa vilivyo na walimu wanasomesha vilivyo na kwa hivyo tunakuwa na ukaguzi. Lakini kwa bahati mbaya kuna skuli na inakuwa ni kawaida yao wenyewao wanasema kupasi kwa mtoto kuingia darasa la kumi na mbili kutoka shule ile basi ni bahati mbaya. Hata baadhi ya shule zina madarasa mpaka ya kumi na mbili, lakini walimu wa shule zile wanawachukua watoto wao kwa wale wenye watoto wao pale au wa jamaa zao, huwapeleka katika shule nyengine na katika uchunguzi tumeona huko katika shule nyengine wanafunzi wale huwa wanafaulu.

Katika utafiti wangu hata hivi karibuni tumesikia kuwa walimu hao hao wamewatoa watoto katika skuli hiyo hiyo darasa la saba kuwapeleka katika skuli nyengine wasome ili waweze kufaulu. Kwa sababu watoto wao hapo nyuma au wanafunzi wenziwao hapo nyuma walikuwa wakifanya mtindo kama huo. Kwa hivyo skuli kama hii iliyokuwa haipasishi mwanafunzi na walimu binafsi wanawaondoa watoto wao wenyewe na kuwapeleka skuli nyengine kwa kiwango kile kile cha elimu. Wizara ina mpango gani ya kufanya uchunguzi wa kina, ukaguzi wa kina katika shule hii ili pafanywe mabadiliko kwa maslahi ya watoto wetu na taifa. Shule zenyewe zikitakiwa ni siri na nitazitaja majina.

Jengine ninaloomba kueleza nilikuwa nashukuru hatua ya wizara inayochukua kuwaelimisha wazee na wanafunzi kuhusu janga zima la ukimwi na halafu pia kutoa ushauri nasaha. Mhe. Mwenyekiti, la kusikitisha ni kuwa sijui walimu wa siku hizi kwa baadhi ya skuli sio wote wanakuwa na maadili gani. Wapo walimu na ushahidi upo wanawapa ujauzito wanafunzi na halafu wanakimbia katika nchi. Mpaka leo sijasikia mwali hata mmoja kupata adhabu kwa kitendo hichi. Sasa ikiwa hata mwalimu anafika kufanya hivyo basi Wizara inamsimamo gani kwa walimu kama hawa ambao wanatakiwa wawe na uwadilifu mkubwa kwa wanafunzi wao. lakini wanafanya mambo ambayo yanakwenda kinyume kabisa na utaratibu wa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, wazee kwa kushirikiana na Waheshimiwa Wawakilishi wao na wabunge wanasaidiana kuisaidia wizara au serikali kujenga mabanda ya skuli kwa ahadi iliyokuwepo kuwa banda likifikia kuezekwa tena Wizara huwa inafanya hiyo kazi. Kuna mabanda mengi yameshajengwa Unguja na Pemba tena mengi sana nab ado hayajaezekwa. Yale mabanda yamejengwa kwa makusudi kuwa tunahitaji kupunguza idadi ya wanafunzi katika madarasa na wanafunzi wasome kwa utulivu. Sijui wizara ina mpango gani wa kuyakamilisha mabanda yale. Msimamo wake ni kuwa tuendelee au kwanza tusitishe kuna mpango mwengine.

Mwisho Mhe. Spika, kwa sababu umenipa muda mdogo wa kuzungumza. Vijana wetu wanajitahidi sana na kusoma. Wengine alhamdulillahi wanapasi kwa kupitia shule tofauti wanazokwenda. Lakini wengine wanajitahidi kwa fedha zao wenyewe mpaka wanafikiwa kiwango cha kujiunga katika Vyuo Vikuu. Kiutaratibu nasikia kuna vigezo maalum unapata mkopo na kuna vigezo maalum vya kupasi inabidi ujitegemee. Mhe. Mwenyekiti, mtoto anajitahidi kujielimisha mpaka akafika kile kiwango cha kuingia kwenye Chuo huku nyuma keshapoteza au keshagharamika vibaya sana hasa kwa Wazazi wao mpaka kuuza vipande vya shamba na kadhalika kwa sababu elimu ni kitu muhimu sana.

Lakini tukifika huku juu tunasikia kuna kiwango fulani cha kufaulu ndio unaweza ukapewa mkopo. Mimi kwa hili naiyomba serikali kwa sababu hawa watoto wamejitahidi sana japo kuwa ni wa *private* lakini wamefikia kiwango cha kufaulu naiyomba serikali ijitahidi kama inavyowezekana ili na wao wapatiwe mkopo licha ya kuangalia ni kiwango gani walichofaulu.

Mwisho Mhe. Mwenyekiti, tuna Vyuo vyetu Vikuu na hasa kiliopo Tunguu. Kile ni chuo muhimu sana na kwa bahati mbaya safari hii fedha iliyoingizwa haifikii kukamilisha malengo yake waliyoyahitajia katika kutoa taaluma. Kwa hivyo kuwa na Chuo Kikuu ni jambo moja lakini kile kinachopatikana kutoka kile chuo ndio kitu muhimu sana. Pamoja na kuwa fedha iliyoingizwa ni kidogo sana lakini kwa sababu Mhe. Waziri ana kila njia ya kwenda hapa na pale ya kupata misaada na kadhalika. Namuomba kile chuo akipe jicho la huruma kuona yale malengo yaliyokusudiwa kufikiwa kwa mwaka huu yamefikiwa ili kiweze kufanyakazi ipasavyo.

Nashukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa na fasi yakuchangia machache katika hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Elimu. Kwanza naomba nimpongeze sana Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara hii mwana mama mmoja mchapa kazi sana, Naibu Katibu mkuu na wafanyakazi wengine wa Wizara ya Elimu. Namna ambayo wanavyoiendesha wizara hii. Ni kweli wanawake wakiwezeshwa wanaweza. Vile ambavyo Mhe. Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara hii wanavyomsaidia na kumshauri Mhe. Waziri wao kama ni wanawake kwa kweli wanamsaidia sana Mhe. Waziri wetu.

Ndio maana ikaonekana maendeleo mazuri katika wizara hii. Kwa sababu ni hii ni wizara muhimu sana katika nchi yetu. Kama walivyosema wenzangu sote

tumepitia katika wizara hii. Kila mmoja anajikumbuka alivyoanza na alivyo leo. Jitihada kubwa iliyofanywa na walimu imetufikisha hapa tulipo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo naomba pia niwapongeze wizara kwa namna wanavyoendeleza ujenzi wa skuli za sekondari 15. Mimi nimepata bahati ya kuzitembelea baadhi ya skuli zinazojengwa. Zinajengwa vizuri na *quality* yake zile skuli ni safi sana, ujenzi wake uko hali ya juu. Ningemuomba sana Mhe. Waziri skuli zile zitakapomaliza basi aandae utaratibu mzuri wa kuzitunza ili ziweze kutumika kwa muda mrefu sana kwa wanaokuja.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwezi wa tano, Mhe. Rais alikuwa na ziara katika Mikoa mitano ya Zanzibar. Miongoni mwa maeneo ambayo aliyatembelea ni sekta ya Wizara ya Elimu, alitembelea siku nyingi Unguja na Pemba katika Mikoa yote mitano. Mimi nilipata bahati ya kuungana na Mhe. Rais katika ziara. Katika Mkoa wa Kaskazini Pemba aliweka jiwe la Msingi katika Skuli ya Msingi Kizimbani Wete.

Maelezo yaliyotoka pale Mhe. Mwenyekiti sote tuliokuwepo pale tulivutika na tuliridhika na jitihada zinazofanywa na walimu pale. Kwa hivyo, kwa niaba yangu naomba sana Mhe. Waziri nimpongeze kwa jitihada zinafanywa pale, lakini pia anipelekee salamu zangu kwa walimu wa skuli ile. Mhe. Mwenyekiti, tuliambiwa kwamba skuli ile kwa muda wa miaka minne mfululizo wameshika ama nafasi ya kwanza au ya pili katika mitihani ya darasa la saba. Haya ni mafanikio makubwa lakini zaidi lilotuvutia umepiga hatua nzuri katika kushika nafasi ya kwanza au ya pili katika masomo ya sayansi hasa somo la Hesabati.

Mhe. Mwenyekiti, hii ni jitihada kubwa na mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri jitihada kama zile zinapaswa kuungwa mkono sana na angalitafuta aina fulani ya zawadi akawapelekea wajione kwamba jitihada yao inaungwa mkono na wizara wenyewe. Mhe. Rais alivutika pale na aliwaahidi ahadi nyingi ambazo tabaan zitakuwa zimeshatekelezwa. Kwa hivyo, na wizara nayo inapaswa kwanza kuwapongeza na kuwazawadia kwa jitihada zao.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nizungumze kwamba miaka ya nyuma kidogo mzee wetu Al-Hajj Aboud Jumbe Mwinyi alikuwa na *vision* moja nzuri sana. Mhe. Mwenyekiti, kwa kuangalia mazingira ya nchi yetu aliteuwa Skuli ya Sekondari ya Fidel Castro kuwa ni skuli ya kilimo. Pia akateuwa Skuli ya Sekondari ya Lumumba akasema kama skuli ya bahari na uvuvi. Muono ule wa mzee wetu aliuweka makusudi kwa kuangalia hali halisi ya nchi yetu na mazingira ya nchi yetu, kama isingewezekana hata kidogo katika nchi yetu tusiwe na mitaala inayohusu na mambo hayo ya kiuchumi. Bahati mbaya hapo kati kati sera yetu ikatuelekeza katika maeneo muhimu ambayo yale tuliyaona

kidogo tuyaweke upande. Mimi namshauri Mhe. Waziri kwamba pamoja na vyuo mbali mbali ambavyo vinafunguliwa, lakini wizara yake ndio wizara ambayo kitaaluma tunaitegemea katika nchi yetu. Na kwamba mitaala ambayo anaielekeza kuisomesha katika skuli zetu lazima ilenge katika yale mambo ambayo yana maslahi ya kiuchumi katika nchi yetu. Katika nchi kama hii ambayo inazungukwa na bahari suala la mitaala ya mambo ya bahari na uvuvi ni jambo muhimu sana. Kwa hivyo, sisemi kwamba turudi kule alikoanzisha Mzee Aboud Jumbe, lakini lazima tuangalie na huko kwamba tuyaangalie mazingira ya nchi yetu halafu vijana wetu tuwaandae katika mambo hayo ambayo *environment* inatuzunguka. Mhe. Mwenyekiti, hilo ni jambo muhimu sana vyenginevyo tutapata tabu sana wakati mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimshauri Mhe. Waziri kuna baadhi ya mitaala ni muhimu kuianzisha halafu watu wanasema udongo uupatize ungali maji. Huu ndio utaratibu wa mambo. Kwa hivyo, kuna mitaala ni muhimu sana katika elimu yetu ili vijana wetu waanze kuondokana nayo tangu wadogo, kuna mambo sasa hivi yanaanza kuibuka halafu yanatupa tabu sana kuyadhibiti. Kwa mfano, suala la madawa ya kulevya, hili ni janga kubwa sasa katika nchi nyingi na hao vijana wengine wanaingia pale tu kwa sababu ya kutojua.

Lakini kungelikuwa na utaratibu juu ya vijana wetu katika mitaala yao wakaanza kujua ubaya wa madawa ya kulevya na bangi, sasa hiyo inakuwa anakuwa anaondokana nayo tangu chekechea, msingi hadi sekondari. Kwa hivyo, sasa imekuwa ni kama sehemu ya masomo yao, lakini kuna wengine ni kwa ujinga wanavuta bangi kwa sababu hawajui. Kwa hivyo, ingekuwa utaratibu wa kufundishwa wangali wadogo wakajua madhara ya bangi na unga kwa kweli tutapunguza kwa kiasi kikubwa sana athari wanazopata vijana wetu.

Mhe. Mwenyekiti, pia kuna tatizo la mazingira nalo ni suala ambalo vijana hasa wale wadogo wadogo wa *primary* wanasoma somo la mazingira, lakini ni kwa kiwango kidogo. Mhe. Mwenyekiti, mabadiliko ya tabia ya nchi ni tatizo hasa sisi tunaoishi katika visiwa, katika ziara hii ya Mhe. Rais tuliyotembelea wenzangu wanakumbuka maeneo ambayo tumetembelea, miaka mitatu au minne nyuma ilikuwa ni maeneo watu walikuwa wanalima mpunga, leo imekuwa watu wanatafuta vitoweo. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba maji ya bahari yameshaingia katika mabonde hilo ni tatizo kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, yote hii ni kwa sababu ni taaluma ndogo katika masuala ya kuhifadhi mazingira yetu. Hili jambo huwezi kuliacha mpaka kijana keshamaliza *Form two* ukamwambia nikufundishe mazingira, huyo ndiye mtu wa kwanza anayeharibu mazingira. Kwa hivyo, taaluma hii Mhe. Mwenyekiti, hasa sisi ambao tunaishi katika nchi za visiwa ni jambo la msingi sana.

Nilikwenda eneo moja limechimbwa matofali yaani pana nyumba ile nyumba ni kama sijui kisiwa, huku kumechimbwa matofali kama pima nne chini na ukuta wa pili vile vile na huko nyuma vile vile. Kwa hivyo, mtu anaingia mlango wa mbele tu. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine yanayozungumzwa hali ya maisha, lakini ni kwamba kuna taaluma ndogo juu ya masuala ya mazingira. Hii lazima kabisa tufanye utaratibu wa Mhe. Waziri wa Elimu najua hili akikaa na wataalamu wake wataweza kupanga namna gani mtaala wa mazingira uingizwe katika skuli tangu *primary* ili vijana wetu wakue na namna gani ya kudhibiti mazingira ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, jambo jengine ambalo pia linaweza likaingizwa katika mitaala yetu ni suala la utalii. Wenzetu utalii hawasubiri mpaka vijana wakamaliza *Form four* hawana kazi ndio wakenda wakaingizwa katika vyuo vya utalii. Kwa kweli haiwezekani ile *hospitality* inajengwa tokea vijana wako katika skuli.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nakusudia kusema kwamba Mhe. Waziri anafanya kazi moja muhimu sana na kubwa sana, nampongeza sana kwa hilo lakini ningemshauri kwamba kuna baadhi ya mambo ambayo lazima ayaangalie kwa maslahi ya nchi yetu na kwa mazingira ya nchi yetu. Kwa sababu sisi mazingira yetu yanatofautiana na mazingira kama ya Tanzania Bara, Kenya na Uganda lazima mtaala ambao unasomeshwa uwe unalenga katika kuangalia mazingira yetu na namna gani vijana wetu wataandaliwa kupambana na hali halisi ya mazingira.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwamba ni kweli kuwa katika majimbo yetu wananchi wetu wamefanya kazi moja kubwa sana yakujenga madarasa. Na madarasa yamekuwa mengi sana kiasi ya kwamba tukimtegemea Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali na bajeti yake hii kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, mimi nilipotembelea nimeona ile *load* iliyopo ni kazi kubwa sana. Kwa hivyo, sisi Wawakilishi na Wabunge tunasaidiana na wananchi wetu kuyafikisha pale yalipo, mengine yamekaa miaka mitano, sita yanasubiri. Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba kila skuli kuna madarasa, sio jimbo kila skuli Mhe. Waziri hayawezi yale maana kwa bajeti hii niliyoiona japo kuna mabilioni lakini kwa kweli tukimlazimisha kwamba na mimi skuli yangu itakuwa tabu sana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina skuli saba katika jimbo langu na yote madarasa yamebakia, sasa Mhe. Rais katika ziara hii aliamrisha jambo moja zuri lakini sijui namna gani utaweza kulitekeleza. Yeye katika ziara zote alikuwa anahimiza kufufua moyo wa kujitolea na alianzisha utaratibu harambee. Kwa mfano, katika Jimbo la Chambani kama sikosei harambee ambayo Mhe. Rais aliianza pale alikuwa akishaambiwa kwamba banda letu hili lishakuwa tayari

anamuuliza Mwalimu Mkuu wewe umetoa ngapi, Mwenyekiti, wa Kamati ya Skuli umetoa ngapi? Akasema mambo hayendi hivi hebu tuanzeni harambee hapa. Mhe. Mwenyekiti, zilipatikana karibu milioni 26 kila mwananchi aliyekuwa pale japo shilingi mia ilikuwa inachukuliwa. Kuna bibi mmoja alijifungua akasema hii shilingi hamsini akaambiwa inafaa hiyo mama. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, utaratibu ule ni mzuri na kwa kweli unaweza kutusaidia sana. Kwa hivyo, suala la mwenye kujitolea na suala la kuchangia tulijitahidi sana. Mimi nakusudia baada ya bajeti hii kumualika Mhe. Ismail Jussa Ladhu katika jimbo langu naamini fasaha yake ya kuzungumza na ushawishi wake mbele ya jamii, akisimamia harambee ya Skuli ya Gando nitaondoka na kitita kizuri cha fedha. Mhe. Mwenyekiti, hili jambo ambalo nafikiria tulianzishe na Mhe. Rais ameshalianza na sisi wachini yake Mawaziri, Wawakilishi kwa kweli tunaweza kuisaidia sana jamii yetu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo nakushukuru sana na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Gando naunga mkono hoja hii ya Mhe. Waziri mia kwa mia.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe na mimi nachukua fursa hii vile vile kuwashukuru Wajumbe wote kwa utulivu na kwa michango yao iliyo makini naamini kwamba Jumatatu tutaipitisha bajeti hii, na baada ya kusema hayo machache naomba niwakumbushe Waheshimiwa Wawakilishi kuwa Jumapili tuna semina ya mifugo na uvuvi, semina itaanza saa 3:00 asubuhi lakini tunatakiwa kujisajili saa 2:30 asubuhi. Baada ya hayo naahirisha kikao hiki hadi siku ya Jumatatu saa 3:00 asubuhi.

(Saa 1:45 usiku Baraza liliahirishwa hadi tarehe 18/07/2011 saa 3:00 asubuhi)